Nipashe
Jumatatu Februari 24, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580162
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
The Guardian digital
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US



## Wasafirisha wagonjwa, maiti kwa machela na bodaboda

UKURASA 21




UKURASA 13

# Bashiru sasa awageukia waliorejea CCM



UKURASA 2




Mkazi wa Mwenge wilayani Kinondoni jijini Dar es Salaam, akiondoa mabati kwenye moja ya mabanda yanayomilikiwa na tawi la CCM kwa ajili ya kupisha ujenzi wa kituo cha mabasi kwenye eneo hilo ambao unakwenda sambamba na upanuzi wa barabara ya Mwenge-Morocco. **PICHA: SELEMANI MPOCHI**

## Watiwa mbaroni tuhuma mauaji bodaboda

UKURASA 21

## Hatima ya Tundu Lissu kesho

UKURASA 2



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
GET IT ON Google Play
Download on the App Store

**MICHEZO** **LUSAJO AMKIMBIZA KAGERE KIMYA KIMYA** UK.31 **MAONI, KATUNI** UK.6

# HABARI KITAIFA



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Azzan Zungu, akisisitiza jambo katika mkutano wa majadaliano uliowakutanisha wazalishaji, wasambazaji, waingizaji na wauzaji wa mifuko mbadala kwa lengo la kujadili changamoto ya biashara hiyo na kuwaelimisha juu ya uzingatia wa sheria na kanuni. Kushoto ni Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Dk. Samuel Gwamaka. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Bashiru awageukia waliorejea CCM

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally, amewataka wanachama ambao walikihama chama hicho na hivi sasa wameamua kurejea wasiwe chanzo cha kuanzisha makundi ndani ya chama.

Amewataka wanachama wa CCM kuwasamehe wanachama hao wanaorejea kwa sababu wamekubali kukiri makosa yao.

Aliyasema hayo wilayani Masasi mkoani Mtwara alipokuwa akizungumza na wanachama wa chama hicho Jimbo la Ndanda na maeneo mengine ya mikoa wa Mtwara na Lindi kwenye hafla ya kumpokea rasmi aliyekuwa Mbunge wa jimbo hilo Chadema, Cecil Mwambe, aliyejiunga na CCM.

"Muwasamehe wanachama wote ambao walikihama chama na hivi sasa wameamua kurejea kwa vile wamekubali kukiri makosa yao," alisema Dk. Bashiru na kuongeza:

"Lakini kurudi kwao ndani ya CCM kusiwe chanzo cha makundi ndani ya chama, kwa kuwa CCM siku zote haina utamaduni wa kuishi kwa makundi. Aidha na wao wanapaswa kusamehe yote yale waliyoyafanya na kutoruhusu tabia ya uwapo wa makundi."

Akipokea kadi ya Chadema kutoka kwa Mwambe na kumkabidhi kadi ya CCM, Dk. Bashiru alisema kurejea kwa Mwambe CCM ni wazi kuwa Jimbo la Ndanda linakwenda kukombolewa. Dk. Bashiru alimtaka Mwambe kurudi na wanachama wengine ambao awali walikuwa CCM, lakini walikimbilia Chadema kwa ajili ya kumfuata mbunge huyo.

Kwa upande wake Mwambe alidai jambo pekee ambalo limemfanya arejee CCM ni namna chama hicho kinavyotekeleza miradi mikubwa ya maendeleo kila sehemu ya nchi.

Alidai katika kipindi cha miaka minne aliyokuwa ndani ya Chadema hakuwa na uhuru wa kutoa mawazo yake, hivyo kushindwa kuwatendea haki wananchi wa Jimbo la Ndanda.

Akiwa kwenye ziara katika mikoa ya kusini, Dk. Bashiru alisema kuwa ameridhishwa na utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika mkoa wa Mtwara ukiwamo wa upanuzi wa Bandari ya Mtwara pamoja na ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Kusini.

Dk. Bashiru alisema licha ya kuridhishwa na miradi hiyo, lakini ipo baadhi ya miradi ambayo inaonekana kutofanywa vizuri kama ilivyokusudiwa katika utekelezaji ambayo ni ujenzi wa barabara pamoja na ukarabati wa uwanja wa ndege.

Alisema miradi hiyo haijatekelezwa vizuri na yeye kama Katibu Mkuu wa chama ameshapokea taarifa ya kusuasua, na taarifa hiyo ataiwasilisha kwa Mwenyekiti wa chama hicho, Rais John Magufuli, ili aifanyie kazi.

Alisema serikali imekuwa ikitoa fedha nyingi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kupitia ilani yake, hivyo chama kinataka kuona miradi hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

**INTERNATIONAL HEALTH PARTNERS JEMA TANZANIA**

**VACANT POSITIONS FOR EMPLOYMENT**

**ZINGA CHILDREN'S HOSPITAL** is seeking experienced, dynamic and competent people to fill in vacant people to fill in vacant positions as follows;

**GENERAL PRACTIONER (MD) (1 POST)**
Interested applicants must possess good interpersonal skill and must be registered with relevant professional body.

**HUMAN RESOURCES MANAGER (1 POST)**
Interested applicants must possess good interpersonal skill and must be registered with relevant professional body.

**DENTIST (1 POST)**
Interested applicants must possess good interpersonal skill and must be registered with relevant professional body.
Interested applicants should submit a letter of application for employment attaching Curriculum Vitae together with names and addresses of two referees to reach the undersigned within fourteen days after the first appearance of this advertisement.

**INTERNATIONAL HEALTH PARTNERS-JEMA TANZANIA**
**CHILDREN'S HOSPITAL, ZINGA**
**P.O BOX 246**
**BAGAMOYO**
**www.ihp-jema.or.tz, info@ihpjema.or.tz**

215642302

## Hatima ya Lissu kesho

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MAHAKAMA Kuu kesho itaanza kusikiliza maombi ya aliyekuwa Mbunge wa Singida Mashariki, Tundu Lissu, kumruhusu kwenda Mahakama ya Rufani kupinga uamuzi wa Spika wa Bunge, Job Ndugai, kumvua nafasi ya ubunge wa jimbo hilo.

Juni 20, mwaka jana, Spika alitangaza kumvua Lissu ubunge kwa madai ya kutotimiza masharti ya kuendelea kuwa mshiriki katika shughuli za Bunge.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Arusha, Msemaji wa familia ya Lissu, Wakili Alute Mughway, alisema Mahakama Kuu Masjala ya Dar es Saalam, Februari 25, mwaka huu, itasikiliza maombi ya Lissu, endapo atakubaliwa kwenda Mahakama ya Rufani kupinga uamuzi wa kuvuliwa nafasi yake ya ubunge.

Mughway alisema, Lissu alipeleka ombi hilo Septemba mwaka jana dhidi ya Spika Ndugai kumvua nafasi yake ya ubunge na kutangaza Jimbo la Singida Mashariki kuwa wazi.

Septemba 9, 2019, Mahakama Kuu, ilitupilia mbali ombi la Lissu la kupinga kuvuliwa ubunge.

Akitoa uamuzi huo, Jaji Sirilius Matupa, alisema maombi ya Lissu hayatekelezeki kwa sababu mleta maombi alitakiwa kufungua kesi ya kupinga uchaguzi mahakamani, badala yake alipeleka maombi ya kutaka kupinga uamuzi wa Spika.

"Mahakama imepata wakati mgumu sana katika kupitia maombi haya," alisema Jaji Matupa na kuongeza kuwa, kama maombi ya Lissu yakikubaliwa yatasababisha uvunjaji wa Katiba kwa kuwa italazimika kuwa na wabunge wawili kwenye jimbo moja, pia maombi hayo yalichelewa kufikishwa mahakamani.

Msemaji huyo wa familia, Mughway, alisema Lissu, hajaridhishwa na uamuzi wa Mahakama Kuu, hivyo amepeleka maombi mengine kuruhusiwa kwenda Mahakama ya Rufani kutolea uamuzi kama hukumu ya Jaji Matupa ni sahihi kisheria.

Alisema maombi hayo, kwa mara ya kwanza yalitajwa Desemba mwaka 2019, na Februari 25, mwaka huu yatakwenda kusikilizwa.

Akizungumzia Lissu kurejea nchini kutokana na kukamilisha matibabu yake, alisema atarudi baada ya muda kidogo, kwa kuwa anasubiri uchunguzi wa mwisho wa madaktari kuangalia kama matibabu aliyopewa yamekidhi viwango.

Licha ya kuzungumza hayo, alisema Lissu alikuwa na mpango wa kurejea nchini kuendelea na shughuli zake, lakini kinachomkwamisha ni kuhofia ulinzi na usalama wake.

"Mtakumbuka mwaka 2018, kuna mtu aliandika katika mitandao ya kijamii kuwa akirudi safari hii hatutakosea shabaha," alinukuu Mughway.

"Mimi kwa niaba ya familia nililalamika kwa nini mtu anatishiwa maisha kwamba atauliwa, kosa hili ni la jinai na tulipotoa taarifa kwenye vyombo vya usalama tuliambiwa tuende mahakamani kwa kuwa aliyeandika hivyo, alikuwa anatoa maoni yake kama raia," alidai.

"Kama mlivyomsikia Lissu kwenye vyombo vya habari amesema hawezi kurudi nchini, hadi hapo atakapohakikishiwa usalama wake na sisi kama familia, ndugu, jamaa na marafiki ndio tulimemwambia asirudi," alisema.

"Katika mazingira haya hawezi kuja tumemwambia sisi familia hatutaki atuachie watoto na mjane asubiri hadi hapo usalama wake utakapokuwa vizuri," alisisitiza.

## HABARI KITAIFA

# Serikali yaridhishwa sekta ya madini

**Na Enock Charles**

SERIKALI imesema inaridhishwa na mchango wa sekta ya madini katika kuchangia Pato la Taifa mwaka 2019/2020 baada ya sekta hiyo kuchangia kwa asilimia 15.7 katika nusu ya kwanza ya mwaka huo.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alisema ilichangia Pato la Taifa kwa kiasi cha Sh. bilioni 242.53 sawa na asilimia 55 ya lengo la serikali la kukusanya Sh. bilioni 478.89 kwa mwaka huo wa fedha na kuwa sekta ya pili kuchangia pato hilo baada ya ujenzi iliyochangia kwa asilimia 16.

"Katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2019/2020 mchango wa Sekta ya Madini ulikuwa kwa asilimia 15.7 ikiwa ni sekta ya pili kuchangia pato letu la Taifa baada ya Sekta ya Ujenzi," Waziri Mkuu Majaliwa alisema.



Pia alisema ongezeko hilo linaloridhisha limetokana na mauzo na machapisho ya kibaiolojia ya madini, ada mbalimbali za leseni za madini, mauzo ya madini yenyewe, ukaguzi wa maabara na ada za mwaka za madini.

Alisema kwa sasa serikali imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kudhibiti utoroshwaji wa madini nje ya nchi kwa kushirikiana na vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama na pia kuanzishwa kwa masoko ya madini ili kuwawezesha wafanyabiashara wa madini nchini na nje ya nchi katika mikoa 27 na vituo video 28 kote nchini jambo lililochangia kupunguza uhalifu katika madini.

Kadhalika, alisema kwa sasa masoko ya madini yana ulinzi na usalama wa kutosha na sifa zote zinazohitajika kimataifa za uendeshwaji wa masoko ya madini jambo lililochangia kushamiri kwa biashara hiyo pamoja na kuimarishwa kwa Sera za Madini ikiwamo marekebisho ya Sheria ya Madini, kufutwa kwa baadhi ya kodi jambo lililowezesha Watanzania kuchimba madini wenyewe na si kufanya udalali.

Naye Waziri wa Madini, Dotto Biteko, aliwataka wachimbaji wa madini kupendana ili kuimarisha ustawi wa sekta hiyo badala ya kugombana wenyewe kwa wenyewe jambo alilosema linachangia kwa kiasi kikubwa kuwarudisha nyuma kimaendeleo.

"Kwa sasa huwezi kutenganisha migogoro na wachimbaji wadogo haitakiwi lazima kuwa na furaha na mafanikio ya jirani yako," alisema Waziri Dotto.

"Unakuta kuna chuki kubwa dhidi ya wawekezaji wakubwa tena wazawa...ooh anatunyonya...anatunyonya ukienda kuchunguza hamna kitu."

# Waliokumbwa mafuriko waomba msaada mbegu

**Na Ashton Balaigwa,** KILWA

WANANCHI wa kaya 3,774 zilizopatwa na mafuriko katika vijiji vya Njinjo, Mitole, Kiranjeranje na Kikole, Wilaya ya Kilwa, mkoani Lindi wameiomba serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali kuwasaidia mbegu za mazao mbalimbali yanayokomaa kwa muda mfupi ili waweze kupanda na kujinusuru na baa la njaa baada ya mazao yao kusombwa na maji.

Ombi hilo limetolewa na Mbunge wa Jimbo la Kilwa Kusini, Selemaini Bungara maarufu Bwege kwa niaba ya wananchi hao baada ya kupokea msaada wa mbegu bora za kisasa za mihogo, mahindi, alizeti na choroko zilizotolewa na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (Tari Ilonga), iliyopo wilayani Kilosa mkoani Morogoro.

Mbunge huyo alisema pamoja na serikali kutoa misaada mbalimbali ikiwamo ya kibinadamu, kwa sasa wananchi hao waliopatwa na mafuriko mahitaji yao makubwa ni mbegu ya mazao ya muda mfupi ili waweze kupanda tena kipindi hiki cha mvua. "Nawasilisha ombi hili kwa niaba ya wananchi wangu waliopatwa na maafa haya kutokana na mafuriko, tunawashukuru Tari Ilonga kwa msaada wa mbegu mlizoleta, lakini bado kuna mahitaji makubwa, tunaomba serikali isaidie hili kwa kuwa wasipopatiwa hivi sasa baadaye tutalazimika kuwatafutia chakula," alisema.

Mkurugenzi wa Tari Ilonga, Dk. Joel Meliyo, alisema wanasaidia wananchi hao waliokumbwa na mafuriko baada ya mazao waliyopanda kuchukuliwa na maji.

Dk. Meliyo, alisema kiwango cha mbegu kilichotolewa ingawa hakitaweza kukidhi mahitaji kwa wakazi wote, Tari Ilonga wameona ni vyema kuwasaidia ikiwamo mbegu ya alizeti na choroko ambayo hailimwi katika ukanda huo, ili waweze kuwa na zao mbadala badala ya kutegemea mahindi na korosho pekee.

Akizungumza baada ya kupokea msaada huo, Mkuu wa Wilaya ya Kilwa, Christopher Ngubiagai, alipongeza Tari kwa kusaidia mbegu hizo wananchi ili waweze kupanda mazao mengine baada ya yaliyokuwapo kusombwa na maji na kuwafanya wananchi hao kuwa na uhitaji wa chakula.

Ngubiagai alisema, wameanza kutoa bure viwanja vilivyopimwa kwa ajili ya kaya zilizokumbwa na mafuriko ili kuanzisha makazi mapya na kwa kuanzia jumla kaya zaidi ya 1,700 kati ya 3,774 zimeshapatiwa maeneo ya makazi mapya.


**TAARIFA KWA UMMA | BANK OF AFRICA TANZANIA YAFANIKISHA MKAKATI WAKE WA KUIMARISHA NA KUBORESHA BIASHARA ZAKE NCHINI TANZANIA**

Inapatikana Nchi 31 na mabara manne

NAFASI YA TATU KWA UKUBWA NCHINI MOROCCO KWA MTAJI WA JUMLA

Bilioni $31 MTAJI WA JUMLA WA BANK OF AFRICA GROUP

Faida baada ya kodi ni milioni $294 kufikia 2018.

ZAIDI YA WAFANYAKAZI 15,200

Mtandao mkubwa, kukiwa na sehemu 1,675 za kutolea huduma

BMCE, yenye makao makuu Casablanca, Morocco

BANK OF AFRICA Groupe BMCE BANK

*As strong as a group As close as a partner*

Bank of Africa Tanzania Limited, inapenda kuwahakikishia wateja wake na wadau wake wote kuwa iko madhubuti kutekeleza mipango yake ya kuendesha biashara zake kwa ufanisi zaidi nchini sambamba na kutoa huduma bora na za kisasa. Tunawashukuru wateja wetu na Serikali ya Tanzania kwa kutupatia ushirikiano mkubwa katika kipindi chote cha miaka 13 tangu benki yetu ianze kutoa huduma za kibenki nchini

Hadi kufikia mwishoni mwa mwaka jana, benki yetu ilikuwa na mtaji wa kutosha unaotakiwa kwa kutoa huduma za kibenki nchini. Hesabu za benki zilionyesha ilikuwa na mtaji wenye uwiano wa asilimia 17% dhidi ya unaotakiwa na mamlaka ya udhibiti wa mabenki wa asilimia 14.5%. Katika cha mwaka 2019, wamiliki wa benki waliongeza mtaji wa Shilingi Bilioni 22.9 kwa lengo la kuiwezesha kutoa huduma ya mikopo na kuboresha huduma. Benki ina mzunguko mzuri wa mtaji unaofikia uwiano wa asilimia 33% dhidi ya mtaji unaotakiwa na mamlaka ya udhibiti wa asilimia 20%.

Mtaji wa jumla wa benki ulikua kwa asilimia 23% katika kipindi cha mwisho wa mwaka 2019 na kufikia Shilingi Bilioni 564, mafanikio hayo yalitokana na ongezeko la akiba za wateja na huduma za mikopo. Huduma za mikopo zilikua kwa asilimia 4.4% na kufikia Shilingi Bilioni 277 mwishoni mwa mwaka. Mikopo mingi iliyotolewa ililenga kuwezesha makundi ya biashara ndogo na za kati, lengo likiwa ni kufanikisha kukuza uchumi wa nchi. Ongezeko la akiba za wateja lilikuwa kwa asilimia 17.5% na kufikia Shilingi Bilioni 390 na ongezeko la fedha za mtaji kutoka kwa wamiliki wa Benki uliongezeka kutoka Shilingi Bilioni 68 mwaka 2015 na kufikia Shilingi Bilioni 74 mwaka 2019.

Hadi mwishoni mwa mwaka 2019, benki ilipunguza uwiano wa mikopo chechefu kufikia Shilingi Bilioni 12 ambayo ni asilimia 9.2% kulinganisha na asilimia 16% ya mikopo hiyo iliyokuwa nayo katika kipindi cha kufikia mwishoni mwa mwaka 2018, kiwango hiki kiko chini ya kilichozoeleka kwenye soko cha asilimia 10%. Mikopo chechefu hadi mwishoni mwa mwaka ilipunguzwa kwa zaidi ya asilimia 90%.

Benki imekuwa ikipata faida katika kipindi cha miaka 5 kuanzia mwaka 2015. Faida iliyopatikana baada ya kulipa kodi ni kiasi cha Shilingi Bilioni 12 katika kipindi cha miaka 3 kuanzia 2015 hadi 2017, ambayo ilitokana na ukuaji wa uendeshaji wa huduma za kibenki kila mwaka kwa asilimia 9% au Shilingi Bilioni 47. Katika kipindi cha mwaka 2018 na 2019,benki ilifanya jitihada za kuhakikisha huduma za mikopo zinaboreshwa,mchakato huo katika kipindi hicho cha mpito uliathiri faida ya benki.

Kwa kuelewa umuhimu wa kujumuisha wanachi kiuchumi, Bank of Africa Tanzania Limited, mwaka jana ilifanya uwekezaji mkubwa wa zaidi ya dola za Kimarekani milioni moja katika miundombinu yake ya Teknolojia ya Habari (TEHAMA) kuwezesha huduma zake kupatikana kwa wateja kwa urahisi. Benki imeweka kufunga mashine za kutolea fedha (ATM) za kisasa katika mtandao wa matawi yake yote nchini,i meanzisha huduma za kibenki za kidigitali na kuimarisha utunzaji wa taarifa zake kwa njia za kisasa zaidi.

Bank of Africa Tanzania Limited ambayo iko chini ya kampuni mama ya Bank of Africa Group, yenye mtandao wa biashara za mabenki katika nchi 18 za Afrika, itaendelea kutoa huduma bora kwa wateja wake wa makundi mbalimbali kuanzia makampuni makubwa,wafanyabiashara wadogo na wa kati kupitia mtandao wake wa matawi 25 yaliyopo katika mikoa 11 nchini Tanzania. Bank of Africa Group, imekuwa ikishiriki kukuza biashara barani Afrika kuanzia mwaka 1985 na Bank of Africa Tanzania Limited itaendelea kufanikisha ajenda hiyo kupitia mpango mkakati wake wa miaka mitatu unaoanzia mwaka 2019 - 2021.

Baada ya kufanikiwa kuichukua benki iliyokuwa ikijulikana kama EURAFRICAN Bank, mnamo mwaka 2007, Bank of Africa imewekeza kwa kiasi kikubwa nchini Tanzania,na kubuni huduma za kisasa za wateja zinazokubalika nchini kote.

Benki inajivunia kuendelea kupata mafanikio kutokana na kuwa chini ya kampuni mama kubwa ya BMCE BANK OF AFRICA, ambayo inaendesha shughuli za kibenki kwa mafanikio katika nchi 18 za Afrika. Kampuni ya Bank of Africa Group, imekuwa katika biashara kwa miaka ipatayo 36 sasa kiwa na mtandao wa matawi zaidi ya 560 na mtaji wa rasilimali unaofikia Euro Bilioni 7.6 ambao umekuwa ukikua mwaka hadi mwaka pia kampuni mama imekuwa na mikakati ya kuendesha biashara zake katika nchi 18 ilipowekeza kwa mafanikio ikiwemo nchini Tanzania. Mtaji uliotolewa na wanahisa wa benki kwa BOA Tanzania, mwezi Septemba mwaka 2019, kunadhihirisha dhamira ya mkakati wake wa kukuza biashara zake nchini.

Dira na Mkakati wa kampuni mama ni kuendeleza wadau wake mbalimbali inaoshirikiana nao kibishara,kuleta msukumo wa kukuza uchumi katika nchi inazofanyia biashara zake, kutoa huduma za kisasa kwa wateja wake na kuhakikisha inakuwa benki bora katika masoko yake.

Asilimia 17.5% Ongezeko Akiba za Wateja

Asilimia 16% mwaka 2018 Mikopo Chechefu Hadi kufikia asilimia 9.2% mwaka 2019

Ukuaji wa asilimia 23.3% wa mtaji wa jumla. Mtaji wa jumla kufika shilingi bilioni 564 mwaka 2019

Ongezeko la asilimia 4.4% katika utoaji wa mikopo. Jumla ya shilingi bilioni 277 ilitolewa mwaka 2019

NDC Development House, Mtaa wa Ohio | Kivukoni | S.L.P 3054 - Dar es Salaam - TANZANIA | Simu ya mezani: (255) 22 221 4000| Simu ya mkononi: 080078 1122(Piga Bure) | info@boatanzania.co.tz

Fuatilia taarifa zetu kupitia: @BankofAfricaTZ @bankofafricatz @bankofafrica_tz BANK OF AFRICA TANZANIA LIMITED

www.boatanzania.co.tz

# Serikali kuendelea kutoa ruzuku dawa za mifugo

**Na Edward Kondela**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega (pichani), amesema serikali itahakikisha inaendelea kutoa dawa za ruzuku za kuogeshea mifugo nchini ikiwa na lengo la kutokomeza magonjwa ya mifugo.



Ulega alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika katika mnada wa mifugo wa Ndelema, Halmashauri ya Mji wa Handeni mkoani Tanga na kuwataka wafugaji kutoacha kuosha mifugo yao ili iweze kuwa na afya njema na hatimaye kupata bei nzuri ya soko.

"Mwaka jana tulipata pesa kutoka kwa Rais zaidi ya Sh. milioni 300 kwa ajili ya kununua dawa na kugawa kwa majosho 1,400 nchi nzima, mwaka huu ametuongeza tumepata zaidi ya Sh. milioni 400 kwa ajili ya kununua dawa na kusambaza katika majosho 1,700, tutaendelea na kutoa dawa za ruzuku bila kuacha ili kuhakikisha tunapiga kabisa vita magonjwa ya mifugo," alisema.

Kuhusu wafugaji wa Wilaya ya Handeni kuingiza mifugo yao katika misitu ya serikali, akizungumza moja kwa moja kwa njia ya simu katika mkutano huo na Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), Prof. Dos Santos Silayo, alimtaka kuweka alama katika misitu hiyo ili wafugaji watambue misitu ya serikali na kutoingiza mifugo yao bila kukusudia.

Prof. Silayo alimwahidi Naibu Waziri kutuma wataalamu leo ili kuanza utekelezaji huo na kuondoa migogoro ya wafugaji kuingiza mifugo yao katika misitu ya serikali.

Ulega pia aliutaka uongozi wa Halmashauri ya Mji wa Handeni kutatua changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo ikiwamo ya miundombinu katika mnada huo pamoja na barabara ili waweze kusafirisha mifugo yao kwa urahisi zaidi.

Baadhi ya wafugaji wameipongeza serikali kwa kuboresha mazingira ya shughuli zao huku wakiomba wazidi kupatiwa elimu zaidi ya masuala mbalimbali ili wafanye shughuli zao bila kukiuka sheria za nchi.

Awali akitembelea bwawa la asili katika Kijiji cha Kweingoma Wilaya ya Handeni Vijijini, Ulega aliwataka wananchi wanaofanya shughuli za uvuvi katika bwawa hilo lenye urefu wa kilomita nne kujiunga katika ushirika ili serikali iweze kuwasaidia huku akiahidi kutoa mashine kwa ajili ya mtumbwi utakaotengenezwa na uongozi wa wilaya hiyo kurahisisha shughuli za uvuvi.






## Masoko madini yawezesha ukusanyaji kodi bil. 1.5/-

**Na Mohab Dominick,** SHINYANGA

SERIKALI imeridhishwa na mwenendo wa masoko ya madini nchini ulioanzishwa na serikali kupitia Wizara ya Madini ili kuinua uchumi.

Kipindi cha Februari 1 hadi 20, mwaka huu, viongozi mbalimbali wa serikali walifanya ziara mkoani Shinyanga katika soko dogo la mnada wa madini ya almasi lililopo Maganzo ili kujionea shughuli zinazoendelea.

Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Shinyanga, Mhandisi Joseph Kumburu, akitoa taarifa kwa vyombo vya habari jana, alisema kuanzia Februari 1, 2020 kuna ongezeko la wageni kutembelea masoko na vituo vya madini vya mkoa huo kujifunza na kujionea mafanikio yaliyopatikana katika Sekta ya Madini tangu kuanzishwa kwa masoko hayo.

Kumburu alieleza kuwa utaratibu mzuri uliowekwa kwenye usimamizi wa uzalishaji na biashara ya madini kwa wachimbaji wasio rasmi mkoani kwake umewezesha serikali kukusanya Sh. bilioni 1.56 kama kodi ya mrabaha na ada ya ukaguzi kuanzia mwezi Mei, 2019 hadi Januari, 2020. Akielezea mafanikio yaliyopatikana tangu kuanzishwa kwa masoko ya madini katika mkoa huo, alisema kabla ya kuanzishwa uzalishaji wa madini ya dhahabu ulikuwa ni kilo 231 kwa thamani ya Sh. bilioni 19.5 na Sh. bilioni 1.3 zililipwa kama mrabaha na ada ya ukaguzi.

Pia baada ya kuanzishwa kwa masoko ya madini kipindi cha Mei 2019, madini yenye uzito wa kilo 329 yenye thamani ya Sh. bilioni 31.9 yaliuzwa na Sh. bilioni 2.2 zikilipwa serikalini kama mrabaha na ada ya ukaguzi.

Alisema mafanikio ya uanzishwaji wa masoko ni pamoja na udhibiti wa utoroshwaji wa madini hali iliyowezesha uzalishaji katika mkoa wa kimadini Kahama kuongezeka kutoka kilo 100 kwa mwaka hadi 1,572 na kukusanya Sh. bilioni 9.7 kama mrabaha na ada ya ukaguzi.

# Kigwangalla akumbana na Faru 'Vicky' ndani ya kreta

**Na Marc Nkwame,** NGORONGORO

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Khamis Kigwangalla, wikiendi alishuka ndani ya Bonde la Ngorongoro kukagua miundombinu iliyoharibiwa na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha eneo hilo.

Hata hivyo, wakati akiendelea kutembelea njia za kreta zilizoharibiwa kwa mafuriko, ghafla faru mwenye umri mkubwa kuliko wote duniani, ajulikanaye kama 'Mama Vicky,' akaibuka na kulazimisha msafara wa Waziri kusimama kwa muda ili kumshuhudia mnyama huyo adimu.

Pamoja na kuwa ndiye faru mwenye umri mkubwa kuliko wote kwa sasa, Faru Vicky pia ni moja ya wanyama wenye miili mikubwa sana kiasi cha kwamba akiwa mbali ni rahisi kudhani kuwa ni tembo.

Meneja wa Mahusiano katika Mamlaka ya Ngorongoro, Joyce Mgaya, aliongeza kuwa, Faru Vicky pia ana rangi nyeusi zaidi kuliko faru wengine ndio maana ni rahisi kumtambua hata akiwa mbali.

'Faru Vicky,' mwenye umri wa miaka 46 kwa sasa, anashika nafasi ya 'marehemu,' Faru Fausta aliyefariki Desemba mwaka jana, na ambaye alivunja rekodi ya kuwa faru mwenye umri mkubwa kuliko wote duniani. Yeye alikuwa na miaka 57 alipokufa.

Faru wanakadiriwa kufikisha umri wa miaka 35 mpaka 40 wakiwa porini na kuishi zaidi ya hapo wakiwa chini ya ulinzi maalum.

Faru mwingine mweusi na jike aliyeishi porini kama Fausta na aliyefahamika kwa umri wake mkubwa ni Solio, wa nchini Kenya ambaye hata hivyo, hajafikia umri wa 'Vicky' (49) na aliachwa mbali na Fausta (57), huyo Solio alikuwa akiishi Kenya na kufa akiwa na umri wa miaka 42 mwaka 2016.

Tanzania inadaiwa kuwa na idadi kubwa ya faru, wanyama ambao ni adimu na hatarini kutoweka duniani. Hata hivyo, namba halisi ya faru waliopo katika hifadhi za Maswa, Serengeti, Mkomazi (Kilimanjaro) na Ngorongoro huwa haitajwi kwa sababu za kiusalama.

Wakati huo huo, juhudi za kurekebisha sehemu za barabara zilizomo ndani ya kreta ya Ngorongoro zimeanza kuzaa matunda, kwani sasa barabara hizo zinapitika kwa asilimia kubwa.

"Kwa sasa hali ni nzuri na tumejiweka sawa kwa mvua zaidi zinazotarajiwa kushuka kipindi cha masika kitakachoanza mwishoni mwa mwezi ujao (Machi)," alisema Dk. Freddy Manongi, Kamishna wa Uhifadhi wa Mamlaka ya Ngorongoro.

Hivi karibuni Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Adolf Mkenda, pia alitembelea miundombinu ya hifadhi za Serengeti na Ngorongoro, baada ya kuibuka taarifa kwamba mvua imeziharibu vibaya barabara za maeneo hayo.

# Diwani wa Chadema atimkia CCM

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

DIWANI wa Kata ya Mtandi kwa tiketi ya Chadema katika Halmashauri ya Mji Masasi mkoani Mtwara, Sande Chipojora, amejiuzulu nafasi hiyo na kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Chipojora alitangaza uamuzi huo na kutimkia CCM juzi wilayani Masasi mbele ya Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, ambaye alifika mjini Masasi kwa ajili ya kushiriki hafla ya kumpokea aliyekuwa Mbunge wa Ndanda, Cecil Mwambe na kumkabidhi kadi ya CCM.

Diwani huyo alidai kuwa CCM ni chama ambacho alikuwa akikipenda tangia yuko mdogo na alipokuwa kuwa mtu mzima na kushiriki siasa alishawishiwa na watu wa Chadema kujiunga chama hicho. Alidai kuwa tangu Rais John Magufuli alipoingia madarakani, amekuwa akifanya yale ambayo wapinzani wamekuwa wakiyasema siku zote hivyo kwa upande wake haoni sababu ya kuendelea kubaki upinzani, badala yake ni bora arejee nyumbani CCM.

"Nimekuwa diwani takribani miaka minne sasa nikiwa ndani ya Chadema sijaona kama kuna demokrasia yoyote zaidi ya kuvaa gwanda pekee," alidai na kuongeza:

Jinsi Rais Magufuli anavyotekeleza miradi mikubwa ya maendeleo siwezi kuwa Chadema tena, narudi CCM kumuunga mkono ili tuijenge Tanzania tukiwa ndani ya CCM."

Alidai shida ya vyama vya upinzani ni moja, viongozi wa ngazi ya chini wanakuwa hawawezi kutumia nafasi zao kufanya majukumu ambayo yapo chini yao, kila kitu kinafanywa na kiongozi wa ngazi ya juu pekee yake.

Sande alisema hata pale unapotaka kufanya kwa kutambua jambo hilo lipo katika mamlaka yako utakuta kiongozi wako wa ngazi ya juu anakupa onyo kwa maana hiyo ni wazi kuwa hakuna demokrasia halisi ndani ya upinzani ukilinganisha na CCM.


LAS VEGAS CASINO

## LAS VEGAS CASINO

## EMPLOYMENT OPPORTUNITY

We are inviting applications for experience Dealers and inspectors.

**Qualifications:**

- Education of not less than form IV and above, with good knowledge of English and Mathematics.
- Applicant should have 18 months minimum gaming experience.

**Application should be accompanied by:**

- Detailed C.V.
- Copies of any relevant certificates academic and work related (if any).
- 2 passport size colored photographs.
- 2 names of referees and their daytime telephone number.
- Applicant's daytime telephone number.
- NIDA card

All applications should be addressed to 'Casino Manager' and handed to the Reception desk between 9:00 am and 4:00 pm at:

Las Vegas Casino, Ali Hassan Mwinyi Road, Upanga, not later than **29/02/2020**

115640902

NMB Karibu yako

## Taarifa ya Mkutano Mkuu Maalum wa 7 wa Wanahisa wa Benki ya NMB

Taarifa inatolewa kwamba Mkutano Mkuu Maalum wa Saba wa Wanahisa wa NMB utafanyika katika ukumbi wa Mlimani City, Dar es Salaam saa 4 asubuhi siku ya Jumatano, tarehe 18 Machi, 2020.

**AJENDA:**

7.1 MATANGAZO NA AKIDI

7.2 KUPITISHA AJENDA ZA MKUTANO

7.3 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA MABADILIKO KWENYE KANUNI ZA KAMPUNI

7.4 KUPOKEA NA KUTHIBITISHA KUJIUDHURU NA KUTEULIWA KWA WAKURUGENZI WA BODI

7.5 MENGINEYO

**MAELEZO MUHIMU**

1. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria Mkutano lazima aje na nakala yake ya risiti ya uwekezaji wa hisa (Depository receipt) au kitambulisho cha Taifa au Hati ya kusafiria au kadi yake ya benki.
2. Mjumbe anayeruhusiwa kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano anaruhusiwa kuchagua mwakilishi kuhudhuria na kupiga kura kwa niaba yake kwa kufuata /kuzingatia taratibu na Sheria za Kampuni kama zilivyorekebishwa. Fomu ya uwakilishi lazima iwasilishwe kwenye ofisi iliyosajiliwa ya Kampuni kabla ya saa 4 asubuhi, Jumanne ya tarehe 17 Machi 2020.
3. Mwanachama anayetarajia kuhudhuria kikao atatakiwa kuhudhuria kwa gharama zake mwenyewe. Fomu za mwakilishi zitapatikana matawini.

Kwa amri ya Bodi ya Wakurugenzi.

Lilian R. Komwihangiro
Katibu wa Kampuni

24 Februari 2020

215641702

www.nmbbank.co.tz

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wachezaji Stars msisubiri kambi maandalizi CHAN

**TAYARI** kipenga cha Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), kimepulizwa baada ya makundi ya michuano hiyo kupangwa.

Katika michuano hiyo itakayofanyika nchini Cameroon kuanzia Aprili 4 hadi 25, mwaka huu, ikishirikisha nchi 16, Tanzania (Taifa Stars) imepangwa Kundi D sambamba na Zambia, Namibia na Guinea.

Ingawa wengi wanaliona ni kundi jepesi wakilinganisha na makundi mengi, sisi tunasema wachezaji Taifa Stars ndio wanaoweza kulifanya kuwa gumu ama jepesi.

Tunasema hivyo kutokana na ukweli kwamba wachezaji wa Stars watakwenda katika michuano hiyo wakiwa wa moto kwa kuwa watatokea Ligi Kuu ambayo italazimika kusimama kwa muda kupisha fainali hizo.

Hivyo, wakati huu Ligi Kuu Bara na Zanzibar ikiendelea, ni wakati mwafaka kwa kila mchezaji kuitumia kuboresha viwango vyao ndani na nje ya uwanja.

Ikumbukwe hakuna mwenye namba ya kudumu katika timu ya taifa, na Kocha Mkuu wa Taifa Stars, Mrundi Etienne Ndayiragije anafuatilia kwa makini Ligi Kuu akiangali wachezaji wanaokidhi vigezo vya kuiwakilisha Tanzania katika fainali hizo.

Na tunaamini kiwango na nidhamu ya mchezaji nje na ndani ya uwanja ndivyo vigezo muhimu atakavyotumia Ndayiragije kupata kikosi chake cha CHAN.

Kwa mantiki hiyo, ni jukumu la kila mchezaji awe amewahi kuitwa Stars ama la, kuendelea kuboresha kiwango chake kikiongozwa na nidhamu ndani na nje ya uwanja ili kujiongezea nafasi ya kuitwa.

Tunatambua michuano hii ina faida kubwa kwa wachezaji wanaopata nafasi ya kwenda kushiriki kwani ni fursa pekee kwao kutangaza viwango vyao nje ya nchi.

Hii ni kutokana na michuano hii kushuhudiwa na mawakala wengi, ambao huitumia kutafuta wachezaji wa kuwauza ndani na nje ya Bara la Afrika, hivyo ni wakati wa kila mchezaji kupigania fursa hiyo muhimu.

Na ndiyo maana tunasema huu si wakati kwa wachezaji wa Tanzania kusubiri hadi Ndayiragije kuwaita kambini ndipo waanze kujipanga kwa fainali hizo.

Tunawakumbusha wakati wa maandalizi ni sasa na kwa wale watakaopata nafasi ya kuitwa watambue wanapaswa kuingia kambini wakiwa fiti ili kazi ya Ndayiragije iwe ni moja tu, kuwaunganisha kwa mfumo anaotaka kuutumia.


Hapo ndipo tutakapoweza kujua kundi la Stars ni gumu ama jepesi kutokana na ubora wa kikosi cha Ndayiragije kuelekea michuano hiyo.

Nchi nyingi za Afrika kwa sasa zimewekeza katika soka na zina wachezaji wengi bora wanaocheza soka la ndani, hivyo huu uwe wakati wa maandalizi ya kina badala ya kuwaaminisha wachezaji kwamba Tanzania imepangwa kundi jepesi.

Nipashe hatuoni uwepesi wa kundi hilo, hasa tukizingatia nchi kama Guinea imewahi kuandaa Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) hivyo si ya kitoto, lakini Zambia tunaifahamu ubora wa soka lake huwezi kuilinganisha na Tanzania.

Sisi tunaamini katika maandalizi ya mapema kwa wachezaji kugundua jukumu lililo mbele yao la kuhakikisha safari hii Tanzania ikishiriki michuano hiyo kwa mara ya pili tangu mwaka 2009, hawafanyi makosa katika kutimiza majukumu yao uwanjani kuanzia sasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuwa staa mechi moja, hakukufanyi ucheze Ulaya



Na Adam Fungamwango

**WAKATI** mwingine huwa nacheka, nikisoma baadhi ya makala za wachezaji wa Kitanzania wanapokuwa wanahojiwa baada ya kucheza vizuri kwenye mechi moja tu.

Wachezaji wa timu za mikoani, wakicheza na timu za Simba au Yanga na kuwa nyota wa mchezo wa siku hiyo, wakihojiwa utasikia wanasema kuwa malengo ni kwenda kucheza Ulaya.

Na hata baadhi ya wachezaji wa timu za Simba, Yanga na Azam nao siku wakionyesha kandanda la hali ya juu, nao wanasema kuwa malengo yao ni kwenda kucheza soka la kulipwa Ulaya.

Halafu wachezaji wengine wanaosema hivyo ni wale ambao walishatoka nchini kwenda kucheza soka la kulipwa nchini za jirani tu, lakini wameshindwa na kurejea tena nchini Tanzania.

Wengine ukitazama hata umri wao ni kwamba hauruhusu kabisa wao kwenda kucheza soka huko, lakini bado wanadai wana ndoto za kucheza soka Ulaya tena baadhi wanakwenda mbali zaidi na kuzitaja timu kubwa barani Ulaya.

Wakati mwingine Wabongo wanaaminishwa ndoto za mchana.

Mtanzania Mbwana Samatta ambaye kwa sasa anaichezea Aston Villa, yeye mwenyewe pamoja na kufika huko bado anajuta kwa nini hakutoka nchini mapema, kwani kwa umri wake wa miaka 27, anaonekana alichelewa kufika Ulaya.

Hapa Tanzania ukiangalia wachezaji wengi wana zaidi ya umri huo na hata wale ambao wana umri mdogo zaidi ya huo, walitakiwa tayari wawe wameshatoka kwenye ligi ya Tanzania, angalau wamesogela kwenye ligi kadhaa bora za Afrika, lakini bado wameendelea kung'ang'ana na ligi ya Tanzania na kutuaminisha kuwa wanataka kwenda kucheza Ulaya.

Wenzetu wana baadhi ya wachezaji wenye umri wa miaka 19 hadi 23, wanacheza Ligi Barani Ulaya tena kwa kiwango cha hali ya juu, kwenye timu kubwa ambapo kwa umri huo kwa Watanzania bado wanakuwa kwenye timu za vijana tu.

Kwa umri walionao wachezaji wanaocheza Ligi ya Tanzania walitakiwa wawe tayari wapo Ulaya wakizichezea klabu za Uturuki, Ubelgiji, Sweden, Denmark na nyingine.

Unashangaa kama kwa umri walionao bado wapo hapa, wanawezaje kutoka kufika ligi za Ulaya bila kupitia njia ngumu kama walizopita kina Samatta na Msuva?

Tusidanganyane, kwa sasa anaoweza kucheza Ulaya ni Nickson Kibabage na Kelvin John ambao bado wana umri mdogo na tayari wameshaondoka kwenye soka la Kibongo. Kingine cha kushangaza ni kwamba mchezaji wanayetamba kucheza Ulaya, anacheza vizuri mechi sita tu kwa msimu za kukamia, mechi zilizobaki anacheza kwenye kiwango cha kawaida sana, hapo huwezi kucheza hata soka la Afrika Kusini, achilia mbali Ulaya.

Kuna wachezaji wanaosubiri mechi za Simba, Yanga au Azam ndiyo aonyeshe ufundi wake, zingine anakuwa mchezaji wa kawaida sana.

Hakuna klabu yoyote Ulaya inayoweza kumchukua mchezaji ambao anaonyesha kujituma na kucheza soka safi kwenye baadhi ya mechi tu.

Kinachotakiwa mchezaji ni kuonyesha uwezo ulionao kwa msimu mzima, kwa sababu huwezi kujua kuwa kuna watu wanakufuatilia.

Tatizo lingine kubwa kwa wachezaji wa Kibongo ni kujitunza na kulinda kiwango.

Hili linaoathiri hadi timu ya taifa, Taifa Stars. Mchezaji anachaguliwa akiwa kwenye kiwango kizuri, lakini baada ya mechi moja au mbili kiwango kinashuka.

Mchezaji hawezi kwenda Ulaya kama anashindwa kulinda kiwango chake na kujitunza mwenyewe bila ya kuwekwa kambini.

Ndiyo maana hata wachezaji wa kigeni wanawashindia wachezaji wa Kitanzania hapo tu.

Mchezaji wa kigeni anaweza akawa na kiwango cha kawaida kuliko Mbongo, lakini mgeni anaweza kukupa kiwango chake kile kile kila mechi, tofauti na Mbongo ambapo inakuwa maji kupwa na kujaa.

Nadhani kwanza wachezaji wa Kitanzania waliangalie hili kwanza kabla ya kutuambia kuwa wana ndoto za kucheza soka la kulipwa Ulaya.

TANGAZO


SAMSUNG
Galaxy S20+ | S20 Ultra
24 MONTH WARRANTY FOR AFRICA
Pre-order now and get Galaxy Buds+
5G
SPACE ZOOM 100X
Always be the first with Tigo!
Pre-order now Samsung Galaxy S20 | S20+ | S20 Ultra and get Galaxy Buds and 78 GB FREE Internet one year.
Samsung Galaxy S20
Tshs. 2,235,000
Samsung Galaxy S20+
Tshs. 2,480,000
Samsung Galaxy S20 Ultra
Tshs. 3,100,000
4G+
Pre-order now on www.tigo.co.tz or at any Tigo shop by paying 10% of actual price.
Offer available until 12 March. *Terms & Conditions Apply.
tigo
215642902

# Waharibu nguzo kushinikiza kupatiwa umeme

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

WANANCHI wa Kijiji cha Lipumburu Kata ya Lipumburu Wilaya ya Masasi mkoani Mtwara, wamekata na kuangusha nguzo ya umeme kwa kutumia msumeno wakishinikiza kijiji chao kupatiwa huduma ya umeme wa REA.

Kufuatia tukio hilo ambalo linadaiwa kutokea mwishoni mwa wiki katika kijiji hicho, kamati ya ulinzi na usalama wilaya ya Masasi ikiongozwa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Selemani Mzee, walifika katika kijiji hicho kwa ajili ya kujionea tukio hilo na kufanya mkutano wa hadhara wa dharura na wanakijiji.

Mzee alisema serikali haitavumilia kitendo hicho, na kwamba wahusika waliofanya jambo hilo lazima wabainike na wafikishwe kwenye vyombo vya sheria.

Mkuu huyo wa wilaya alisema kuwa serikali itawapa saa 24 wanakijiji kuhakikisha wanawatafuta na kuwabaini wahusika kisha kutoa taarifa serikalini ili hatua za kisheria zichukuwe mkondo dhidi ya wahusika.

Mzee alisema kitendo hicho cha kukata na kuangusha nguzo ya umeme ni wazi kwamba kina lengo la kurudisha nyuma jitihada za serikali katika kuleta maendeleo kwa wananchi wake.

Alieleza kuwa zipo njia sahihi ambazo kama wananchi wanakuwa na malalamiko wanaweza kuzitumia ikiwamo kukutana na viongozi wao wa vijiji na kata kufikisha kero au malalamiko walionayo badala ya kutumia njia ambazo sio rafiki na hazina tija kwao. Mzee alisema kuharibu miundombinu kama njia ya kufikisha ujumbe kwa wahusika au kupinga jambo linalowakabili kamwe hakuwezi kumaliza malalamiko yao bali ni kutaka kupambana na serikali.

"Nawapa saa 24 nataka nipate taarifa ya kufahamika kwa hawa waliofanya kitendo hiki cha kukata na kuangusha nguzo hii ya umeme... mimi najiuliza kwanini mtumie njia ya kuharibu miundombinu ya serikali, tena yenye faida kwenu badala ya kufikisha malalamiko yenu kwa njia sahihi," alisema Mzee.

Rufile Milanzi, mkazi wa kijiji cha Njawala, alisema kwa muda mrefu waliahidiwa kupatiwa umeme kwenye kijiji hicho, lakini hadi sasa ahadi hiyo haijatekelezwa licha ya kusimikwa kwa nguzo katika kijiji hicho.

Alisema jitihada za uwekaji umeme zimekuwa zikifanyika katika kijiji jirani na kijiji chao, huku katika kijiji chao nyaya za umeme zikiwa zimepita juu kwenda mpaka kijiji cha jirani cha Njawala ambako ndiko kuonekana umeme utawaka.

Naye Stella Mkapa, alisema awali wananchi hao walishaorodheshwa majina yao kwa lengo la kupatiwa umeme na kwamba walichokiona ni uwekaji wa nguzo pekee.

Kwa upande wake Meneja wa Tanesco Mkoa wa Mtwara, Fadhil Chilombe, alisema utekelezaji wa uwekaji umeme katika kijiji hicho umekamilika, na kwamba kuanzia mwezi ujao, umeme utakuwa umeshafika kwa wananchi wa kijiji hicho. "Taratibu zote za kuleta umeme hapa na vijiji vingine zimeshakamilika, mimi niwaombe wananchi waendelee kuwa wavumilivu wakati taratibu zikiendelea kufanyika na sio kuamua kuharibu miundombinu, hili sio jambo la busara," alisema Chilombe.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akionyeshwa pete na Mkurugenzi wa Gem Tanzanite Ltd, Osman AbdulSattar, kwenye Mkutano wa Kimataifa wa Uwekezaji katika sekta ya madini Tanzania 2020, uliofanyika jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Ongezeko la sangara laishtua CCM

**Na Mwandishi Wetu,** SIMIYU

CHAMA cha Mapinduzi (CCM) kimeshtushwa na ongezeko kubwa la samaki aina ya sangara ikiwa ni miaka mitatu tu tangu serikali ya awamu ya tano kuanza operesheni za kudhibiti uvuvi haramu katika Ziwa Victoria.

Kutokana na hali hiyo, CCM imeitaka serikali kuchukua hatua za haraka kutafuta masoko ya uhakika ya samaki ndani na nje ya nchi.

Wakizungumza kwenye ziara ya wajumbe wa Sektetarieti ya CCM Mkoa wa Simiyu, baadhi ya wavuvi katika Mwalo wa Nyamikoma wilayani Busega, walisema kabla ya operesheni kuanza walikuwa wakisafirisha wastani wa tani sita za samaki kwa mwezi, lakini tangu serikali ilipoamua kuchukua hatua za kudhibiti uvuvi haramu, samaki wameongezeka na sasa wanasafirisha wastani wa tani 60 kwa mwezi. Mwenyekiti wa Kikundi cha Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi 'BMU' Mwalo wa Nyamikoma wilayani Busega mkoani Simiyu, George James, alisema ongezeko hilo kubwa la samaki pia limepunguza bei ya sangara kutoka wastani wa Sh. 9,000 kwa kilo hadi Sh. 4,000 kwa kilo.

Mbali na mafanikio hayo, pia wavuvi hao wameiomba serikali kuwasaidia kupata mtambo wa kutengeneza barafu katika eneo hilo kwani kwa sasa wanalazimika kusafiri hadi jijini Mwanza umbali wa zaidi ya kilomita 150 kufuata barafu.

Hivyo walimwomba Katibu wa CCM Mkoa wa Simiyu kumfikishia shukrani Rais John Magufuli kwa uongozi wake imara hasa katika usimamizi wake wa rasilimali za uvuvi, na kwamba sasa samaki ni wengi ombi lao kubwa ni kusaidiwa kupata soko baada ya ongezeko hilo la samaki.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika katika Mwalo wa Nyamikoma wilayani Busega, Katibu wa CCM Mkoa wa Simiyu, Haula Kachwamba, aliitaka serikali kupitia Dawati la Sekta Binafsi lililoko Wizara ya Mifugo na Uvuvi kufika katika mwalo huo wa Nyamikoma ili kuwaunganisha wavuvi hao na taasisi za kifedha kuweza kupata mtambo wa kutengeneza barafu.

Pia ameitaka serikali kutanua wigo wa kuwatafutia masoko ya samaki wavuvi hao ili kunufaika na fursa kubwa ya ongezeko hilo la samaki aina ya sangara kwa kupeleka katika masoko ya mikoa ya mbali na Ziwa Victoria pamoja na nchi za jirani za Kongo, Zambia, Burundi, Rwanda, Malawi na Msumbiji.

## Walimu Monduli wapewa motisha

**Na Asraji Mvungi,** MONDULI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Monduli, mkoani Arusha imetoa motisha kwa walimu kwa kuwapa samani na vifaa vya ndani ili kukabiliana na changamoto zao.

Ofisa Elimu wa wilaya hiyo, Teresia Kyara alisema hatua hiyo inalenga kuwaongezea walimu motisha kukabiliana na changamoto zilizo ndani ya uwezo wao kwenye shule zao.

Akizungumza wakati wa kutoa zawadi hizo ambazo ni samani, majiko na mitungi ya gesi, Kyara alisema kuna haja ya jamii kuwa na utaratibu kusaidiana na walimu kukabiliana na matatizo yanayojitokeza badala ya kuwalaumu hasa wanaposhindwa kufikia malengo.

"Ni jambo la kawaida kuwabebesha walimu mzigo wa lawama hasa shule zinapopata matokeo mabaya bila kuangalia chanzo cha tatizo husika, wakati mwingine matatizo yanakuwa nje ya uwezo wao jambo ambalo licha ya kukatisha tamaa linaendelea kuongeza tatizo badala ya kupunguza," alisema.

Alisema licha ya tatizo la utoro kwa wanafunzi hasa wa kike linalochangiwa na baadhi yao kupata mimba, wanaobaki wanafanya vizuri na asilimia kubwa wamefaulu.

Ofisa elimu taaluma wa wilaya hiyo, Jumanne Masuke, alisema ufaulu unaongezeka kwa mwaka 2019 /20 halmashauri hiyo imeshika nafasi ya 25 kati ya halmashauri 186 na kimkoa imeshika nafasi ya nne kati ya halmashauri saba za Mkoa wa Arusha.

Mkuu wa Wilaya ya Monduli, Iddy Kimanta, alisema matatizo yaliyopona yanaoendelea kujitokeza likiwamo la utoro wa wanafunzi yanaendelea kupungua kwa kasi kutokana na matokeo ya ushirikiano unaoendelea kati ya walimu, wazazi na viongozi.

"Ukisikiliza maelezo yanayotolewa na mambo yanayosemwa kuhusu matatizo yanayoikabili Monduli unaweza kuona kama vile hakuna kitu kinachofanyika, lakini kazi inafanyika na kuna mafanikio makubwa, Monduli haikuwa hivi hali ilikuwa mbaya sana," alisema Kimanta.

Aliwataka walimu wa shule zinazofanya vibaya kila mwaka kujitafakari kujua tatizo na kulifanyiakazi.

Halmashauri ya Wilaya ya Monduli yenye kata 20, ina shule za msingi 72 zenye walimu 762.

# Mwekezaji Misri kujenga kiwanda cha mitungi gesi

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Supreme Holding kutoka Misri inatarajiwa kuwekeza kiasi Dola za Kimarekani milioni 25 (zaidi ya bilioni 40) kujenga kiwanda cha kutengeneza mitungi ya gesi wilayani Mkuranga, mkoani Pwani.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana baada ya kufanya mazungumzo na mmiliki wa kampuni hiyo, Dk. Moharram Helal, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, alisema mbali ya kutengeneza mitungi, kampuni hitakuwa inajaza gesi na kurejeleza mitungi ambayo imeshatumika. "Hatujawahi kuwa na kiwanda cha aina hii hapa nchini kwani mitungi yote inayotumika kujaza gezi imekuwa ikiingizwa kutoka nje ya nchi. Hii ni fursa ya kipekee kwa Tanzania ambayo ina hazina kubwa ya gesi," alisema Waziri Kairuki.

Kwa mujibu wa Kairuki, kiwanda hicho kitakuwa na uwezo wa kutengeneza mitungi 1,000 kwa siku na pia kujaza gesi kwenye mitungi 3,000 kwa siku ambayo itakuwa na ujazo kati ya kilo 15 na kilo 30.

"Mpaka kiwanda kitapokamilika kitaweza kuajiri Watanzania 300 na Wamisri 30," alisema nakuongeza kuwa Serikali ya Awamu ya Tano imeazimia kuifanya Tanzania kuwa nchi ya uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025. Waziri Kairuki amekiagiza Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) kuhakikisha kinatoa msaada stahiki kwa mwekezaji huyo ikiwamo kujisajili kwa kituo ili aweze kunufaika na huduma zinatolewa na kituo kwa wawekezaji hapa nchini.

"Ningependa kuwashauri wawekezaji nchini kuwasiliana moja kwa moja TIC ili kujiepusha na urasimu usio wa lazima kutoka kwa watu wa kati. Nitaendelea pia kuwakumbusha wawekezaji kuendelea kujisajili na TIC kwani faida zake ni kubwa sana," alisema.

Alisema amemwomba pia mwekezaji huyo kufikiria pia kuzalisha mitungi yenye ujazo wa chini zaidi ili watu kima cha chini waweze kunufaika na bidhaa zitakazozalishwa au kutengenezwa na kiwanda hicho. "Tuna mhitaji sana huyu mwekezaji katika eneo hili la kutengeneza mitungi badala ya kuagiza kutoka nje. Nimemwomba afanye mawasiliano na TIC moja kwa moja anapohitaji msaada badala ya kupitia kwa watu wa kati.

Kairuki alimwakikishia mwekezaji kuwa Tanzania ni sehemu sahihi ya kuwekeza na pia kuna fursa nyingi za uwekezaji na mazingira mazuri na rafiki kwa uwekezaji. Kwa upande wake Dk. Helal ambaye aliambatana na Meneja Mkuu wa Intergas, Dk. Hatem Ahmed, alimshukuru Waziri Kairuki na kumhakikishia kuwa kiwanda kitakamilika kwa muda baada ya kukamilisha taratibu za kisheria.




Mkuu wa Wilaya ya Lindi, Shaibu Ndemanga, akipokea mabati kutoka kwa Meneja wa NMB Kanda ya Kusini, Janeth Shango, ambayo ni msaada katika Shule ya Sekondari Kiwalala. Tukio hilo lilifanyika mwishoni mwa wiki katika Shule ya Sekondari Mnolela iliyopo Halmashauri ya Mtama.
**PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SAT yakamilisha mtaala mpya wa kilimo vyuo 29

**Na Faustine Feliciane,**
MOROGORO

SHIRIKA la Kilimo Endelevu Tanzania (SAT), limesema limekamilisha mtaala mpya wa kilimo ambao unatarajiwa kuanza kutumia kwenye vyuo vya mafunzo ya kilimo 29 nchini huku mtaala huo ukizingatia mahitaji ya sasa kwenye kilimo.

Akizungumza na waandishi wa habari za kilimo hai wilayani Mvomero mkoani hapa, Meneja wa Mradi wa SAT, Mgeta Daudi, alisema mtaala huo wameufanikisha kwa kushirikiana na Serikali kupitia Wizara ya Kilimo divisheni ya Mafunzo, Huduma za Ugani na Utafiti kwa hisani ya Shirika la Maendeleo la Leichtenstein.

Alisema kwa sasa awamu ya kwanza ya mtaala huo ulianza kufundishwa katika vyuo saba vya Mati-Ilonga, Chuo cha Taifa cha Sukari (NSI), Mati Kartini, Mati-Ilonga, Mati horti-Tengeru, KATC-Moshi, TRACDI na Chuo cha St.John's.

"Lengo ni kuhakikisha mradi huu unaendelea kupanua wigo wake na kuvifikia vyuo vyote 29 vya mafunzo ya kilimo nchini katika kanda zote saba za kilimo, mradi huu ambao unafahamika kama 'CISTI' unatekelezwa katika ngazi tatu kuu," alisema Mgeta.

Alifafanua ngazi hizo za mradi ya kwanza unajenga uwezo kwa wakufunzi wa vyuo vilivyopo katika mradi.

"Katika ngazi ya pili mradi unaimarisha uwezo wa vyuo ya mafunzo ya kilimo kimiundombinu ili kuleta ufanisi zaidi katika utekelezaji wa mtaala mpya wa kilimo, tatu mradi unashirikiana na divisheni ya mafunzo, huduma za ugani na utafiti ya wizara ya kilimo ambayo ndiyo ina dhamana ya kusimamia vyuo vyote vya kilimo kuhakikisha mtaala unatekelezwa vyema na matokeo chanya yanatokea," alisema Mgeta.

Alisema SAT lilishiriki kikamilifu katika hatua zote za muhimu za kuhuboresha mtaala na hatimaye ushawishi wake ulisababisha kuingizwa kwa moduli mpya tatu za kilimo hai, jinsia katika kilimo na usimamizi wa mazingira katika mtaala mpya.

"Taratibu na hatua zote za kuboresha mtaala na kuthibitishwa na Baraza la Elimu ya Ufundi la Taifa (NACTE) na kilele cha mchakato huu kilihitimishwa kwa kuzinduliwa kwa mtaala mpya ambao ndio unachukua nafasi ya mtaala wa zamani," alisema Mgeta.

Aalisema namna bora ya kuongeza wigo wa kilimo hai Tanzania ni kuzalisha wataalamu wenye umahiri katika maarifa na ujuzi wa kilimo hicho.

# Wanawake waaswa kuukataa udumavu

**Na Neema Sawaka,**
KAHAMA

WITO umetolewa kwa wanawake vijijini wenye watoto wadogo kuzingatia usafi kabla ya kunyonyesha na kuandaa vyakula vyenye lishe ili kukabiliana na udumavu, ambao una madhara makubwa kwa makuzi ya mtoto.

Hayo yalielezwa na mhamasishaji wa masuala ya lishe wa Shirika la Huheso Foundation la wilayani Kahama, Irene Ezekiel, alipokuwa akizungumza na wanawake wa Kijiji cha Kakebe, Kata ya Nyandekwa katika Halmashauri ya Mji wa Kahama.

Ezekiel alisema wanawake wa vijijini hukabiliwa na shughuli nyingi zikiwamo za shambani na pindi wanapohitaji kunyonyesha watoto hufanya tendo hilo bila kusafisha ziwa, hivyo kushindwa kubaini hali hiyo inaweza kusababisha maradhi yanayoweza kusababisha udumavu.

"Muache kunyonyesha kwa mazoea, safisheni matiti yenu muhakikishe yapo safi ndipo mwapatie watoto wenu," alisema Ezekiel.

Mhamasishaji mwingine, Silaji Michael, kutoka shirika hilo ambalo linatekeleza mradi wa mtoto mwelevu kwa ufadhili wa Ima Health World kwa kushirikiana na Jukwaa la Lishe Tanzania (PANITA), aliwataka wazingatie lishe bora.

Michael alisisitiza kuwa familia za vijijini kuzingatia lishe kwa kutumia vyakula vyenye gharama nafuu vinavyopatikana katika maeneo yao ili kuepuka maradhi ambayo yakifumuka husababisha umaskini.

Kwa upande wake Muuguzi Mkunga kutoka Hospitali ya Halmashauri ya Mji wa Kahama, Joyce Mhagama, alisema msingi wa kukabiliana na udumavu ni kuhakikisha mjamzito anahakikisha anapata makundi matano ya vyakula, huku wakihudhuria kliniki tangu wapatapo ujauzito.

Mhagama alisema wakizingatia makundi hayo ya vyakula sambamba na kupata mapumziko ya kutosha, itasaidia kutojifungua watoto wadumavu na hasa wakiondokana na tabia ya kuchelewa kuripoti kliniki, ambalo limekuwa tatizo kubwa.

# Hoteli hifadhini zaagizwa sifa za walinzi

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameziagiza taasisi za uhifadhi nchini kuhakikisha zinasimamia utaratibu wa wamiliki wa malazi ndani ya hifadhi wanawaajiri walinzi waliopata mafunzo katika vyuo vya taaluma ya wanyamapori nchini au waliopitia mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT).

Alisema sababu ya kufanya hivyo ni kutokana na kuripotiwa kwa matukio kadhaa ya watalii nyakati za usiku wakiwa wamelala kuvamiwa na wanyamapori wakali, huku walinzi hao wasiokuwa na ujuzi kuhusiana wanyamapori hujinusuru kwa kuwakimbia watalii hao.

Aidha, amesema kumekuwa na tuhuma za mara kwa mara kila kunapotokea wizi wa mali za watalii walinzi hao wamekuwa wakinyooshewa vidole kwa madai ya kushiriki kuiba mali hizo.

Kufuatia hali hiyo, Kanyasu ametaka kazi hiyo ifanywe na wahitimu wa vyuo vya wanyamapori nchini au JKT ili pale inapotokea watalii kuvamiwa waweze kutoa msaada kwa vile wana ujuzi wa namna ya kukabiliana na wanyama hao.

Ametoa agizo hilo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizungumza na wajumbe wa kamati ya ulinzi na usalama wakati alipofanya ziara ya kikazi katika ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza.

Alisema watalii wanapokuja nchini wanahitaji vitu viwili ikiwamo suala la usalama wao pamoja ukarimu.

Alisema agizo hilo litawahusu wadau wote wa utalii wanaowalaza watalii ndani ya hifadhi wakiwamo wamiliki wa hoteli pamoja na mahema.

Alisema kitendo cha walinzi kuwakimbia watalii wanapopata matatizo badala ya kutoa msaada ni kasoro ambazo kama hazitadhibitiwa ipasavyo zitaijeruhi sekta ya utalii.

Akizungumzia kuhusu kuajiri wahitimu wa vyuo vya wanyamapori nchini, alisema mbali ya kuwa na ujuzi wa kukabiliana na wanyamapori bali wana ujuzi wa namna ya kuwahudumia watalii kwa vile wanatambua thamani ya watalii.

Kanyasu alizitaka taasisi hizo hasa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (Tanapa) kuhakikisha walinzi wanaohusika na jukumu la kuwalinda watalii ni lazima wawe na sifa stahiki hali itakayosaidia endapo wakivamiwa wakiwa wamelala waweze kupata msaada.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya ZOLA Afrika Mashariki na Tanzania, Yusuph Nassor (kulia), akizungumza mwishoni mwa wiki na baadhi ya wanafunzi wa shule za sekondari zilizopo Wilaya ya Kisarawe wakati wa uzinduzi wa kampeni ya Bukua na Ushinde iliyoandaliwa na kampuni hiyo, yenye lengo la kuhamasisha wanafunzi wa kidato cha nne 2020 kufanya vizuri katika mtihani wa Taifa.

# Watakiwa kuchangamkia fursa zao rozela

**Na Faustine Feliciane,** mvomero

WAKULIMA nchini wametakiwa kuchangamkia fursa ya zao la rozela katika masoko, wakitakiwa kulima kwa wingi kutumia njia ya kilimo hai.

Wito huo ulitolewa na Mkurugenzi wa Shirika la Kilimo endelevu Tanzania (SAT), Janeth Maro, kwenye ziara ya waandishi wa habari wa kilimo hai kwenye Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Hai inayomilikiwa na shirika hilo wilayani Mvomero, mkoani Morogoro.

Maro alisema rozela ni moja ya zao lenye soko kubwa ndani na nje ya nchi lakini wakulima wengi bado hawajui fursa zilizopo kwenye zao hilo.

"Wakulima wengi hasa kwenye maeneo ambayo zao hili linastawi vizuri hawajui fursa zilizopo ndani yake, rozela lina soko kubwa sana nje ya nchi na hata hapa ndani, lakini uzalishaji wake sio mkubwa hapa ndani," alisema Maro.

Alisema rozela ya Tanzania ina soko kubwa nje ya nchi hasa kwenye nchi ya Uswisi na kwamba taasisi hiyo imekuwa ikipeleka zao hilo wanalolima kwenye kituo chao kwa njia ya asili.

"Tumepata soko zuri Uswisi na hata hapa ndani ya Tanzania, kwa sasa tupo hatua ya mwisho ya kupeleka rozela tuliyoifunga kwenye pakiti 5,000 na inauzwa kwa bei nzuri," alisema Maro na kuongeza:

"Kwa mfano tunauza rozela ya pakiti ndogo ya gramu 50 kwa gharama ya dola tano (zaidi ya Sh. 2,700), kwa hiyo wakulima wajaribu kuangalia fursa zilizopo kwenye zao hili," alisema Maro. Alisema mazao mengine yenye soko nchini Uswisi ni pamoja na mazao ya viungo, mdarasini na pilipili manga, pia wapo kwenye hatua ya mwisho kupeleka nchini humo tani 10 mpaka 15.

Alisema zao hilo halina ugumu kwenye kulima kwa kuwa linapaliliwa, linaota na kustawi kwenye mvua chache hasa ikinyesha wakati wa kukaribia mavuno.

Alisema kwa Tanzania zao hilo linastawi zaidi kwenye maeneo ya Mvomero ambako kuna mvua ndogo kwa mwaka na maeneo mengine yenye hali kama ya wilaya hiyo.

Naye, Meneja wa Kituo cha Utafiti cha Kilimo Hai cha SAT, Frank Marwa, alisema rozela ni zao muhimu kwa maisha ya binadamu na faida yake kubwa ni ina chembe chembe za kuondoa sumu mwilini, inaongeza chembechembe za uzalishaji damu mwilini, inaondoa msongo wa mawazo, lakini inatumika kutengeneza vinywaji kama juice na mvinyo.

# Bodi Chauru yafanya ukaguzi miundombinu ya mashamba

**Na Julieth Mkireri**, CHALINZE

WAJUMBE wa Bodi ya Chama cha Ushirika wa Wakulima wa Umwagiliaji Ruvu (CHAURU), wamefanya ukaguzi wa miundombinu ya shamba lao ikiwa ni moja ya mikakati ya maandalizi ya msimu wa kilimo unaotarajia kuanza hivi karibuni.

Ukaguzi uliofanywa katika shamba hilo lililopo Ruvu, Halmashauri ya Chalinze, mkoani Pwani, ulihusisha ukarabati wa mifereji ambao unaendelea kwa sasa.

Akizungumza baada ya ukaguzi, Mwenyekiti wa Chauru, Sadala Chacha, alisema lengo lao ni kujiridhisha ili msimu utakapoanza kusiwapo na malalamiko kutoka kwa wakulima kukosa maji kwenye mashamba yao na kupata mavuno hafifu.

Alisema, Februari 29, wanatarajia kufanya kikao cha bodi, hivyo kati ya mambo wanayotaka kuyajadili ni pamoja na miundombinu ya shamba hilo.

Alisema hivyo ilikuwa ni lazima kufanya ukaguzi huo ili kujiridhisha na ukarabati unaoendelea.

"Wananchi wameanza kufyeka mashamba kwa ajili ya msimu wa kilimo, imetulazimu na sisi kufanya ukaguzi wa miundombinu na kuangalia hali ya ukarabati inayoendelea, kuepuka changamoto za maji kutofika kwenye baadhi ya maeneo inayosababishwa na miundombinu."

"Msimu uliopita baadhi ya wakulima hawakuwa na mavuno mazuri kutokana na uhaba wa maji kwa baadhi ya mifereji kubomoka," alisema Sadala.

Aidha, alisema ukarabati huo unaoendelea umetokana na fedha zaidi ya Sh. milioni 45 fedha zilizochangwa na wanachama wa Chauru.

Alibainisha kuwa changamoto wanayokabiliana nayo kwa sasa katika ukarabati huo ni, baadhi ya mafundi kutokuwa waaminifu na kuiba vifaa vya ujenzi.

Sadala aliwaomba wanachama kutoa ushirikiano kulinda mali za chama, pamoja na kudhibiti mafunzo wanaokarabati miundombinu hiyo ili kuepuka hasara ambayo inaweza kutokea.

Mwenyekiti huyo pia alitoa wito kwa wanachama kufuata ushauri wa wataalamu, wakati wanapoandaa mashamba, na msimu unapoanza ili kuongeza mavuno.

Sadala alisema kwa msimu ujao wa kilimo wanalenga kuongeza mavuno, kutoka tani saba kwa hekta hadi tani 10, kwani hali ya soko kwasasa imeanza kufunguka kutoka maeneo mbalimbali ndani ya nchi.

Wanachama wa Chauru ambao kilimo chao kikubwa ni mpunga wanatoka katika maeneo ya ndani na nje ya Mkoa wa Pwani.

# Kanisa kusaidia upatikanaji maji, elimu

**Na Jaliwason Jasson,**
MANYARA

ASKOFU Samweli Nyanza wa Kanisa la Tanzania Methodist (TMC) wa Jimbo la Manyara, ameahidi kuendelea kushirikiana na serikali kupitia kanisa lake, kusaidia huduma za kijamii hasa upatikanaji wa maji na elimu, ili kuondoa changamoto kwa wananchi hasa maskini.

Alisema hayo jana Mjini Babati, wakati wa hafla ya kumwapisha kuwa Askofu wa jimbo hilo jipya.

Nyanza alisema Kanisa la TMC litashirikiana na serikali kupata majisafi na salama pamoja na elimu ya awali kwa watoto.

"Mfano mzuri tumechimba visima vitano vya maji katika mkoa huu wa Manyara na tumeweka matangi kituo cha afya Magugu na tutaendelea kutoa huduma hizi ili kuisaidia serikali maana haiwezi kufanya yote yenyewe, lazima sisi wadau tusaidie serikali yetu," alisema Askofu Nyanza. Kadhalika katika kuhakikisha elimu inaendelea kutolewa alisema wanasaidiana na serikali kuwapatia elimu ya msingi watoto ili wainuke kielimu.

Pia kanisa hilo litaendelea kushirikiana na serikali kuwaletea maendeleo wananchi na ameapa kuwa mwaminifu kiongozi mwema katika utume wake.

Naye Askofu Mkuu wa kanisa hilo, Joseph Bundala, akimwapisha Askofu Nyanza, alimtaka kulinda kanisa dhidi ya upotoshaji, kutokupenda fedha kwa kutoa huduma kwa waumini aliyopewa na Mungu.

"Ni lazima uwe na busara, mtu wa kiasi, mtu wa utaratibu na lazima uwe mkaribishaji maana siku hizi nyumba za maaskofu unakuta mbwa mkali, ukiingia unaulizwa wee ni nani," alisema Bundala.

Akihubiri kabla ya kumwapisha Askofu Nyanza, aliwaambia waumini kuwa maisha ya mwanadamu yapo mikononi mwa Mungu na mtu akitaka kuyapoteza ni pale anapojitenga naye.

Mgeni rasmi Mkuu wa Wilaya ya Babati, Elizabeth Kitundu, aliwataka maaskofu na wachungaji wa kanisa hilo kuendelea kusisitiza maadili hasa kwa watoto na kuhamasisha wazazi wawapeleke shule watoto wao. Kitundu pia aliwataka viongozi hao kupiga vita matumizi ya dawa za kulevya ambayo yana athari kwa waumini na kuangamiza nguvu kazi ya taifa.



Mwalimu wa Shule ya Msingi Mazinde-Toima Kata ya Loiborsoit, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Kaika Elias, akiwaonyesha wageni namna alivyokuwa anawafundisha watoto chini ya mti, baada ya Shirika la ECLAT Foundation kujenga madarasa manne mapya na kukabidhi kwa serikali juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mkandarasi atakiwa kutengeneza vivuko alivyoharibu

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MADIWANI wa Halmashauri ya Jiji la Arusha, wameiagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira (AUWSA) kumsimamia vema mkandarasi anayetekeleza mradi mkubwa wa maji wa Sh. bilioni 520 mkoani humo, ili arudishe vivuko kwenye barabara alivyoharibu wakati wa kupitisha mabomba.

Akizungumza mwishoni mwa wiki katika kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo, Mwenyekiti wa kikao hicho, Isaya Doita wa Kata ya Ngarenaro, alisema hali ya barabara za jiji hilo ni mbaya.

"Huyu mkandarasi wenu wa Kampuni ya Wachina nyie AUWSA, ameharibu barabara sana wakipitisha mabomba wanakata barabara hawarudishi udongo vizuri ikija mvua balaa, lakini sehemu za vivuko nako amevuruga," alisema.

Alisema kwa kuwa AUWSA ndio msimamizi mkuu ni vema wakamsimamia kuhakikisha anarudisha vivuko vyote alivyovuruga katika barabara, ili wananchi wavuke bila shida na wanafunzi. Aliwataka AUWSA kupita katika maeneo mbalimbali walikopitisha mabomba Wachina hao, ili wajionee hali halisi na wajue jinsi ya kurekebisha.

Naye Diwani wa Kata ya Olsunyai, Elirehema Nnko, alisema malalamiko ya kuharibiwa barabara walishatoa kwa baadhi ya viongozi wa AUWSA, lakini walijibiwa mkandarasi hana wajibu wa kurudisha barabara alizoharibu zote, isipokuwa za lami pekee.

"Hawa watu wametuharibia miundombinu ya barabara zetu huko mitaani balaa, hebu jitafakarini, lakini hata hizo barabara za lami nako ovyo mmevuruga vivuko kwa kukata kwenu barabara," alisema. Akizjibu hoja za madiwani hao, mfanyakazi wa AUWSA, Edes Mushi alisema, kuhusu changamoto hiyo wanayo taarifa na mkandarasi tayari ameanza kufanyia kazi kwa kurudisha vivuko maeneo yote aliyoharibu.

Pia AUWSA wanahakikisha wanamsimamia vema ili barabara zirudi katika hali yake. Kwa upande wake Mhandisi wa Halmashauri ya Jiji hilo, Fordia Mwankenja, alisema wameona changamoto za ubovu wa barabara, wanasubiri mvua zipungue waanze kutengeneza barabara za mitaani zilizoharibiwa na mvua na mkandarasi huyo.

# Serikali yaipongeza Ujerumani kuleta watalii

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

SERIKALI imeipongeza nchi ya Ujerumani kwa kuwa miongoni mwa nchi tano zinazoongoza kuleta wageni wengi wa utalii nchini kila mwaka na kuchangia Pato la Taifa.

Akitoa pongezi hizo mwishoni mwa wiki katika hafla iliyoandaliwa na Ubalozi wa Ujerumani nchini Tanzania, kwa ajili ya kuhamasisha kushiriki maonyesho ya Kimataifa ya Utalii (ITB), yatakayofanyika Machi mwaka huu nchini Ujerumani, Waziri wa Maliasili na Utalii, Hamisi Kigwangalla, alisema kutokana na ushirikiano mzuri uliopo ni lazima Tanzania ishiriki maonyesho hayo ili kutangaza zaidi vivutio vilivyopo.

"Nawapongeza Ujerumani hamjawahi toka kwenye nchi tano, zinazoongoza kuleta wageni nchini, sasa nasi tutatumia fursa ya maonyesho haya kuja kuweka banda letu la maonyesho ya vivutio vyetu ili tuvute wageni wengine zaidi ya sasa," alisema.

Alisema mwaka jana maonyesho hayo yalikuwa na washiriki zaidi ya 160,000 na nchi zaidi ya 180, huku wafanyabiashara zaidi ya 10,000 walivutiwa na maonyesho hayo.

Kingwangalla alisema pamoja na mwaka jana banda la Tanzania kuwa kivutio kwa watu wengi kwenye maonyesho hayo yaliofanyika Berlin, Ujerumani, lakini mwaka huu wataboresha zaidi ili kuvuta wengi zaidi ya mwaka jana.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Prof. Aldof Mkenda, alisema maonyesho hayo ni muhimu kwa Tanzania, kwa kuwa ni fursa nzuri kwa kuongeza soko la utalii.

"Sisi tutashiriki kikamilifu mwaka huu taasisi za umma na binafsi na tunashukuru sana Balozi kutushirikisha katika hili na hatutawaacha kwa kuwa nyie ni washirika wetu wazuri katika kunyanyua sekta ya utalii nchini," alisema.

Akizungumza katika hafla hiyo ya kuhamasisha maonyesho hayo ya kimataifa, Balozi wa Ujerumani nchini Tanzania Regine Hess, aliomba Tanzania kushiriki katika maonyesho hayo ili kupata fursa zaidi katika nyanja za utalii.

Alisema Tanzania imekuwa mstari wa mbele kushiriki maonyesho hayo kila yanapofanyika na kuvutia watu wengi kwenye banda lao, kutokana na kuwa na vivutio vingi kwenye hifadhi zao.



## Mwendokasi madereva wa malori wawakera wananchi

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

WAKAZI wa mji mdogo wa Sanya Juu, Wilaya ya Siha, wamekitaka kikosi cha usalama barabarani mkoani Kilimanjaro, kutafuta mwarobaini wa tatizo la mwendo kasi linalotishia usalama wao kutokana na uendeshaji mbaya wa malori ya mchanga na yale yanayosafirisha mazao kutoka shambani kwenda kwenye masoko mbalimbali nchini.

Wameliomba Jeshi la Polisi kuweka tochi katikati ya mji huo ili kuwadhibiti madereva wanaoendesha kwa kasi na bila kuzingatia alama za barabarani.

Kilio hicho kilitolewa jana wilayani hapa na baadhi ya wafanyabiashara pamoja na wakazi wa mji huo kwa nyakati tofauti, wakati wakieleza masikitiko yao kuhusu mwenendo wa malori hayo katikati ya mji, na namna ambavyo mamlaka za serikali zimekuwa zikichelewa kuchukua hatua.

Mkazi wa Sanya Juu, Kelvin Francis, akieleza namna wasivyopendezwa na mwendo kasi wa malori hayo, alisema madereva wa magari hayo yanayobeba madini ya mchanga, mawe na yanayokwenda na kutoka shambani kupeleka mazao katika masoko ya Dar es Salaam na Zanzibar, wanavunja sheria kwa makusudi na kuhatarisha usalama wa watu wengine.

"Hivi sasa suala la mwendo kasi limekuwa jambo la kawaida kuona magari hayo yakipita kwa mwendo huo, huku baadhi ya watu wakiwamo bodaboda wakiwaunga mkono kwa kuwapigia miluzi kwamba kinachofanywa na madereva wa fusso na malori makubwa ya mzigo ni sawa sawa," alieleza Foibe Mmari.

Naye Richard Goodluck, mkazi wa Majengo wilayani hapa, alisema kutokana na tishio hilo wanaiomba Ofisi ya Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (Tarura) kuangalia uwezekano wa kuweka matuta katikati ya mji huo ili watembea kwa miguu wapite kwa usalama wakiwamo wanafunzi, badala ya kusubiri hadi ajali itokee.

Kwa upande wake, mfanyabiashara wa mazao wilayani hapa, Nicholaus Mshauri, alisema haoni sababu mpaka sasa mamlaka za serikali kushindwa kudhibiti tatizo hilo, wakati tayari serikali ilishatunga kanuni ya usafirishaji wa huduma ya magari makubwa ya mizigo mwaka 2012 na mwaka 2017 ilizifanyia marekebisho kwa lengo la kuhakikisha sekta ya usafirishaji ina imarika na kufanya kazi vizuri.

Wakazi hao wamesema barabara hiyo kwa muda mrefu imekuwa na ajali nyingi za watu kugongwa na magari na kupoteza maisha papo hapo.

# Wanaotajwa kuwania Jimbo la Siha wakutana msibani

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MAKADA saba wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) akiwamo Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Agrey Mwandry, ambao wanatajwa kuwa 'watia nia' ya ubunge wa Jimbo la Siha mkoani Kilimanjaro, wameibukia katika shughuli za mazishi ya kada maarufu wa chama hicho na kiongozi wa mila wa jamii ya wafugaji wa Kimasai, Lazaro Lengere.

Mwanry na wenzake, akiwamo pia Mbunge wa sasa wa Siha, Dk. Godwin Mollel, walikutana juzi katika Kijiji cha Embukoi, Kata ya Donyomoruwa, Wilaya ya Siha na kukaa pamoja.

Akiwa katika msiba huo uliokusanya makada na wanasiasa kutoka maeneo mbalimbali, Mwanry, alipewa nafasi ya kusalimia na aliposimama, alianza kwa kuonya kuhusu ubaguzi wa kubaguana kwa makabila.

"Katika Wilaya ya Siha, kuna makabila mengi wamo Wachaga, Wamasai, Wameru, Wagogo, Wanyaturu, Wasambaa, lakini pamoja na hayo kinachohitajika ni umoja ili kuleta maendeleo.

"Mwenzetu hapa (Lengere), yeye ni mkazi wa Siha aliyetoka katika jamii ya wafugaji, lakini umeona alivyoshirikiana na kuleta maendeleo, tumemuaga leo (juzi) amefanya mengi katika kuleta maendeleo kwenye wilaya yetu na sisi tumuige kwa hayo mazuri aliyoyafanya ya kujenga wilaya hii."

"Lazima kwanza tuanze kuwa na umoja ndani ya wilaya yetu tuachane na unafiki, chuki na fitina. Mmeona mwenzetu tulishirikiana nae kuijenga wilaya na amefanya mengi ndani ya serikali na chama, ameshiriki katika kujenga ofisi ya chama na ameshiriki kujenga Shule ya Sekondari Sekirari," alisema Mwanry.

Wakati wa uhai wake, Lengere aliwahi kuwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Embukoi, kada wa CCM aliyekuwa kiongozi tegemeo ukanda wa tambarare unaojumuisha jamii ya wafugaji wa Kimasai na kiongozi wa mila wa jamii ya wafugaji hao.

Kabla ya kufariki dunia, Lengere alikuwa akisumbuliwa na ugonjwa wa kiharusi kwa muda mrefu. Ibada ya mazishi ya kada huyo, iliongozwa na Mkuu wa Jimbo la Siha la Dayosisi ya Kaskazini ya Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Mchungaji Elisa Kileo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha, Godson Ngomuo, akizungumza katika msiba huo, aliwasisitizia viongozi kuzingatia misingi ya haki na usawa, kwa kuwatumikia wananchi na kuiga yale yote mazuri aliyoyafanya kada huyo.



Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, RPC Salumu Hamduni (wa pili kushoto), akitoa zawadi ya begi la shule kwa mmoja ya wanafunzi waliofanya vizuri katika mashindano ya masomo ya usalama barabarani yaliyotolewa na mabalozi wa usalama barabarani (RSA) mkoani hapo, kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Usalama Barabarani (RTO) kwa ufadhili wa Shirika la Foundation for Civil Society (FCS). Jumla ya shule 12 zilizoko katika maeneo ya barabara kuu mkoani Kilimanjaro zilishiriki mashindano hayo. **PICHA: JAMES LANKA**

# Mbunge apeleka shuka kusaidia wajawazito

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

TATIZO la uhaba wa mashuka linaloikabili Zahanati ya Makuyuni Wilaya ya Moshi, limemwibua Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Mkoa wa Kilimanjaro, Shally Raymond kupeleka mashuka 20 ili kupunguza adha hiyo kwa wajawazito na watoto wanaolazwa hospitalini hapo.

Zahanati ya Makuyuni iko katika Jimbo la Vunjo ambalo linaongozwa na Mbunge wa sasa, James Mbatia (NCCR-Mageuzi).

Msaada huo ulikabidhiwa jana kwa uongozi wa zahanati hiyo na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Umoja wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT), Kata ya Makuyuni, Aisha Mkwizu, kwa niaba ya mbunge huyo.

Katika taarifa yake, Shally alisema amefanya hivyo ili kusaidiana na serikali kupunguza baadhi ya matatizo yaliyopo katika sekta ya afya.

Alisema moja ya matatizo yanayozikumba zahanati zinazohudumia idadi kubwa ya wagonjwa ni upungufu wa mashuka na vitanda, na kwamba katika zahanati ya Makuyuni, yeye ameguswa kupunguza tatizo la mashuka ili kuwapa ahueni wagonjwa wanaopata huduma hospitalini hapo.

Ingawa katika jimbo hilo kuna zahanati nyingi, alisema ameanza na zahanati hiyo na ataendelea kutafuta wafadhili ili kusaidia maeneo mengine yenye uhitaji huo.

"Nimetoa mashuka haya ili kutekeleza ahadi yangu ya kutatua matatizo yaliyopo katika zahanati zetu, wajawazito tunajua wanakutana na changamoto wakati wanapojifungua, nikaona nisaidie kuleta mashuka," alisema Shally.

Mmoja wa wakazi wa Makuyuni, Anande Wehael, alimshukuru mbunge huyo kwa kutatua tatizo hilo, huku akimwomba aendelee kusaidia pia suala la ukarabati wa miundombinu ya zahanati hiyo.

Nipashe
Spotiko




NYOTA WA5 WANAOKERWA NA VIWANGO VYAO MSIMU HUU UK. 16&17




# MSHIKEMSHIKE...

Cristiano Ronaldo akifunga bao kwenye mchezo wake wa 1,000 tangu aanze kucheza soka la ushindani, wakati Juventus ilipoifunga SPAL mabao 2-0 kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia, Jumamosi. **PICHA: MTANDAO**

## ISIKUPITE

PASI ya mwisho 'assist' aliyoitoa winga kinda wa Arsenal, Bukayo Saka wakati Alexandre Lacazette akiifungia bao pekee wakiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Olympiacos kwenye mechi ya Europa League wiki iliyopita, inamfanya yosso huyo mwenye miaka 18, kufikisha pasi za mwisho tano msimu huu kwenye michuano hiyo ya Europa, ikiwa nyingi zaidi kuliko mchezaji yeyote.



SOKA




# WANAOWEZA KUVAA VIATU VYA POGBA UNITED

**MANCHESTER,** England

NYOTA wa Manchester United anayetaka kuondoka, Paul Pogba amekuwa akipamba vichwa vya habari katika vyombo vya habari licha ya kucheza mara saba tu kwenye Ligi Kuu ya England msimu huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kwa sasa anauguza maumivu ya enka na amekuwa akikumbwa na majeruhi ya mara kwa mara. Pogba alirudi dimbani Desemba na kucheza mechi mbili akitokea benchi dhidi ya Newcastle United na Watford, lakini tangu hapo hajaonekana kwenye kikosi cha kocha, Ole Gunnar Solskjaer.

Kocha huyo raia wa Norway hivi karibuni alimbwatukia hadharani wakala wa Pogba, Mino Raiola, ambaye ndiye anayeonekana kumhamasisha bingwa huyo wa Kombe la Dunia mwaka 2018 aondoke pale Old Trafford. Huku uvumi ukimhusisha na mpango wa kurudi Juventus, inaonekana wazi kwamba Pogba anaweza asiwe mchezaji wa Manchester United msimu ujao. Kwa hiyo, makala hii inakuchambulia viungo watano ambao wanaweza kuwa warithi wa Mfaransa huyo pale kwa Mashetani Wekundu.

**5. JUDE BELLINGHAM**

Akiwa na umri wa miaka 16, Jude Bellingham ameonekena kuwashika wengi nchini England baada ya kuonesha kiwango cha kuvutia akiwa na Birmingham City kwenye Ligi daraja la kwanza msimu huu. Kinda huyo ambaye aliingia kwenye timu ya wakubwa Agosti mwaka jana, tayari anatajwa kuwa ni mchezaji mwenye thamani ya pauni milioni 50, hasa kutokana na kiwango chake.

Bellingham ni aina ya kiungo anayependa kucheza ndani ya boxi huku akiwa na mbinu nyingi kwenye ushambuliaji. Licha ya umri wake kuwa mdogo, kinda hili la maajabu la Uingereza linaonekana kuwa na mwili ulijengeka na mwenye spidi kali dimbani. Uwezo wake wa kutengeneza nafasi nyingi kwa wachezaji wenzake, inaweza kumfanya kuwa msaada mkubwa kwa kikosi cha Man United.

**4. DONNY VAN DE BEEK**

Nyota wa Ajax wa msimu uliopita wanaondoka pale kwenye dimba la Johan Cruyff Arena kwa fedha nyingi kwenda kwenye klabu kubwa Ulaya. Wachezaji kama Frenkie de Jong, Matthijs de Ligt na Hakim Ziyech wamenunuliwa na Barcelona, Juventus na Chelsea, huku ripoti zikibainisha kwamba wengine wengi wanaweza kufuata.

Mmoja wao ni kiungo Donny van de Beek, ambaye amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia na kikosi hicho cha kocha, Erik ten Hag katika misimu ya hivi karibuni. Msimu uliopita kiungo huyo mwenye umri wa miaka 22 alifunga mabao 17 na kutoa asisti 13 kwenye mashindano yote. Ameendelea kuwa kwenye kiwango bora msimu huu akiwa na mabao 10 na asisti 10. Mashabiki wa Ajax hawatasahau bao la ushindi dhidi ya Tottenham Hotspur kwenye mchezo wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu uliopita.

Raia huyo wa Uholanzi anaonekana kuwa mrithi wa Pogba kutokana na kiwango chake, ubunifu na kipaji chake.

Hakuna shaka yoyote kwamba, de Beek ana nafasi ya kuwa kiungo bora duniani na uhamisho wake kwenda pale Manchester United unaweza kumweka kwenye ramani kubwa ya kisoka.

**3. SAUL NIGUEZ**

Nyota wa Atletico Madrid, Saul Niguez ana uwezo wa kuja kuwa kiungo bora duniani kwa sababu ya kiwango chake, uwezo wa kupiga pasi na kujituma dimbani. Timu ya kocha, Diego Simeone ni moja ya klabu barani Ulaya yenye kutumia falsafa ya ulinzi. Raia huyo wa Argentina amekuwa akiwataka wachezaji wake kucheza kwa kujituma, bila kujali staili ya uchezaji, lakini akiingiza timu uwanjani lengo lake ni moja tu kushinda.

Na hivyo, hujikuta wakicheza zaidi kwa staili ya mashambulizi ya kushtukiza. Hata hivyo, Niguez amekuwa na uwezo mkubwa kwa kuichezesha timu dimbani.

Mchezaji huyu mwenye umri wa miaka 25 anaweza kuwa msaada mkubwa zaidi kwa kikosi cha Manchester United kwenye safu ya kiungo na kuchukua mikoba ya Paul Pogba. Saul anaweza kuwa patina mzuri zaidi wa Bruno Fernandes aliyesajiliwa hivi karibuni.

**2. SERGEJ MILINKOVIC-SAVIC**

Kuchomoza kwa Lazio kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, msimu huu kumechangia mno na mabao ya Ciro Immobile, ambaye kwa sasa anaongoza kwenye mbio za kuwania kiatu cha dhahabu kwa ufungaji bora katika Ligi tano kubwa Ulaya mbele ya Robert Lewandowski na Cristiano Ronaldo. Hata hivyo, mafanikio makubwa ya klabu hiyo katika mbio za Serie A yanabebwa na uwepo wa kiungo, Sergej Milinkovic-Savic. Raia huyu wa Serbia amekuwa kwenye kiwango bora kabisa cha kuilisha mipira safu ya ushambuliaji na kama Manchester United wakimsajili watakuwa wameramba dume.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 tayari amejiimarisha yeye mwenyewe kwenye ligi hiyo ya Italia katika safu ya kiungo pamoja na timu ya taifa ya Serbia, hivyo kama Man United watamtwaa wakati wa kipindi cha majira ya joto ataweza kuwasaidia kwa kiwango kikubwa.

**1. YOURI TIELEMANS**

Manchester United mara kadhaa imekuwa ikihusishwa na mpango wa kutaka kumsajili kiungo mchezeshaji wa Leicester City, James Maddison baada ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 kuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi msimu huu. Kwa uwepo wa Bruno Fernandes aliyesajiliwa Januari, Man United sasa wanamhitaji zaidi Youri Tielemans mchezaji mwenzake na Maddison kwa ajili ya kuziba pengo la Paul Pogba akiondoka.

Kiungo huyu raia wa Ubelgiji anaweza kuisaidia zaidi safu ya ushambuliaji ya Manchester United kutokana na kiwango chake na katika umri wake wa miaka 22 atakuwa bidhaa nzuri zaidi kwa mashetani wekundu hao.

**JE, WAJUA?**

LIVERPOOL haikuweza kulenga shuti hata moja kwenye goli la Atletico Madrid wiki iliyopita kwenye mechi ya mkondo wa kwanza hatua ya 16-bora Ligi ya Mabingwa Ulaya, hiyo ikiwa ni kwa mara ya pili Wekundu hao wakishindwa kumjaribu golikipa wa timu pinzani tangu Jurgen Klopp achukue mikoba ya kuinoa timu hiyo mwaka 2015.



MICHEZO



# MECHI 8 MTIBWA SUGAR BILA USHINDI LIGI KUU

Na Adam Fungamwango

TANGU ilipokwenda Zanzibar kucheza Kombe la Mapinduzi na kulitwaa kwa kuifunga Simba bao 1-0 kwenye mechi ya fainali na kurejea Tanzania Bara, timu ya Mtibwa Sugar haijashinda mechi yoyote ile ya Ligi Kuu.

**Juzi Jumamosi iliendelea tena kugawa takrima, ilipobamizwa bao 1-0 dhidi ya Mbeya City kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya na kuzidi kujiweka pabaya kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Mara ya mwisho kushinda mechi yake ya ligi ilikuwa Januari 3 mwaka huu, ilipoifunga Mbao FC bao 1-0 kwenye Uwanja wa CCM Gairo, ikiwa ni kabla ya michuano ya Kombe la Mapinduzi.

Baada ya hapo, imecheza mechi nane za Ligi Kuu, imefungwa sita na kutoka sare mbili tu, yakiwa ni matokeo mabaya zaidi kuwahi kutokea kwenye historia ya klabu hiyo.

Katika mechi hiyo, Mtibwa imefungwa jumla ya mabao 10, ikifunga bao moja tu.

Kwa sasa inashika nafasi ya 14 kwenye msimamo, ikiwa imeshacheza mechi 24, ikiwa pia na pointi 24, sawa na pointi moja kila mechi.

Mtibwa Sugar kwa sasa haipo kwenye nafasi nzuri, kwani badala ya kupanda juu kimsimamo inaelekea chini kwenye timu zinazopigana kutoka kwenye msitari wa timu nne za mwisho zitakazoshuka daraja na mbili zitakazocheza michezo maalum, maarufu kama 'play off'.

Msemaji wa Mtibwa, Thobias Kifaru, amekiri kwenye timu yao haipo kwenye wakati mzuri, lakini akasema wanajitahidi kwa kila hali kuweka mambo sawa.

"Ni upepo mbaya umetupitia kwa sasa, lakini tunaahidi kuweka mambo sawa, hatutoshuka daraja kama baadhi ya watu wanavyosema, Mtibwa ni klabu kubwa sana." alisema Kifaru.

Zifuatazo ni mechi ambazo Mtibwa amecheza baada ya kutoka kutwaa Kombe la Mapinduzi mjini Zanzibar.

**1. MTIBWA SUGAR 0-2 KMC**

Mechi ya kwanza ya Mtibwa baada ya kutoka Zanzibar ilikuwa dhidi ya KMC kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam, Januari 17 mwaka huu.

Kwa hali ya kushangaza, mabingwa hao wakakumbana na kipigo cha mabao 2-0, yote yakifungwa na Sadallah Lipangile.

**2. MTIBWA SUGAR 1-1 AZAM FC**

Kwenye mechi hii Mtibwa ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Azam FC, mechi ilichezwa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam Januari 30 mwaka huu. Na ndiyo mechi pekee kati ya nane ilizocheza mpaka sasa ambayo imepata bao lililofungwa na Ismail Mhesa. Goli la Azam lilifungwa na Richard Djodi.

**3. MTIBWA SUGAR 0-1 YANGA**

Mtibwa ilicheza mechi yake ya tatu tangu itoke Zanzibar dhidi ya Yanga Februari 2 mwaka huu na ikachapwa bao 1-0 jijini Dar es Salaam, lililofungwa na David Molinga dakika ya 50, na kuzidi kuiweka kwenye wakati mgumu timu hiyo ambayo iliwahi kutwaa ubingwa wa Tanzania Bara mwaka 1999 na 2000.

**4. MTIBWA SUGAR 0-1 LIPULI FC**

Mkosi ulizidi kuiandama timu hiyo, kwani ilikwenda kucheza dhidi ya Lipuli FC kwenye Uwanja wa Samora mjini Iringa na kukutana na kipigo kingine cha bao 1-0. Mechi hiyo ilichezwa Februari 8, na bao pekee la washindi lilifungwa na Elias Mwinyi.

**5. MTIBWA SUGAR 0-3 SIMBA**

Siku tatu baadaye, Februari 11 mwaka huu, ikiwa kwenye uwanja wake wa nyumbani, Jamhuri Morogoro, Mtibwa ilikutana na dhoruba ya kuchapwa magoli 3-0 dhidi ya Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba.

Waliopeleka kilio Mtibwa ni John Bocco, Mohamed Hussein 'Tshabalala' na Hasaan Dilunga.

**6. MTIBWA SUGAR 0-1 JKT TANZANIA**

Mtibwa Sugar bado haikuwa na jipya ilipokwenda kucheza dhidi ya JKT Tanzania, Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam na kukutana na kipigo cha bao 1-0, likifungwa na Daniel Lyanga kwa mkwaju wa penalti, mechi ikichezwa Fabruari 15.


**7. MTIBWA SUGAR 0-0 PRISONS**

Februari 19, Mtibwa ilikwenda kutoa sare ya bila kufungana dhidi ya Prisons kwenye Uwanja wa Jamhuri mjini Dodoma ambao ulikuwa ukitumiwa na timu hiyo, kabla ya Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya kufunguliwa rasmi.

**8. MTIBWA SUGAR 0-1 MBEYA CITY**

Hii ilikuwa ni mechi ya Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, Mtibwa ikisafiri kwenda kuweka mambo sawa, lakini ilijikuta ikilala ugenini kwa bao 1-0 dhidi ya wenyeji Mbeya City kwa bao la mkwaju wa penalti iliyopigwa na Peter Mapunda.

NJE YA UWANJA



PENALTI ya Sergio Aguero aliyoiokoa Kipa wa Leicester City, Kasper Schmeichel wakati Manchester City ikishinda 1-0 kwenye Ligi Kuu England Jumamosi, ni ya nne kwake kuokoa katika ligi hiyo, ambapo ni moja zaidi alizookoa baba yake, Peter kwenye kipindi chake chote cha soka EPL.




PEPE

# NYOTA WATANO WANAOKERWA NA VIWANGO VYAO MSIMU HUU

**LONDON,** England

MSIMU wa 2019/20 umekuwa mgumu kwa wachezaji wengi katika ligi tano kubwa za Ulaya.

Kuelekea msimu huu kulikuwa na matumaini makubwa kwa baadhi ya wachezaji kutokana na kiasi kikubwa cha fedha walichonunuliwa. Baadhi wameweza kuishi kwenye ndoto zao, lakini wengine wameshindwa. Bila shaka majina kama Cristiano Ronaldo, Lionel Messi, Marcus Rashford na Kylian Mbappe yameendelea kutamba.

**Makala hii inakuchambulia wachezaji watano ambao wanaonekana kukerwa na viwango vyao msimu huu.**

**5. AARON RAMSEY**

Majaliwa ya Aaron Ramsey ulikuwa ni mjadala mrefu kwa kipindi chote cha msimu wote uliopita, huku Arsenal wakishindwa kufikia mahitaji ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales hasa kwa mshahara wake. Mwishoe kiungo huyo akafanikisha usajili wa kwenda nchini Italia na kupata mkataba wa miaka minne. Tangu alipojiunga Juventus kama mchezaji huru, Ramsey ameshindwa kuonesha kiwango chake. Katika mechi 12 alizocheza kwenye Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Ramsey amefunga bao moja na hajatoa asisti hata moja.

Ramsey ameshindwa kutamba nchini Italia na kocha Maurizio Sarri ameshindwa kumtumia kati ya yeye na Adrien Rabiot mbele ya Miralem Pjanic kutokana na wote kutokuwa kwenye kiwango cha juu.

Mashabiki wengi wa Juventus kwa sasa hawaoni umuhimu wa Ramsey na sasa wanamwona kama mzigo. Kama Ramsey anataka kuwalipa fadhira mabingwa hao wa Serie A kwa uwekezaji wao kwake, anatakiwa kuonyesha kiwango cha kuvutia kwenye safu ya kiungo.

**4. NICOLAS OTAMENDI**

Kuondoka bila kutarajia kwa Vincent Kompany wakati wa kipindi cha majira ya joto, kulimaanisha kwamba Nicolas Otamendi sasa angeweza kuwa kwenye mipango ya kocha, Pep Guardiola pale Manchester City. Badala yake raia huyo wa Argentina ameshindwa kuonesha kiwango chake na hivyo kusababisha Pep kutomtumia kwenye mechi nyingi. Kama hilo halitoshi, kocha huyo raia wa Hispania ameamua kumtumia kiungo mkabaji, Fernandinho mwenye umri wa miaka 34 kama beki wa kati.

Yote hayo yalianza kwenye mchezo uliopigwa pale katika dimba la Carrow Road, ambapo mabingwa hao watetezi walifurumushwa na Norwich iliyopanda daraja. Katika mchezo huo, Teemu Pukki alimkimbiza Otamendi kwa dakika zote 90. Sasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 amekuwa akikalia benchi katika kila mchezo. Ni wazi kwamba Pep hana imani na beki huyo na hata siku zake za kukaa pale Etihad zinahesababika.

**3. ANTOINE GRIEZMANN**

Miaka michache iliyopita, Lionel Messi - Luis Suarez - Neymar Jr. ilikuwa safu ya ushambuliaji inayoogopwa zaidi kwenye soka duniani. Tangu kuondoka kwa Neymar kumeacha kivuli kwa Messi na Barcelona wakaingia sokoni kwa ajili ya kutafuta mrithi wa nyota huyo wa Brazil. Waliwasajili Philippe Coutinho, Ousmane Dembele zaidi ni Antoine Griezmann. Mfaransa huyo amekuwa kwenye kiwango kisichovutia kabisa tangu atue hapo. Alisajiliwa kipindi kilichopita cha majira ya joto kwa pauni milioni 107 pale Katalunya na kupewa mkataba wa miaka 5.

Mchezaji ambaye alitarajiwa kutoa changamoto kwa wachezaji kama Messi na Ronaldo, lakini nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 amekutana na wakati mgumu tangu kutua kwake pale Nou Camp. Katika mechi 23 alizocheza kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, amefunga mabao 8 na kutoa asisti 4. Badala ya kuonekana kwenda kumsaidia kubeba mzigo Messi, sasa anaonekana amekwenda kuongeza uzito zaidi. Griezmann alionekana kama ndiye ambaye angechukua mikoba ya Messi, lakini ameshindwa kabisa kufikia hata robo ya kiwango chake.

**2. PHILIPPE COUTINHO**

Miaka miwili iliyopita, nani angeweza kufikiria kwamba Liverpool ingekuwa kwenye nafasi ya kushinda kombe la Ligi Kuu ya England kwa mara ya kwanza bila Philippe Coutinho. Raia huyo wa Brazil alikuwa nguzo ya Liverpool, lakini Barcelona walipomuita hakujali kuhusu Anfield. Sasa wekundu hao ni mabingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku Coutinho kiwango chake kilishuka vibaya na kupelekwa kwa mkopo kule Bayern Munich. Na sasa kule Ujerumani nako mambo magumu na Bayern hawataki kumnunua kwa mkataba wa kudumu mwishoni mwa msimu.

Kiukweli mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 haanzi kwenye mchezo wowote wa Munich, huku Thomas Muller akiwa amerudi kwenye kiwango chake. Katika mechi 19 za Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Coutinho amefunga mara 6. Kiwango cha Coutinho kinaonekana kushuka kwa kasi ya ajabu. Baada ya Coutinho kushindwa kutamba Ujerumani nini utakuwa mwisho wake? Kwa uhakika hakuna klabu ya Ulaya itakayokuwa tayari kumpa nafasi.

**1. NICOLAS PEPE**

Alisajiliwa kwa pauni milioni 72 kipindi cha majira ya joto, ukiwa usajili ulioweka rekodi kwa klabu ya Arsenal, lakini kiwango chake kimeshuka vibaya kwenye mwanzo wake wa maisha ya soka England. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ivory Coast ni wazi mambo yanaonekana kwenda kombo pale katika dimba la Emirates. Hata hivyo, ukizingatia kiasi cha fedha alichonunuliwa mchezaji huyo, kiwango chake kinaonekana hakina msaada kwa timu. Msimu huu Nicolas Pepe amefunga mabao 3 na kutoa asisti 3 katika mechi 21 za Ligi Kuu.

Maisha yake pale kwenye dimba la Emirates inaonesha ni kama hana mchango wowote kwa timu na pia nafasi ya kuanza kikosi cha kwanza nayo imekuwa ngumu kwa upande wake. Mwanzo mashabiki wa Arsenal walikuwa na matumaini makubwa mno na nyota huyo ambaye alionesha kiwango cha kuvutia zaidi katika Ligi Kuu ya Ufaransa.

Hata mashabiki wa Manchester United waliokuwa wanamfananisha Pepe na nyota wao Daniel James sasa wanajua kwamba walikosea.

## Nukuu


Mashabiki wa Atletico ambao wanaweza kupata tiketi nawakaribisha Anfield, hisia ni muhimu. Usiku ule kwa vyovyote ulikuwa mzuri zaidi kwa Atletico, lakini naangalia mbele kuelekea mchezo wa pili. Niliona sura nyingi zenye furaha kwa Atletico, lakini mambo bado hayajaisha, watakuja Anfield," **Kocha wa Liverpool, Jurgen Klopp baada ya kupigwa bao 1-0 na Atletico kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa.**



"Kiukweli, hivi karibuni nilifaulu mtihani wa kupata uraia wa Uingereza, ilikuwa ngumu. Maswali ni magumu sana, hata marafiki zangu Waingereza walishindwa kupata majibu yake! Nilishindwa mtihani mara mbili na mara hii ya tatu ndio nimefaulu na sasa mimi ni raia wa Uingereza! Hivyo, London ndio sehemu ninayotaka kukaa. Hapa ndio nilipo na familia yangu, kanisa langu, nataka binti zangu wakulie hapa," **Mbrazil Willian akieleza hata kama akiachana na Chelsea hatahamisha familia yake London.**




"Kama klabu haitanifukuza, nitabakia hapa kwa asilimia 100 na zaidi ya hapo. Kwanza kwa sababu nataka kubakia hapa zaidi ya mkataba wangu nilionao. Ni kitu fulani maalumu, nataka kubakia, nataka kuisaidia klabu, kama inawezekana, kuendelea kuifanya klabu iwe kwenye kiwango kilekile, kwa nini niondoke wakati nilishasema mwezi mmoja uliopita kwamba naipenda klabu hii na nataka kubakia hapa," **Kocha wa Manchester City, Pep Guardiola.**





# BAO LA DIDA LILIVYOMPELEKA ANGA ZA KASEJA

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA wa Lipuli ya Iringa, Deogratius Munishi 'Dida', ameweka rekodi ya kuwamo kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu msimu wa 2019/20, baada ya kupachika bao Jumanne iliyopita kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, alipofunga bao kwenye mechi ambayo timu yake ilicheza dhidi ya Mbeya City.

**Katika mechi hiyo ambayo Lipuli ilchapwa mabao 2-1, Dida alifunga bao la kufutia machozi kwa mkwaju wa penalti dakika za majeruhi.**

Bao hilo si tu linamwingiza kwenye orodha ya wafungaji kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, lakini pia linamwingiza kwenye orodha ya magolikipa wachache nchini kufunga magoli kwenye ligi.

Dida alijiunga na Lipuli kwenye kipindi cha dirisha dogo la uhamisho na sasa anaonekana kuwa ndiye kipa namba moja kwenye kikosi hicho.

Alionekana na mashabiki wengi wa soka nchini kwenye mechi dhidi ya Yanga Februari 5 mwaka huu, Lipuli ikilala mabao 2-1, lakini alionyesha umahiri mkubwa kwenye mechi dhidi ya Simba kwenye Uwanja wa Samora mjini Iringa, lakini timu yake ikilala bao 1-0.

Kabla ya kujiunga na Lipuli, Dida kwa muda wa miezi sita alikuwa hana timu yoyote na aliutumia muda huo kwenye shughuli za kilimo na ufugaji, na sasa amerejea tena kikamilifu, akiandika na rekodi ambazo hajapata kuziweka kwenye soka la Bongo.

Hakupata timu yoyote mwanzo wa msimu, baada ya kumaliza mkataba na Mabingwa wa Soka Tanzania Simba baada ya kuitumikia kwa misimu miwili.

Mwandishi wa makala haya anakuletea rekodi za makipa waliofunga magoli kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania mpaka sasa.

**IDD PAZI 'FATHER'-SIMBA VS YANGA (1984)**

Kipa wa kwanza Tanzania kuweka rekodi ya kufunga goli kwenye Ligi Kuu ni Idd Pazi , maarufu kama 'Father', mchezaji wa kwanza kabisa nchini kuitwa Tanzania One.

Pazi, kipa wa zamani wa Coastal Union, Majimaji, Simba na Taifa Stars, alifunga bao kwa mkwaju wa penalti kwenye mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga iliyochezwa kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam ambayo kwa sasa unaitwa Uwanja wa Uhuru.

Alilifunga kwenye dakika ya 20, baada ya Simba kupata mkwaju wa penalti, lakini kwenye dakika ya 70, winga machachari wa Yanga wakati huo, Omari Hussein aliisawazishia Yanga na mechi ikaisha kwa sare ya bao 1-1, mechi ikichezwa Machi 10, 1984.

**JUMA KASEJA-YANGA VS TOTO AFRICAN-(2009)**

Kipa maarufu nchini Juma Kaseja ndiye anayeongoza kwa kufunga magoli mengi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara mpaka sasa.

Tayari amepachika magoli mawili. Ilikuwa ni Machi 24, 2009, kwenye msimu wa Ligi Kuu 2008/09 wakati akiidakia Yanga aliweka rekodi ya aina yake kwa kufunga bao kwa njia ya kawaida tu.

Ilikuwa ni dakika ya 22, alipopiga mpira mrefu kutoka golini kwake na ukaenda moja kwa moja hadi wavuni, kipa wa Toto akiwa amesongea mbele.

Mechi hiyo ya Ligi Kuu ilichezwa Uwanja wa CCM Kirumba na Yanga iliibuka na ushindi wa mabao 2-1, moja likifungwa na Kaseja na lingine Mike Barasa dakika ya 32, huku la kufutia machozi likiwekwa wavuni na Hussein Swedi.

**JUMA KASEJA-SIMBA VS YANGA (2012)**

Kaseja alifunga goli lingine Mei 6, 2012 wakati huo akiwa amerejea kwenye klabu yake ya Simba.

Ilikuwa ni mechi ya watani kati ya Simba dhidi ya Yanga kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam wakati huo ukiwa mpya kabisa.

Kipa huyo alichangia ushindi wa mabao 5-0 iliyoupata Simba dhidi ya watani zao wa jadi kwenye Ligi Kuu msimu wa 2011/12.

Kaseja alifunga bao dakika ya 69 kwa mkwaju wa penalti, Felix Sunzu akifunga kwa penalti dakika ya 58 na marehemu Patrick Mafisango pia akifunga kwa penalti dakika ya 72. Magoli mawili yaliyofungwa kwa njia ya kawaida yaliwekwa nyavuni na Emmanuel Okwi dakika ya kwanza na 61.

**DEO MUNISHI-LIPULI VS MBEYA CITY (2020)**

Deogratius Munishi naye sasa ameingia kwenye anga hizo baada ya kufunga goli kwa mkwaju wa penalti Februari 18 mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine mjini Mbeya, akifunga dakika ya 90, Lipuli ikilala mabao 2-1.

Linakuwa ni goli la nne kuingia kwenye orodha ya magoli yaliyofungwa na magolikipa kwenye Ligi Kuu ya Tanzania. Selemani Omari na Peter Mapunda waliifungia Mbeya City.


**NAJUA WAJUA**



BAO alilofunga Erling Braut Haaland wakati Borussia Dortmund ikishinda 2-0 dhidi ya Werder Bremen juzi, Jumamosi ni la 40 kwake msimu huu kwenye mechi 30 alizocheza hadi sasa.

SOKA

# MASTAA WATAKAOIKIMBIA CITY KWA KIFUNGO UEFA




WAN-BISSAKA

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester City imefungiwa kwa misimu miwili kutoshiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kutozwa faini ya euro milioni 30 na shirikisho la vyama vya soka barani Ulaya.

**Wakati mashabiki na wachambuzi wengi wa soka wakibashiri matokeo yatakavyokuwa kwenye rufani waliyoikata nanamna gani City ya kocha Pep Guardiola itakavyokabiliwa na wakati mgumu, swali kubwa limeibuka kwa kila mmoja. Nini kitatokea kwa wachezaji wakubwa wa klabu hiyo?**

Huku City ikiwa moja ya klabu kubwa barani Ulaya kwa miaka mingi sasa, wachezaji wengi wanaojiunga na timu hiyo wamekuwa na matarajio makubwa ya kucheza kwenye mashindano ya Ulaya, huku Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiwa kipaumbele kikubwa, na sasa kufungiwa kushiriki mashindano hayo kunaibua maswali mengi kama wachezaji nyota watashawishika kubakia hapo.

Makala hii inawaangalia wachezaji watatu ambao kwa namna yoyote wanaweza kutimka hapo Manchester City kutokana na adhabu hiyo ya kufungiwa kushiriki michuano ya Ulaya.

### #3 RAHEEM STERLING

Pengine Raheem Sterling anaweza kujiona ni mtu asiye na bahati. Winga huyu Muingereza aliondoka Liverpool kwa matarajiao ya kwenda kushinda mataji zaidi na Manchester City, kwa pamoja ya nyumbani na yale ya kimataifa. Sasa waajiri wake wa zamani Liverpool ni mabingwa watetezi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, huku klabu yake ya sasa ikifungiwa kushiriki mashindano hayo.

Kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 aliamua kuondoka Liverpool na kujiunga na Manchester City bila kufikiria sana, ni wazi kwamba anaweza kwenda kwa miamba ya ama Italia, Hispania au Ujerumani, ambayo itakuwa na nafasi ya kubeba taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mshambuliaji huyo anaweza kuigharimu klabu itakayomtaka fedha nyingi, hasa kutokana na kuwa mmoja wa wachezaji Waingereza mwenye ushawishi mkubwa kwa sasa.

### #2 KEVIN DE BRUYNE

Kevin De Bruyne ni mchezaji mwingine ambaye anaweza kufikiri kuhusu majaliwa yake pale Manchester City baada ya kuondolewa kushiriki michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Pengine ndiye mchezaji mwenye kipaji kubwa zaidi pale Manchester City ambaye anaweza kucheza katika nafasi nyingi tofauti, na sasa anaonekana kuvuta macho ya wengi.

Mchezaji huyu wa kimataifa wa Ubelgiji ni mmoja wa wachezaji bora duniani na anaweza kufiti kucheza katika klabu yoyote Ulaya na anaweza kuongeza thamani kubwa kwenye kikosi chochote - sio tu kiufundi, lakini kwa morali. Kumpoteza yeye litakuwa pigo kubwa kwa City ambao wamempa kitambaa cha unahodha wakimwona kama nahodha wa muda mrefu wa klabu hiyo.

Ni ngumu kusema kama De Bruyne atakosa Ligi ya Mabingwa Ulaya kwani itakuwa ni "dhambi" michuano hiyo kumkosa mchezaji wa aina yake hasa wakati huu akiwa kwenye kiwango bora kabisa.

### #1 SERGIO AGÜERO

Sergio Aguero amenukuliwa mara nyingi sana akisema hataondoka Manchester City hadi ashinde taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini umri wake unaonekana kumtupa mkono raia huyo wa Argentina sasa hataweza kucheza michuano hiyo akiwa na klabu hiyo baada ya kufungiwa, hivyo kwa vyovyote anaweza kubadili maamuzi yake.

Akitajwa kama mchezaji bora zaidi wa kigeni kwenye Ligi Kuu ya England na Alan Shearer, Aguero alikuwa akisukuma mafanikio ya Manchester City kwa sapoti ya David Silva, Kevin De Bruyne na Vincent Kompany kwa muongo mmoja uliopita.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 umri unazidi kumtupa mkono siku hadi siku, lakini mabao yake hayawezi kumfanya umri wake kushuka, na bado anaonekana kwamba anauwezo wa kuendelea kufunga zaidi na zaidi. Kipindi cha majira ya joto kijacho kinaweza kumshuhudia Aguero akiondoka hapo City kama watashindwa kwenye rufani yao na ana uwezo wa kujiunga na klabu yoyote kubwa barani Ulaya.

CRISTIANO Ronaldo amefikisha mechi 1,000 tangu aanze kucheza soka la kiushindani kwa staili ya aina yake baada ya Jumamosi kufunga bao, wakati Juventus ikishinda 2-1 dhidi ya SPAL, ambapo sasa amefunga katika mechi 11 mfululizo za Serie A na kuifikia rekodi ya Gabriel Batistuta na Fabio Quagliarella.



NDANI YA 18

Nipashe
Spotika



MSIMU wa 2019/20 umekuwa mgumu kwa wachezaji wengi katika ligi tano kubwa za Ulaya. Kuelekea msimu huu kulikuwa na matumaini makubwa...

Uk. 16&17




# SABABU 3 KWA NINI LIVERPOOL ITAITOA ATLETICO 16-BORA UEFA

**LIVERPOOL,** England

HATUA ya 16 ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mara zote inakuwa ni ya kuvutia na tayari wiki iliyopita tumeshuhudia mshangao wakati Atletico Madrid - amabo kiwango chao kimekuwa sio cha kuvutia sana msimu huu wakiwakwanyua mabingwa watetezi wa mashindano hayo Liverpool 1-0 katika dimba la Wanda Metropolitano.

Baada ya mchezo huo, beki wa Liverpool, Andrew Robertson alibainisha kwamba wachezaji wa Atletico na kocha, Diego Simeone "walisherehekea kama wameshinda mechi zote mbili", lakini ushindi wao wa 1-0 unawapa faida ya uongozi kuelekea mchezo wa pili, kuna nafasi kubwa kwa kikosi hicho cha kocha Jurgen Klopp kuweza kupindua matokeo na kutinga robo fainali.

Hapa tunaangalia sababu 3 kwanini Liverpool bado wanaweza kuifunga Atletico Madrid na kufuzu hatua inayofuata kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya.

**#1 HISTORIA INAWEZA KUJIRUDIA**

Atletico Madrid na mashabiki wake wanaweza kuwa na furaha kubwa ya matokeo hayo na kwa uhakika kabisa kilikuwa kiwango cha kuvutia kwani waliwanyima kabisa Liverpool nafasi hata ya kupiga shuti langoni kwao. Lakini wakirudi kwenye akili yao, lazima watakuwa wanafikiri kuhusu kilichotokea msimu uliopita - wakati kitu kama hicho kilipotokea kwenye hatua hiyo ya 16 walipocheza na Juventus.

Kikosi hicho cha kocha Diego Simeone kwenye mchezo wa kwanza dhidi ya miamba hao wa Italia kilishinda 2-0 pale pale kwenye dimba la Wanda Metropolitano huku mabao yake yakifungwa na walinzi wa kati, Diego Godin na Jose Gimenez. Na kama ilivyotokea wiki iliyopita kwa Liverpool, kibibi kizee hicho cha Turini kilizuiwa kabisa kupiga mashuti langoni mwa Atleticho licha ya kuwa na washambuliaji wawili wakali Cristiano Ronaldo na Paulo Dybala.

Lakini katika mchezo wa marudiano pale kwenye dimba la Allianz, Juve iliongoza ndani ya dakika 49 kwa mabao mawili ya Ronaldo na nyota huyo wa kimataifa wa Ureno akafunga la tatu dakika ya 86 na kuwatupa nje Atletico.

**#2 ANFIELD UWANJA MGUMU**

Kila timu kubwa, zinapenda kuutumia uwanja wao wa nyumbani kama sehemu ya "mauaji'. Viwanja vikubwa vya miamba wa Ulaya kama Manchester City pale Etihad au Arsenal kule Emirates mara kwa mara vinaonekana kutokuwa vigumu kwa timu ngeni.

Lakini hii ni tofauti na pale Anfield. Mashabiki wa Liverpool wanakuwa na nguvu kubwa ya hamasa kwenye uwanja wao na kuwapa nguvu kubwa wachezaji wao. Hivyo uwanja wa Anfield sio sehemu rahisi kwa timu ngeni kupata matokeo.

Kama ilivyokuwa kwa Barcelona ambao walikuwa wanaongoza kwa mabao 3-0 kwenye mchezo wao wa kwanza wa nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, lakini walipofika pale Anfield mambo yaliwageukia na kuchezea kichapo cha mabao 4-0.

**#3 LIVERPOOL LAZIMA WAFUNGE**

Hata kama Atletico wangeifunga Liverpool 2-0 au hata 3-0 kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya mtoano wa timu 16, wasingeweza kuizuia kupata bao kwenye mchezo wa marudiano. Sasa ushindi wa 1-0 kwenye mchezo wa kwanza ni wazi kwamba Atletico wana kazi kubwa mno katika mchezo wa marudiano.

Nafasi ya Atletico kuwazuia Liverpool kutopiga shuti hata moja langoni mwao kwenye mchezo wa kwanza, ni wazi kwamba kwenye mchezo huu wa marudiano hawataweza.

Kiukweli kabisa timu yenye wachezaji wenye vipaji kama Mo Salah, Roberto Firmino na Sadio Mane kuwazuia kufunga ni ngumu mno.

**USILOLIJUA**



KIKOSI cha Frank Lampard, Chelsea imekuwa timu ya kwanza kuifunga nyumbani na ugenini timu inayonolewa na Jose Mourinho katika msimu wa kwanza wa ligi.







Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, wakipokelewa kwa kupigiwa makofi na wanafunzi wa Shule ya Msingi Itiki wilayani Rungwe, mwishoni mwa wiki, wakati wa ziara ya kamati hiyo iliyolenga kukagua miradi ya maendeleo wilayani humo, ikiwamo ya elimu na afya. **PICHA NA NEBART MSOKWA**

# Wasafirisha wagonjwa, maiti kwa machela na bodaboda

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI wa kata tatu za wilaya za Mbeya na Rungwe mkoani Mbeya na Wilaya ya Ileje mkoani Songwe, wamesema wanabeba wagonjwa na maiti kwenye machela na pikipiki, kutokana na miundombinu ya barabara katika maeneo yao kuwa mibovu.

Kata hizo zinazokabiliwa na tatizo ni zile zilizopo mpakani mwa wilaya zote tatu ambazo ni Ngulilo iliyopo Wilaya ya Ileje, Santilia ambayo ipo Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na Kata ya Mkunga wilayani Rungwe ambazo kwa ujumla zina vijiji zaidi ya 10.

Wakizungumza na wanahabari juzi wakati walipoungana kuchimba barabara kwa kutumia majembe ya mkono, wananchi hao walidai kuwa barabara hiyo imetelekezwa na serikali kwa muda mrefu na kwamba halmashauri zote zinakataa kuwajibika.

Mawazo Mwambwiga, mkazi wa Kijiji cha Sanje kilichopo Kata ya Santiliya katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, alisema barabara hiyo ndiyo mpaka kati ya Wilaya ya Mbeya na Rungwe.

Alisema wanashirikiana na wananchi wa Ileje kuchimba barabara hiyo kwa sababu na wao ndiyo wanayoitegemea wanapoenda kununua mahitaji yao katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi ama Mbeya Mjini.

"Tunamwomba Waziri mwenye dhamana na hizi barabara, atusaidie maana hawa viongozi wetu wameshindwa kutusaidia, ukienda Rungwe wanasema sio ya kwao na Mbeya nao wanasema sio ya kwao, shughuli zetu zinakwama," alisema Mwambwiga. Naye Asha Mwawa, mkazi wa Kijiji cha Sapanda Kata ya Ngulilo wilayani Ileje, alisema kutokana na hali ya barabara hiyo kwa sasa wanawake wengi wanaogopa kushika mimba wakihofia kupata shida ya usafiri wakati wa kwenda kujifungua.

Alisema katika kipindi chote cha mvua magari hayawezi kupita kutokana na barabara hiyo kuwa na mashimo mengi ambayo hata pikipiki wakati mwingine zinashindwa kupita. "Ukiwa mjamzito unataka kujifungua inakuwa ni shida, mashimo ya barabara hii hata ukibebwa kwenye pikipiki unaweza ukampoteza mtoto ama wewe mwenyewe, tunaomba serikali itusaidie kabla madhara makubwa hayajatukuta," alisema Asha.

Petro Lyamba, alisema kutokana na ubovu wa barabara hiyo, uchumi wao umeanza kuyumba kutokana na kushindwa kusafirisha mazao yao kwenda sokoni.

Alisema uchumi wa wananchi wa eneo hilo unategemea kilimo cha viazi, pareto, mahindi na miti ya mbao na kwamba soko kubwa la mazao hayo lipo kuanzia katika Mji wa Mbalizi. Alisema kwa sasa wanauza mbao mpaka Sh. 500 na viazi Sh. 4,500 mpaka 5,000 kwa kipeto ambacho huwa kinauzwa mpaka Sh. 20,000 hivyo akaiomba Serikali Kuu kuingilia kati.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Sapanda, Samwel Lusubilo, alisema pamoja na barabara hiyo kutelekezwa kwa muda mrefu, lakini viongozi wa Wilaya ya Rungwe wamekuwa wakikusanya ushuru wa mazao yanayopitishwa huku viongozi wa Mbeya wakidai kuwa haina mapato kwao.

Alimwomba Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Isack Kamwelwe, kutembelea barabara hiyo ili awasaidie kufanya maamuzi ambayo yatawaokoa.

# CWT yatoa mifuko 200 ujenzi shule maalumu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA cha Walimu Tanzania (CWT), kimeunga mkono maono ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila, ya kuanzisha shule maalumu za sekondari katika kila Halmashauri ya Mkoa huo ambazo zitakuwa zinapokea wanafunzi wanaofanya vibaya kwenye mitihani ya kidato cha nne.

Hivi karibuni Chalamila aliagiza maofisa Elimu Sekondari na Msingi wa Halmashauri zote za mkoa huo, kuandaa mipango ya ujenzi wa shule hizo ambazo zitakuwa zinapokea wanafunzi wanaopata daraja sifuri na daraja la nne kwenye mitihani ya kidato cha nne.

Alisema wanafunzi hao watakaokuwa wanapokelewa kwenye shule hizo watakuwa wanasoma miaka miwili yaani kidato cha tatu na nne kisha wanarudia kufanya mtihani wa taifa na wakifauru wanaendelea na masomo.

Mwishoni mwa wiki, CWT iliwasilisha mchango wa mifuko 200 ya saruji kwa ajili ya kuunga mkono ujenzi wa shule hizo utakapokuwa umeanza huku kikidai kuwa maono hayo ni mazuri.

Akiwasilisha mchango huo kwa niaba ya viongozi wa chama hicho taifa, Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Mbeya, Mwalimu Nelusigwe Kajuni, alisema chama hicho kiliguswa na maono kwa maelezo kuwa ni mazuri na ndio maana kiliamua kutoa mchango huo.

Kajuni alisema chama hicho kinatamani maono hayo yatekelezwe nchi nzima ili wanafunzi wote wanaofeli kwenye mitihani ya taifa warudie kufanya mitihani hiyo katika mfumo rasmi tofauti na sasa ambapo huwa wanarudia kwenye vituo vya watu binafsi.

"Viongozi wetu wa juu waliguswa sana na maono haya, sisi walimu ndio tunajua matatizo ya wanafunzi kusomea kwenye mazingira magumu na moja ya majukumu ya chama chetu ni kushirikiana na serikali kuboresha miundombinu, sasa tumechangia mifuko hii ili isaidie," alisema Kajuni.

Alisema fedha zilizotumika kutoa mchango huo zinatokana na michango ya walimu ambao huwa wanakatwa kwenye mishahara yao asilimia mbili.

Akizungumza wakati wa kupokea mchango huo, Chalamila aliushukuru uongozi wa CWT kwa kuunga mkono jambo hilo huku akisisitiza kuwa mpango huo ni lazima utekelezwe.

# Tuhuma mauaji ya bodaboda

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kuhusika na matukio ya kuwateka waendesha pikipiki maarufu kwa jina la 'Bodaboda', kuwaua na kupora pikipiki zao nyakati za usiku.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, alisema watuhumiwa wanatuhumiwa kushiriki katika matukio mbalimbali ya uporaji nwa pikipiki hizo.

Aliwataja watu hao ni Masikitiko Pastoni maarufu kwa jina la Mbuzi (34), Ezekia Sinkala (26) na Huruma Mwasile (36), wote wakazi wa Mtakuja pamoja na Amani Mswima (21), mkazi wa Mlima Reli katika Malmaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi.

Alisema watuhumiwa walikamatwa kuanzia Februari 12, mwaka huu baada ya Jeshi la Polisi kufanya msako maalumu katika maeneo mbalimbali ya mji huo wa Mbalizi uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

"Tumewahoji watuhumiwa hawa na wamekiri kuhusika kwenye baadhi ya matukio ambayo yalitokea hivi karibuni yakiwemo ya mauaji ya madereva wetu, sasa tunaendelea na upelelezi zaidi ili kujua matukio mengine waliyoshiriki," alisema Kamanda Matei.

Aliyataja baadhi ya matukio ambayo watuhumiwa hao walikiri kushiriki ni kumuua kwa kumchoma na kitu chenye ncha kali dereva bodaboda, Zacharia Jackson (30) kisha kumpora pikipiki yake aina ya T- Better yenye namba za usajili MC. 149 CFJ Desemba 20 mwaka jana.

Tukio lingine ambalo Kamanda Matei alisema watuhumiwa walikiri kushiriki ni kumuua dereva bodaboda, Shukuru Juma (26) kisha kumpora pikipiki yake aina ya King Lion, tukio ambalo lilitokea Februari 10 mwaka huu.

Alilitaja tukio lingine kuwa ni la kumvamia na kumkata na kitu chenye ncha kali dereva bodaboda, Sadock Nimrod (21) kisha wakamnyang'anya pikipiki yake na kutokomea.

Alisema katika Mkoa huo matukio ya wizi wa pikipiki yamekuwa yakiongezekana, hivyo akawatahadharisha wahusika wengine wa matukio hayo kuacha mara moja tabia hiyo kwa maelezo kuwa jeshi lake litawamaliza.



# Magereza kujenga nyumba gharama nafuu

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

JESHI la Magereza mkoani Dodoma limesema litaendelea kujenga nyumba za gharama nafuu ili kutatua tatizo la uhaba wa nyumba za watumishi wa jeshi hilo.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Magereza mkoani humo, Keneth Mwambije, katika ukaguzi wa nyumba 20 za maofisa wa jeshi hilo. Alisema mradi huo ni endelevu na pia unahusisha ufyatuaji matofali ambayo huuza na mengine kutumika katika mradi.

Wanatarajia pia kutambulisha miradi mbalimbali ambayo wamepanga kuifanya kwa mwaka huu.

"Hizi nyumba tumetumia Sh. milioni saba katika ujenzi, tungetumia nguvu kazi toka nje ya Magereza gharama ingekuwa kubwa sana," alisema.

Alisema kauli ya Kamishna Jenerali wa Magereza wameichukua kama agizo na wanakwenda kuifanyia kazi ipasavyo.

Jeshi hilo pia limejipanga kufanya kazi zao kwa kujitegemea bila kuomba msaada sehemu yoyote.

Alieleza kuwa lengo lao ni kuona ujenzi wa nyumba hizo unakuwa mradi endelevu wa Magereza ambao utasaidia kutatua upungufu wa nyumba za watumishi wa jeshi hilo hapa nchini.



Mbunge wa Viti Maalumu (CCM) Jimbo la Dodoma, Verister Bura, akizungumza na waumini juu ya umuhimu wa kuombea uchaguzi mkuu wa mwaka huu ili uwe na amani kwenye kanisa la Tanzania Mothodist Church Dodoma katika ibada ya kumsimika Askofu wa Jimbo, John Mjelwa, iliyofanyika kwenye kanisa hilo jana. **PICHA PETER MKWAVILA**

# Sababu kupungua bajeti Jiji la Dodoma zatajwa

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi, amesema makadirio ya bajeti ya mwaka 2020/21 yamepungua hadi Sh. bilioni 47, kutokana na uuzaji viwanja kupungua.

Katika bajeti ya mwaka wa fedha 2019/20, jiji lilikadiria kukusanya Sh. bilioni 72 kutoka katika vyanzo vyake mbalimbali ikiwamo uuzaji wa viwanja na hadi kufikia Desemba 2019, lilikuwa limekusanya Sh. bilioni 75.

Akizungumza katika kikao cha Baraza la Madiwani wa jiji hilo, Kunambi alisema bajeti ya mwaka ujao wa fedha wamepunguza kutokana na mwaka uliopita kulikuwa na mauzo makubwa ya viwanja ikilinganishwa sasa.

Vile vile, mwaka jana jiji hilo liliongoza kimapato kutokana na mapato ya viwanja kuwa juu.

"Nashukuru Mungu na watendaji wetu wako vizuri katika makusanyo ya mapato, kwa kuwa mpaka Desemba tumekuwa tukiongoza kwa mapato kwa Sh. bilioni 75," alisema Kunambi.

Alisema, bado kuna maeneo ambayo hayajatembelewa, hivyo mkakati wa sasa, ni kutembelea maeneo yote ya makusanyo ili kuongeza mapato ya jiji hilo.

"Unajua Dodoma hivi sasa ni jiji ndio Makao Makuu ya nchi, hivyo ni lazima tujiongeze kukusanya mapato, ili kutekeleza miradi ya maendeleo kwa kutumia fedha za ndani," alisema Kunambi.

Baadhi ya madiwani wakichangia mjadala wa bajeti, waliomba halmashauri hiyo kuwajengea barabara za mitaani ambazo zimeharibika kutoka na mvua.

Kwa upande wake, Mratibu wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (Tarura) jijini hapa, Mhandisi Geoffrey Mkinga, alisema kwa mwaka 2020/21 wametenga Sh. bilioni 4.39 kwa ajili ya kutengeneza barabara yenye urefu wa kilometa 333.

"Tuna ufinyu wa bajeti, hivyo niwaombe madiwani kama mna wadau wa maendeleo, wapelekeni kwa Mkurugenzi ili kusaidia ujenzi wa baadhi ya barabara," alisema.

Naye, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Patrobas Katambi, aliwataka waratibu wa Tarura kufika katika vikao vya Baraza la Madiwani ili kujua maeneo ambayo yana kero za barabara.

"Katika vikao vya madiwani ndio kuna taarifa mbalimbali za ukaguzi, hivyo ni rahisi kujua maeneo gani ambayo yanashida ili kufanyiwa kazi," alisema Katambi.

Akizungumzia kuhusu makusanyo, Katambi alisema, licha ya kuongoza katika ukusanyaji mapato jiji hilo bado hawakusanyi ipasavyo kutokana na baadhi ya nyumba za wageni kutolipa kodi.

"Tunaanza msako katika magesti, maana kuna baadhi ya nyumba hizo hazilipi ipasavyo kwa kila anayelala humo anatakiwa kuandikwa katika kitabu cha vitabu vya halmashauri ili kupata kodi zetu," alisema Katambi.

# Waganga tiba mbadala wapewa elimu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAGANGA wa asili na tiba mbadala wametakiwa kutengeneza dawa na kuziweka katika mfumo wa vifungashio vyenye ubora ili kutumika ndani na nje ya nchi.

Rai hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Mkurugenzi msaidizi anayesimamia huduma ya asili ya tiba mbadala kutoka Wizara ya Afya Maendeleo ya Jamii Jinsia Watoto na Wazee, Dk. Paul Peter, kwenye mafunzo ya tiba mbadala ya asili.

Dk. Peter alisema waganga hao wakipata elimu ya kutosha watakuwa na viwanda vidogo ambavyo vitatengeneza dawa na kuziweka kwenye vifungashio bora ili kuuza ndani na nje ya nchi.

Alisema hivi sasa Serikali ya Tanzania imeridhia huduma ya tiba mbadala ya asili.

"Sheria ya tiba asili kifungu na 23 iliyotungwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano Tanzania na kutoa usajili wake mwaka 2010 kwa chama cha umoja wa waganga wa waganga Tanzania (UWAWATA), mpaka sasa serikali imesajili waganga wa tiba asili na mbadala 22 nchi nzima na vituo vyake 715," alisema.

Alisema hatua hiyo itasaidia waganga hao kutofanya tiba kienyeji.

Mwenyekiti wa umoja huo wa tiba asili Mkoa wa Kagera, Rajabu Rugemalila, aliwaasa waganga hao kujiendeleza kielimu zaidi na mafunzo ili kujiepusha na uganga wa kitapeli ambao hivi sasa umeingiliwa na kusababisha kuchafuliwa kwa huduma hiyo.

Alisema waganga wa kienyeji wakishiriki kwenye mafunzo watabadilika.

"Wakipata mafunzo kama haya watafahamu namna ya utengenezaji, uandaaji na ukaushaji wa dawa pamoja na sheria yake na hatimaye tukafikia malengo ya kuanzisha hata na viwanda hivyo ambavyo serikali inahimiza kwa wananchi wake," alisema.

Aliitaka serikali kuendelea kuchukua hatua kali kwa waganga wa dawa asili ambao bado wanaotumia taaluma yao kufanya utapeli kwa kuhitaji viungo vya binadamu.

Naye Katibu wa UWAWATA anayewakilisha mikoa ya Kilimanjaro, Tanga, Manyara na Arusha, Ally Maganyari aliwataka wananchi kupuuza matangazo ya waganga wa kienyeji yanayobandikwa ovyo kwenye miti.

Awali, Mwalimu wa waganga hao, Dk. Jacob Chembele, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuongeza ujuzi na uelewa namna bora ya kutoa huduma ya tiba kwa wateja wao. Aliiomba serikali kuandaa mpango mkakati wa kuelimishaji tiba asili ili watu wajiepushe na matapeli wanaotumia nembo ya uganga kujipatia fedha na mali kwa njia ya udanganyifu.



# ZEC yaandaa rasimu elimu wapigakura

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

TUME ya Uchaguzi ya Zanzibar (ZEC) imeandaa rasimu ya mtaala wa elimu ya wapigakura ambao utatumika kwa taasisi zinazotakutoa elimu ya wapigakura baada ya kupewa kibali na tume cha kutoa elimu.

Kamishna wa ZEC, Jokha Khamis Makame, alieleza hayo katika ofisi za tume hiyo wakati akifungua mkutano wa kujadili rasimu ya mtaala wa elimu ya wapigakura.

Alisema matayarisho ya mtaala huo yanatokana na maelekezo ya kifungu cha 106(1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar Namba 4 ya mwaka 2018 yanayoitaka Tume kutayarisha mtaala wa elimu ya wapigakura utakaotumiwa na wadau wa uchaguzi wanaotaka kutoa elimu ya wapigakura. Naye mshauri elekezi, Juma Haji Ussi, alisema tume kwa upande wake inatarajia utekelezaji wa mtaala huo wa elimu utawasaidia wadau wa uchaguzi wakiwamo washirika wa maendeleo, waangalizi wa uchaguzi, vyama vya siasa na asasi za kiraia, na kwamba lengo la mtaala huo ni kuwajengea uelewa na kuangalia kwa kiasi gani elimu hiyo itawafikia walengwa.

Juma alisema mtaala huo umeainisha misingi ya utoaji wa elimu ya wapigakura pamoja na Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ambayo imetoa mamlaka ya kuratibu, kusimamia, na kuendesha elimu ya wapigakura kwa mujibu wa Sheria ya Uchaguzi ya Zanzibar ya Namba. 4 ya mwaka 2018.

Alieleza kuwa utayarishaji wa mtaala huo pia ulifanyika kwa kuzingatia vigezo vya kisheria na ushirikishwaji wa makundi ya kijamii ili umsaidie Mzanzibari kupata elimu bora inayohusu demokrasia katika masuala ya uchaguzi.

Kwa upande wao, washiriki wa mkutano huo walioipongeza Tume kwa kuandaa mtaala ambao umekidhi vigezo na kuzingatia umuhimu wa makundi mbalimbali katika masuala ya uchaguzi



Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, akifanyiwa uhakiki kwenye Daftari la Kudumu la Wapigakura, alipofika kwenye kituo chake cha kupiga kura katika Shule ya Sekondari ya Kitope Mkoa wa Kaskazini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMANI**

# Askofu ataja sifa za viongozi 2020

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

ASKOFU wa Kanisa la Anglikana Dayosisi ya Kondoa, Given Gaula, amewataka Watanzania kujitayarisha na uchaguzi mkuu kwa kuchagua viongozi wenye nia na kuweka mbele maslahi ya taifa, amani na uzalendo.

Askofu Gaula alisema hayo alipozungumza na waandishi wa habari Mjini Zanzibar wakati akielezea kuhusu mkutano utakaowakutanisha zaidi ya wajumbe 50 kutoka nchi 10 ikiwamo za Ulaya pamoja na maaskofu nane unaofanyika Zanzibar.

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi chache katika Bara la Afrika ambayo wananchi wake wanaendelea kuishi kwa amani na utulivu katika mazingira tofauti ya waumini wa dini zao.

Alisema utulivu huo unatakiwa kuenziwa ambapo wananchi wanatakiwa kushiriki katika uchaguzi mkuu kwa kuchaguwa viongozi wenye kuzingatia uzalendo wa kupenda nchi.

"Uzalendo na amani ni vipaumbele ambavyo vinatakiwa kuzingatiwa kwa kiongozi yoyote atakayeongoza Jamhuri ya Muungano wa Tanzania," alisema.

Alieleza kuwa watu wengi wanashangazwa jinsi wananchi wa Zanzibar wanavyoishi ambapo Waislamu wamekuwa wakioana na Wakristo bila ya kubaguana.

"Sifa moja kubwa ya Wazanzibari ni kujenga uvumilivu wa kidini...watu wanawashangaa kuona Waislamu wanawaoa Wakristo bila ya kuwapo ubaguzi," alisema.

Alisema lengo la mkutano huo ni kubadilisha mawazo juu ya uchumi wa kanisa unavyofanya kazi.

"Makanisa yanapita katika kipindi cha mabadiliko makubwa ikiwamo ya kiuchumi, kwa hivyo tumekutana kubadilisha mawazo juu ya kuendesha taasisi hizo za kidini kwa mafanikio makubwa," alisema.

Naye Askofu wa Kanisa la Anglikana Zanzibar, Michael Hafidh, alisema ujumbe huo ni faraja kubwa kwa Zanzibar katika kujitangaza katika sekta mbalimbali ikiwamo utalii. Aidha, alisema Zanzibar ni miongoni mwa nchi ambazo wananchi wake wanasifika kwa kujenga mshikamano wa kidini na kuvumiliana kwa lengo la kujenga mshikamano.

"Wazanzibari tunatakiwa kuendelea kujenga tabia ya uvumilivu wa imani ya dini tofauti bila kuhitilafiana," alisema.

Maaskofu hao jana walishiriki misa iliyoendeshwa na Mkuu wa Kanisa hilo nchini.

## Tahadhari yatakiwa dhidi chakula, dawa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Wakala wa Chakula Dawa na Vipodozi Zanzibar, Dk. Khamis Ali Omar, amewataka wananchi kuwa na tahadhari na matumizi ya chakula na dawa ambazo zimemaliza muda pamoja vipodozi ambavyo havijathibitishwa ili kuepuka maradhi yatokanayo na sumu.

Aliyasema hayo katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mjini alipokuwa akitoa mafunzo ya usalama wa chakula, dawa na vipodozi kwa masheha wa wilaya hiyo, na kuwataka kuwa na ushirikiano kuhakikisha wanadhibiti matumizi hayo kwa wananchi.

Alisema madhara yatokanayo na matumizi ya chakula, dawa na vipodozi ambavyo haviko katika kiwango kuhatarisha afya ya mtumiaji pamoja na kupata madhara makubwa ikiwamo saratani ya ngozi.

Aidha, aliwataka masheha kutoa ushirikiano kwa maofisa hao kwa kufuatilia uingizwaji wa bidhaa za chakula, dawa na vipodozi katika shehia zao, bidhaa ambazo hazijafanyiwa uchunguzi zinazozalishwa ndani ya nchi na nje ya nchi.

Naye Mkuu wa Ukaguzi Idara ya Uthibiti Usalama wa Chakula, Mohamed Shadhil Shomar, alisema wanafanya ukaguzi wa usalama wa bidhaa katika majengo tofauti yakiwamo maghala ya chakula na vipodozi, maduka, bekari, bucha, migahawa, hoteli, supermarket, viwanda na kufanya ukaguzi katika vituo vya forodha, bandari na viwanja vya ndege.

Alieleza kuwa Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar inafanya usajili wa majengo yote yanayotoa huduma za bidhaa kwa jamii ili kuyadhibitisha majengo hayo kwa kuzuia uzalishaji, usambazaji na uzaji wa bidhaa za chakula dawa na vipodozi ambavyo havijasajiliwa na ZFDA.

Mkuu wa Ukaguzi Kitengo cha Vipodozi Zanzibar, Salum Hamad Kassim, aliwataka wananchi waachane na matumizi ya vipodozi haramu.

Masheha wa Wilaya ya Mjini walisema watu sio waaminifu na kuwa wanatumia njia isio sahihi kwa kuuza bidhaa zao kwa bei rahisi na kujipatia kipato, bidhaa ambazo zinakaribia kumaliza muda au zimeshamaliza muda wa matumizi.

# Kampeni ya TRA yagusa wafanyabiashara Iringa

**Na Mwandishi Wetu**

WAFANYABIASHARA Mkoa wa Iringa wameifurahia kampeni ya elimu kwa mlipakodi inayoendelea kufanyika mkoani hapa na kuiomba Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kufanya kampeni hiyo mara kwa mara, ili waweze kuelewa kwa undani zaidi masuala mbalimbali yanayohusu kodi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa kampeni hiyo, wafanyabiashara hao walisema wamefurahishwa na kitendo cha TRA kuwafikishia elimu ya kodi sehemu wanazofanyia biashara kwani imekuwa rahisi kwao kueleza changamoto zao na kuelimishwa masuala ya kodi ambayo wengine hawakuwa na uelewa nayo.

Mmoja wa wafanyabiashara wa vipodozi mkoani humo, Vitusi Muhungile, alisema: "Binafsi nimefurahi kutembelewa na TRA kazini kwangu hapa na kutokana na elimu niliyopewa na maofisa wa TRA, nimetambua kwamba kuna mambo niliyokuwa nayafanya kwa kutokuwa na elimu, mfano mzuri ni utunzaji wa kumbukumbu za biashara yangu, leo nimejifunza umuhimu wake na ninaanza kufanya hivyo mara moja".

Mfanyabiashara wa duka la vifaa vya ujenzi wa Manispaa ya Iringa, Samson Ngakonda, alisema elimu ya kodi ina umuhimu kwani baadhi ya wafanyabiashara elimu yao ni ndogo, hivyo kutembelewa ni msaada mkubwa kwao.

"Elimu tuliyopewa leo ina umuhimu mno maana unaweza kukosea na ukipata elimu ukabadilika hivyo ninaomba elimu hii ifanyike mara kwa mara ili hata sisi ambao hatukwenda shule tuweze kujua vizuri haya mambo ya kodi," alisema Ngakonda.

Mfanyabiashara wa mbao katika Wilaya ya Mufindi, Dina Mwampendwa, alisema kutokana na elimu ya umuhimu wa kutumia Mashine ya Kielektroniki ya Kutolea Risiti (EFD) aliyopata kwenye kampeni ya elimu kwa mlipakodi ataanza kutumia mashine hiyo.

"Leo nimejisikia vizuri kutembelewa na maofisa wa TRA kwenye biashara yangu, mwanzoni nilivyoona gari niliogopa lakini baadaye nikaona wamekuja kirafiki na wameniemisha mambo mengi na hasa umuhimu wa kutumia mashine ya EFD na kuanzia leo naanza kuwatafuta mawakala ili ninunue mashine," alisema Mwampendwa.

Kampeni ya elimu kwa mlipakodi inaendelea kufanyika mkoani Iringa na kwa sasa timu ya maofisa wa TRA wanaofanya kampeni hiyo wako wilayani Mufindi baada ya kutoka Wilaya ya Kilolo na Manispaa ya Iringa.




Naibu Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile (wa pili kulia), akipata maelezo kutoka kwa Meneja Uhusiano wa Benki ya Biashara ya NBC, William Kalaghe (kulia), wakati wa maadhimisho ya miaka 55 ya Chama cha Madaktari Tanzania (MAT), yaliohudhuriwa na Rais John Magufuli, yaliofanyika mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam. Kushoto ni Ofisa Masoko wa Tawi la Benki ya NBC la Samora, Dustane Lipawaga na Meneja Huduma za Jamii, Irene Peter. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mafanikio katazo mifuko plastiki yaanikwa

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), limesema mafanikio yaliyopatikana tangu serikali itoe tamko la kusitisha matumizi ya mifuko ya plastiki Juni mwaka jana, yametokana na ushirikiano kutoka kwa wananchi na wazalishaji kwa ujumla wake.

Akizungumza baada ya kikao cha wadau wa uzalishaji, uingizaji, usambazaji na uuzaji wa mifuko mbadala ya plastiki mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam,

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alisema licha ya kuwapo kwa changamoto mbalimbali lakini utekelezaji wake umekuwa wa mafanikio makubwa.

"Takribani ni miezi saba sasa tangu kuwapo kwa katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki, Ofisi ya Makamu wa Rais iliunda Kikosi Kazi na NEMC tukawa waratibu wa utekelezaji wa katazo, tunashukuru kusema kwamba tumeifanya kazi hiyo kwa ufanisi mkubwa na sasa matokeo yake yanapongezwa na kila mpenda maendeleo na mazingira," alisema Dk. Gwamaka.

Alisema haikuwa kazi rahisi kufanikisha utekelezaji wa katazo hilo kwani liligusa maslahi ya watu wachache, lakini wenye nguvu ya kiuchumi, hivyo palihitajika ubunifu na weledi wa hali ya juu kudhibiti.

"Zoezi lilikuwa gumu katika kuratibu utekelezaji wake hivyo tulianza kwa kubaini viwanda vyote vya mifuko ya plastiki, wauzaji na wasambazaji, uandaaji wa miundombinu ya kuteketeza mifuko pamoja na kutoa elimu juu ya athari ya matumizi ya mifuko hiyo," alisema Dk. Gwamaka.

Aidha, alieleza mafanikio yaliyopatikana baada ya katazo hilo kuwa ni ongezeko la viwanda vya kutengeneza mifuko mbadala, ajira na ufahamu mpana kwa jamii juu ya utunzaji wa mazingira.

"Mpaka sasa kuna viwanda zaidi ya 70 ambavyo vinazalisha mifuko mbadala vimeanzishwa na kutengeneza ajira 2,761 nchi nzima hali ambayo inaimarisha uchumi kwa Taifa," alisema, na kuongeza kuwa nafasi bado ipo kwa wawekezaji kufanya uwekezaji katika viwanda hivyo kwa kuwa mahitaji bado ni makubwa.

Alizishukuru mamlaka na taasisi zote zilizohusika katika kusaidia kufanikisha katazo hilo lililotolewa na Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, Aprili 10, 2019 na utekelezaji wake kuanza Juni Mosi, 2019.

"Nitumie nafasi hii kuzishukuru mamlaka zote za serikali za mitaa nchini pamoja na taasisi mbalimbali zilizoshikirikiana pamoja na NEMC hususan Shirika la Viwango nchini na wadau wote wa mazingira kwa kufanikisha utekelezaji wa katazo hali ambalo imefanya mazingira yetu yawe na mwonekano mzuri," alisema.

# RC Nchimbi ahimiza viwango kwa bidhaa

**Na Felix Andrew**

WAZALISHAJI wa bidhaa mbalimbali mkoani Singida, wametakiwa kutambua kuwa suala la viwango ni la kisheria hivyo ni lazima kuthibitisha ubora wa bidhaa ili kumlinda mlaji na kupata uhakika wa soko la bidhaa wanazozizalisha.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dk. Rehema Nchimbi, alipokuwa akifungua mafunzo ya wazalishaji wa bidhaa za vyakula yakiwamo mafuta ya alizeti na wauzaji wa vipodozi na vyakula yaliyofanyika katika ukumbi wa VETA mkoani humo.

Dk. Nchimbi alisema suala la ubora wa bidhaa linapaswa kuzingatiwa katika mnyororo wote wa uzalishaji ili mlaji awe salama na kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza kutokana na kutozingatia viwango.

"Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ndiyo hakikisho la wazalishaji na fursa zinazotengenezwa zitakuwa dhahiri iwapo masuala ya viwango yatazingatiwa, vilevile TBS ni daraja kati ya mzalishaji na soko, hivyo mzalishaji ni lazima kufuata utaratibu," alisisitiza Dk. Nchimbi.

Alisema maisha ya binadamu ni chakula, hivyo ni muhimu kuzingatia usalama wake, kwani bidhaa hafifu zinagharimu afya ya walaji, na kwamba magonjwa mengi yanatokana na jinsi ya uandaaji wa chakula na jinsi ya ulaji, hivyo wazalishaji wanapaswa kuwa waaminifu katika kuzalisha bidhaa yoyote.

Dk. Nchimbi alisema TBS siyo adui ya wazalishaji hawapaswi kuichukia na wajenge dhana kuwa TBS ni salama, hivyo wazalishaji wa Singida wahakikishe kuwa wanazalisha bidhaa bora wakati wote ilikudhidhirisha kauli kwamba Singida ni njema wakati wote.

Akizungumzia kwa upande wa TBS, Dk. Nchimbi alisema shirika linapaswa kuangalia namna ya kuongea na wajasiriamali ili kuhakikisha kuwa yale wanayo wafundisha wanaelewa kikamilifu.

"Mafunzo haya yawe na kipimo ili kujua kama yameeleweka vizuri na kwamba watakaopokea mafunzo ndiyo watakaowapima," alisema.

Meneja wa Mafunzo na Utafiti kutoka TBS, Hamisi Sudi, alisema shirika litaendelea kutoa mafunzo kwa wajasiriamali ili kuhakikisha kuwa wanazalisha bidhaa kwa kuzingatia viwango.

Alisema shirika linatambua kuwa wajasiriamali wanamchango mkubwa katika kukuza pato la taifa na kutengeneza ajira kwa wananchi walio wengi hivyo shirika linamchakato endelevu wa kutoa elimu kwa jamii hasa wajasiriamali ili kuwa ni mojawapo ya majukumu yake ya kila siku.

Shirika likiwa mkoani Singida limetoa mafunzo kwa wajasiriamali 221katika wilaya za Iramba, Singida na Manyoni, ambayo pia yamewashirikisha watendajiwa Halmashauri wakiwemo maafisa Biashara, Maendeleo ya Jamii na Afya

HABARI KIMATAIFA

# Ujerumani yajiandaa kwa mashambulizi ya kisasi

**BERLIN,** Ujeruman

VIKOSI vya usalama nchini Ujerumani vinajiandaa kwa uwezekano wa kutokea mashambulizi ya kulipiza kisasi kufuatia tukio la wiki hii la ufyatuaji risasi katika mji wa magharibi mwa Ujerumani Hanau.

Hatua hiyo inatokana na tukio lililotokea mwishoni mwa wiki wakati raia wa Ujerumani mwenye umri wa miaka 43 aliwapiga risasi na kuwaua watu tisa mjini Hanau, karibu na Frankfurt.

Watu wote waliofariki walikuwa na asili ya uhamiaji. Muuaji huyo kisha alipatikana akiwa amekufa nyumbani kwake, pamoja na mama yake aliyekuwa na umri wa miaka 72.

Shirika la habari la 'The Funke' limewataja wapelelezi wa ugaidi wakisema kuwa kuna uwezekano wa kutokea mashambulizi ya kulipiza kisasi kutoka kwa watu wa siasa kali za mrengo wa kushoto, pamoja na mashambulizi dhidi ya wawakilishi wa chama cha siasa kali za mrengo wa kulia cha'Alternative for Germany – AfD'.

Taarifa zinaeleza kuwa ijapokuwa hakuna kitisho maalumu cha mashambulizi ya kulipiza kisasi kutoka kwa watu wa itikadi kali, uwezekano huo hauwezi kufutiliwa mbali.

Wakati huo huo, vyama viwili vya kisiasa Ujerumani vimependekeza uwezakano wa kufanywa vipimo vya lazima vya kisaikolojia kwa wamiliki wa silaha na wanaotuma maombi ya kutaka kumiliki.

Mtaalamu wa masuala ya ndani wa Chama cha Social Democratic – SPD, Helge Lindh, alisema: "baada ya shambulizi la Hanau, tunapaswa kutathmini vikali kama tunahitaji kuirekebisha sheria ya umiliki wa silaha."

Katika toleo la gazeti la 'Bild' kiongozi wa chama cha Christian Social Union – CSU, Horst Seehorfer, alidai kufanyika vipimo zaidi vya kisaikolojia katika njia ya ripoti ya matibabu au uthibitisho wa wamiliki wa leseni za silaha.

Seehofer alisema kuwa Ujerumani tayari imeimarisha juhudi za kupambana na siasa kali za mrengo wa kulia. Alisema rasilimali nyingi zimetolewa kupambana na makundi ya wanazi-mamboleo, ikiwa ni pamoja na kuwaajiri mamia ya wapelelezi wapya wa serikali na maofisa wa ujasusi wa ndani ya nchi. **DW**

# Corona yashika kasi Korea, watu 556 waambukizwa

**SEOUL,** Korea Kusini

KOREA Kusini imeripoti ongezeko la maambukizi mapya ya virusi vya corona 123 na kufanya walioambukizwa kufikia 556, wakati Italia na Iran zikichukua hatua zaidi za kukabiliana na mlipuko huo.

Idadi ya vifo nchini Korea Kusini nayo imeongezeka hadi kufikia watu wanne. Ijumaa Italia ilikuwa nchi ya kwanza barani ulaya kuripoti kuwa raia wake mmoja amefariki kutokana na corona na kufuatiwa na kifo kingine juzi Jumamosi.

**Idadi ya vifo nchini Korea Kusini nayo imeongezeka hadi kufikia watu wanne.**

Zaidi ya raia 50,000 katika miji kadhaa ya Kaskazini mwa Italia wameamuriwa kusalia nyumbani wakati maduka na shule vikifungwa.

Iran nayo imezifunga shule, vyuo na vituo vya utamaduni katika majimbo 14 jana kufuatia vifo vya watu watano.

Ingawa Misri ndio taifa pekee Afrika ambalo limethibitisha kisa cha COVID-19, lakini Shirika la Afya Duniani (WHO) limeonya kuwa mifumo ya afya Afrika sio imara kuweza kukabiliana na milipuko mikubwa na kuomba ushirikiano zaidi ndani ya Umoja wa Afrika (EU). **DW**



Rais wa Sudan Kusini, Slava Kiir (kushoto), akiwa ameshikana mkono na kiongozi wa upinzani nchini humo, Riek Machar baada ya kuunda serikali ya muungano. **PICHA: REUTERS**

# Sudan Kusini yaunda serikali ya muungano

**JUBA,** Sudan

SUDAN Kusini imefungua ukurasa mpya baada ya viongozi hasimu kuunda serikali ya mseto ambayo wengi wanatumai itadumu.

Siku moja baada ya Rais Slava Kiir kuivunja serikali iliyokuwapo, kiongozi wa upinzani, Riek Machar alijitangaza kuwa makamu wa rais, muundo ambao ulishindwa kufanya kazi mara mbili na kuitumbukiza nchi hiyo kwenye mzozo wa vita uliowaua karibu watu 400,000.

Sudan Kusini, ilitumbukia kwenye vita vya wenyewe kwa wenyewe mwaka 2013 baada ya wafuasi wa Rais Kiir na Machar kuingia kwenye makabiliano makali miaka miwili tangu iliposhinda harakati za kudai uhuru kutoka Sudan.

Msukumo kutoka jumuiya ya kimataifa uliwezesha kupatikana kwa makubaliano ya amani ya mwaka 2018.

Sherehe za kuundwa serikali mpya mjini Juba zilianza kwa viongozi hao kukabidhiwa picha ya tukio hilo ile iwe iwakumbushe wajibu walio nao.

Wasiwasi kutoka Marekani, ambayo ni mchangiaji mkubwa wa misaada kwa Sudan Kusini uliongezeka wakati Rais Kiir na Machar waliposogeza mbele mara mbili muda wa mwisho uliowekwa kuunda serikali mwaka jana.

Hata hivyo, chini ya wiki moja kabla ya muda wa mwishoni uliowekwa, mahasimu hao wawili walifikia makubaliano kwa kila upande kuwa tayari kulegeza misimamo kadhaa.

Rais Kiir alitangaza uamuzi mgumu kuhusu suala tete la idadi ya majimbo na Machar aliridhia Rais Kiir kushughulikia suala la ulinzi wake.

Alhamisi wawili hao walitangaza kufikia makubaliano ya kuunda serikali itakayoongoza kwa miaka mitatu kabla ya kufanyika uchaguzi mkuu utakaokuwa wa kwanza tangu taifa hilo lilipopata uhuru. **DW**

## Aliyeimba kusifia wanawake atafutwa

**RIYADH,** Saud Arabia

WAKUU wa Saudia wameagiza kukamatwa kwa mwimbaji wa kike wa muziki wa 'rap', Asayel Slay ambaye ametoa video ya muziki kwa jina Mecca ambayo ina wasifu wanawake.

Mwimbaji huo aliiomba kwa kueleza kuwa wanawake katika mji huo mtakatifu ni wenye nguvu na wazuri. Watumiaji wa mitandao ya kijamii walionyesha hasira yao na kusema kwamba mamlaka ina unafiki. Mwaka 2018, mwanamfalme mwenye msimamo mkali alianzisha pogramu ya kuendeleza mabadiliko.

Lakini wanaharakati wamesema matukio ya ukandamizaji yameongezeka na kumekuwa na msako wa kutishia uhuru wa kujieleza. Video hiyo ilitolewa kupitia mtandao wa YouTube wiki iliyopita na mwanamuziki huyo kijana. Muziki wa mwanadada huyo aina ya rap, unazungumzia wanawake wa mji wa Mecca, eneo takatifu kwa waumini wa Kiislamu ambao huenda mji huo kuhiji kila mwaka.

"Heshima yetu kwa wasichana wengine lakini wasichana wa Mecca ni wazuri sana," Ni moja ya mashairi yaliyomo katika video ya wimbo huo huku wanaume na wanawake wakicheza katika mgahawa.

Video hiyo ilisambaa sana katika mitandao ya kijamii na watu wakitumia hashtag #Mecca_Girl_Represents_Me kuisifu. **BBC**

# Mkapa afurahia ubinafsishaji Benki NMB

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS mstaafu wa Serikali ya Awamu ya Tatu, Benjamin Mkapa, amesifu uamuzi wa serikali yake wa kuamua kuibinafsisha Benki ya NMB.

Akizungumza jijini Mwanza juzi wakati wa hafla ya kutambulisha kitabu chake cha: My Life, My Purpose - A Tanzanian President Remembers (Maisha Yangu, Dhamira Yangu: Rais wa Tanzania Akumbuka), Rais huyo mstaafu alisema suala la ubinafsishaji taasisi hiyo ulitokana na uamuzi wa mwanzoni mwa utawala wake, baada ya kuingia madarakani mwaka 1995.

Ilipofika mwaka 1997, Serikali ya Rais Mkapa iliamua kuundwa kwa Benki ya NMB baada ya kugawanywa kwa iliyokuwa Benki ya Taifa ya Biashara (NBC).

Baada ya kuundwa kwa NMB mwaka 1997, mwaka 2005 serikali ya Rais Mkapa iliuza asilimia 49 ya hisa za NMB kwa wawekezaji wa Rabobank ya Uholanzi.

"Nafarijika kuona NMB ni miongoni mwa benki kubwa zenye mtandao mkubwa nchini ikihudumia wananchi wa kawaida hadi vijijini," alisema Mkapa.

Akionyesha kuchukizwa na wanaokosoa uamuzi wa ubinafsishaji uliochukuliwa na serikali yake, Rais Mkapa alisema watu wanataakiwa kuelewa kuwa wakati huo ilikuwa ni lazima kufanya uamuzi ili kuokoa pesa za walipakodi zilizokuwa zikipotea kwa kutolewa kama ruzuku ya kuendeshea mashirika ya umma.

Ndani ya kitabu chake, kuna aya inayosema wanaokosoa uamuzi wa ubinafsishaji wanapaswa kuelewa kuwa wakati huo, mashirika ya umma yalikuwa na hali mbaya kifedha kiasi kwamba serikali ililazimika kutumia kiasi kikubwa cha pesa za walipakodi kugharamia uendeshaji wa mashirika hayo. "...hiyo siyo kazi moja wapo ya pesa za serikali," anaandika Mkapa.

Akizungumzia mafanikio ya benki hiyo, Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema kwa kipindi cha miaka 22 iliyopita, benki hiyo imejipambanua kuwa mfano bora wa uamuzi wa ubinafsishaji baada ya kufikia kuwa kimbilio la wafanyabiashara wadogo, kati na wakubwa kwa mitaji na ushauri wa kitaalamu.

Kwa miaka 22 ya uwepo wake, Benki ya NMB imetoa jumla ya Sh. trilioni 1.2 kusaidia biashara ndogo na za kati na mikopo mingine Sh. trilioni 2.2 kusaidia wateja binafsi.

Katika kusaidia wakulima, Zaipuna alisema mwaka huu wa 2020, benki imepanga kufungua akaunti zaidi ya 300,000 za wakulima ili kuhakikisha kuwa wakulima wanapata malipo yao kupitia mfumo rasmi wa fedha na hivyo kuchangia katika kukuza huduma jumuishi za fedha nchini.

Zaipuna alisema Benki ya NMB imeendeleza ushirikiano wake na Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali (government's electronic payment system - GePG), ambapo mpaka hivi sasa taasisi 590 za serikali zimeunganishwa katika mfumo huo. Kupitia mfumo wa GePG, Benki ya NMB huwezesha kukusanya kwa jumla ya mapato ya serikali yapatayo shilingi trilioni 2.1.

"Tunafanya hivyo kwa kutambua kuwa ni wajibu wetu kuunga mkono miradi ya kimkakati ya serikali. NMB ndiyo iliyokuwa benki ya kwanza kuunganishwa na mfumo wa GePG," alisema.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki (kulia), akijadiliana jambo na mwekezaji na Mwenyekiti wa Kampuni ya Supreme Holding kutoka Misri, Dk. Moharram Helal (kushoto), baada ya kufanya mazungumzo kuhusu ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza mitungi ya gesi Mkuranga, mkoani Pwani mwishoni mwa wiki, (katikati) ni Meneja Mkuu wa Kampuni ya Intergas, Dk. Hatem Ahmed. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Kiwanda cha kuchakata nyama Soga kuanza Agosti

**Na Mwandishi Wetu**

KIWANDA cha kisasa cha kuchakata nyama cha Tan Choice Tanzania kilichopo Soga, Wilaya ya Kibaha, Mkoa wa Pwani, kinatarajia kuanza uzalishaji mwezi Agosti, mwaka huu.

Mradi huo ni uwekezaji wa zaidi ya Sh. bilioni 30 ukiwa kati ya miradi ya viwanda vilivyoanzishwa katika maeneo maalum ya uwekezaji baada ya kupata leseni kutoka Mamlaka ya Ukanda Maalumu wa Uwekezaji (EPZA).

Mratibu wa kiwanda hicho, Dk. Bonaventure Mtei, alimweleza Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Prof. Riziki Shemdoe, aliyekuwa ziarani kwenye kiwanda hicho mwishoni mwa wiki kuwa mradi wa kuchakata nyama upo katika hatua za mwisho kuanza uzalishaji mwezi Agosti.

Prof. Shemdoe alisema, mradi huo ni mkubwa kwenye sekta ya mifugo ambao utakuwa na matokeo chanya katika uchumi wa nchi.

"Serikali ipo makini kuwaunga mkono wawekezaji wote hasa hawa wanaotekeleza uwekezaji huu mkubwa ambao utakuwa na mchango mkubwa katika ujenzi wa uchumi wa viwanda," alisema.

Kiwanda hicho chenye kutumia teknolojia ya kisasa, kitakuwa na uwezo wa kuchakata ng'ombe 1,000 na mbuzi na kondoo 4,500 kwa siku. Pia utaajiri zaidi ya watu 500 ajira za moja kwa moja na kutengeneza nyingine nyingi zisizo za moja kwa moja.

"Nawapongeza Tan Choice kwa uwekezaji huu mkubwa ambao unaunga mkono juhudi za Raisi John Magufuli wa kujenga uchumi wa viwanda. Pia mradi huu utaifanya sekta ya mifugo kuwa ya kibiashara zaidi," alisema Prof. Shemdoe.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya EPZA, Kanali mstaafu Joseph Simbakalia, alisema mradi wa kuchakata nyama utawahakikishia wakulima wadogo soko la uhakika la mifugo yao na kuongeza kipato.

Alisema uwepo wa mradi huo katika eneo la Soga utawavuta watu wengi karibu ambao watauza huduma mbalimbali kwa wafanyakazi katika kiwanda hivyo kuchangia katika kukuza miji mipya katika eneo hilli.

Naye mratibu wa kiwanda Dk. Mtei alipongeza serikali kutokana na ukaribu wake na juhudi mbalimbali za kushughulikia changamoto ambazo zinakabili mradi wa uchakataji nyama katika eneo la Soga.

## NBC yazindua klabu kukutanisha w'biashara

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC), imezindua klabu ya biashara katika Mkoa wa Tanga yenye lengo la kuwakutanisha wafanyabiashara wadogo na wa kati ili kupeana fursa, mbinu na kujadiliana mambo mbalimbali yanayohusu biashara zao.

Benki hiyo pia imeendesha mafunzo ya kibiashara kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati kuwaongezea uwezo, uelewa na ubunifu katika kufanya biashara zao.

Akizungumza katika hafla ya uzinduzi wa klabu hiyo, Mkurugenzi wa Kitengo cha Biashara NBC, Elvis Ndunguru, alisema benki hiyo imedhamiria kurahisisha huduma za kibenki kwa makundi mbalimbali hususani wafanyabiashara ambao ni muhimu kwa ukuaji wa uchumi nchini.

Alisema kuzinduliwa kwa klabu hiyo ya biashara kunafanya klabu za biashara kuwa tisa nchini huku malengo yake yakiwa ni kuwaunganisha na kuwakutanisha pamoja ili kutafuta fursa za ufanyaji wa biashara na kubadilishana uzoefu.

Ndunguru alisema benki hiyo imeamua kuanzisha vilabu hivyo vya wafanyabiashara (NBC B Clubs) ili kukuza na kuimarisha biashara nchini.

"NMB B Club ni mahali mwafaka pa kuelimisha wafanyabiashara kuhusu ya masuala mbalimbali ya biashara na tangu kuanzishwa kwa klabu hizi, wanachama wananufaika na mafunzo mbalimbali ikiwamo jinsi ya kutumia vitabu vya mahesabu, elimu ya masoko na pia elimu ya mlipakodi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato nchini (TRA)," alisema.

Mkurugenzi wa Jiji la Tanga, Daudi Maheji, ambaye alikuwa mgeni rasmi kwenye hafla ya uzinduzi wa klabu hiyo, alipongeza NBC kwa kuamua kufungua klabu na kutoa elimu ya mlipakodi, utunzaji wa kumbukumbu na jinsi ya kuweka mahesabu sawa.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

**YUMBA INAUZWA MIL 70 ARUSHA GULELO:,** SELF VYUMBA 3 KIMOJA IASTER, SITTING, JIKO NA STORE, INA MEME ãNA MAJI INAFAA KUISHI, INISHING NA FENSI UNAIMALIZIA. IWENYE NYUMBA **0757 804 970**


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

imu: +255 26 2324455
ax: +255 26 2323233
arua Pepe: ps@mow.go.tz
ovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

Tarehe 22/02/2019

### TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATATU tarehe 24/2/2020** kampuni ya **FAMARI INVESTMENT** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **TUNDUMA** kuelekea **DAR ES SALAAM,** gari hilo lenye namba za usajili: **T 174 DQJ/ T 591 DMG**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Urefu | - mita | 4.6 Mts |
| Upana | - mita | 2.9 Mts |
| Kimo | - mita | 21 Mts |

3. **Njia itakayotumika: TUNDUMA hadi DAR ES SALAAM kupitia MAKAMBAKO**

Gari litasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

### KUPOTEA KWA CHETI



115643102

**Elihudi Petro** Mbwambo anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0916-0030** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2001 katika shule ya Sekondari Chalao na Cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P0798/590** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2006 katika kituo cha Korogwe Teacher College Centre. Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **PWA/MLA/RB/164139/2020**

### KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA/PASSPORT



215643002

**VICENT PARADISE MASSAM** anatangaza kupotea kwa Passport /Hati ya Kusafiria yenye namba **TAE027976** iliyotolewa na Uhamiaji Office za Dar es Salaam mwaka 2018. Yeyote atakaeion atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/CEN/RB/78592/2020**

### TANGAZO

**Katika Mahakama ya Mwanzo…… Moshi Mjini…………………**
**Usimamizi wa Mirathi No, …..10………..2020**
**Ombi la ……….CYRUS OFORO…MAKUPA……**
**Usimamizi wa mirathi ya marehemu ……….IRMA ILLYES MAKUPA………………………**

Kwa …..Yeyote anaehusika

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa

Kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo ….16…/03/….2020………kabla ya huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa .

Tarehe ….20….02….2020…………………

156437

### TANGAZO

**Katika Mahakama ya Mwanzo…… Moshi Mjini……………**
**Usimamizi wa Mirathi No, …..17………..2020**
**Ombi la ……….Abdul Rajabu .Kimaro……………**
**Usimamizi wa mirathi ya marehemu ……….Rajabu Seleman Kimaro………………………**

Kwa …..Yeyote anaehusika

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa

Kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo ….12…/03/….2020………kabla ya huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa .

Tarehe ….19….02….2020…………………

SAHIHI YA HAKIMU

156436


***Kwa habari za kila siku usikose gazeti lako la nipashe leo.Tupigie 0782253676***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO



# MOURINHO AIONEA WIVU CHELSEA KWA GIROUD, ABRAHAM NA BATSHUAYI

**LONDON,** England

JOSE Mourinho aliona namna gani Tottenham Hotspur wanavyopata wakati mgumu kwa kuwakosa nyota wake, Harry Kane na Son Heung-min wakati Olivier Giroud alipoifungia Chelsea Jumamosi.

Giroud, ambaye amekuwa mshambuliaji chaguo la tatu pale Chelsea nyuma ya Tammy Abraham na Michy Batshuayi kwa msimu huu, alianza dhidi ya Spurs na alifunga bao la kwanza kwenye ushindi wa 2-1 pale kwenye dimba la Stamford Bridge.

Kikosi cha Mourinho kinawakosa Kane na Son ambao ni majeruhi na wanatarajia kukaa nje ya dimba kwa kipindi kirefu cha msimu huu.

Baada ya mchezo huo, Mourinho alirudia madai yake kwamba yupo kwenye wakati mgumu kwenye mbio za Ligi Kuu, kombe la FA na Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa sababu hana mbadala kwenye safu yake ya ushambuliaji.

"Ni ngumu sana," alisema akiwaambia waandishi wa habari. "Miezi mitatu ijayo itakuwa migumu mno kwetu.

"Kwa wiki tatu au nne, (Moussa) Sissoko amerudi, na yeye siyo mshambuliaji, lakini ni suluhisho kwetu. Nina matumaini Aprili, Sonny au Harry (Kane) watakuwa wanapona kama alivyofanya Hugo Lloris.

"Hugo alirudi kucheza wiki kadhaa zilizopita kabla ya muda ambao tulimtarajia. Hakuna aliyemtarajia kama angerudi mapema uwanjani."

# Conte hana shaka na Martinez anayewaniwa Barcelona

**MILAN,** Italia

KOCHA wa Inter Milan, Antonio Conte hafikirii kama Lautaro Martinez anaweza "kuvimba kichwa" baada ya kusifiwa na nyota wa Barcelona, Lionel Messi.


Martinez amekuwa akihusishwa na mpango wa kwenda pale Camp Nou kama mrithi wa muda mrefu wa Luis Suarez na wiki iliyopita alisifiwa na Messi.


Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ameripotiwa kwamba kwenye mkataba wake kuna kipengele cha kuachiwa kwa euro milioni 111 na pia ametajwa kuwaniwa na Manchester United, Manchester City na Real Madrid.

Licha ya kutakiwa huko kwa Martinez, Conte anajiamini kwamba mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina akili yake kwa sasa ipo kwa ajili ya kuisaidia Inter Milan.

"Kijana ana majukumu hapa," alisema Conte akiwaambia waandishi wa habari Jumamosi. "Anafanya vizuri na sisi na ataendelea hivyo hivyo.

"Ameimarika vya kutosha msimu uliopita na ndio kwanza ana umri wa miaka 22. Ana majukumu hapa na nina furaha kuwa nae hapa."





# *Tyson Fury bingwa wa ngumi wa Dunia*

**LAS VEGAS,** Marekani

BONDIA Tyson Fury amefanikiwa kumpiga mpinzani wake Deontay Wilder kwenye pambano lao la marudiano la masumbwi ya uzito wa juu lililofanyika usiku wa kuamkia jana Jumapili mjini La Vegas nchini Marekani.

Fury ambaye alitawala pambano hilo kwa muda wote, alimchapa mpinzani wake huyo kwa TKO katika raundi ya saba.

Fury, maarufu pia kwa jina la 'The Gypsy King' sasa amekuwa bingwa wa masumbwi ya uzito wa juu wa duniani kwa mkanda wa WBC, na kuweka rekodi ya kuwa bondia namba moja kwa sasa kwenye uzito huo asiye na rekodi ya kupigwa kwenye mapambano yake 30.

Hakuna aliyetarajia kuwa Fury angeweza kushinda pambano hilo kwa KO, wengi walitabiri kuwa Wilder angeshinda kwa KO au Fury angeshinda kwa alama baada ya kengele ya raundi ya 12.

Aidha, Fury ameweka rekodi ya aina yake kwa kuwa bondia wa kwanza kumwonjesha joto la kipigo cha TKO Wilder ambaye mapambano yake yote ameshinda kwa KO isipokuwa pambano lao la kwanza ambalo lilimalizika kwa sare.

Katika pambano hilo Fury alimtesa Wilder akimpasua sikio lake na kusababisha damu nyingi kutoka huku watu wakisubiri mwamuzi tu amalize pambano.

Tangu raundi ya kwanza Fury alianza kwa kasi na kumpa presha kubwa Wilder ambayo ilimshinda kuhimili.

HABARI MICHEZO

# Guardiola: Tutafunga penalti ijayo

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola anajiamini Manchester City watafunga penalti ijayo baada ya kukosa Jumamosi wakati wakiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Leicester City.

Sergio Aguero alikosa penalti dakika ya 62 baada ya Ilkay Gundogan kumnawisha mpira, Dennis Praet eneo la hatari na golikipa, Kasper Schmeichel aliiokoa.

City sasa imeshindwa kufunga penalti zake nne zilizopita kwenye Ligi Kuu ya England, huku Aguero akiungana na Gundogan, Gabriel Jesus na Raheem Sterling kwa kushindwa kufunga kutoka eneo hilo la umbali wa yadi 12.

Lakini Guardiola, ambaye awali alibainisha kwamba golikipa, Ederson anaweza kuchukua majukumu ya kupiga penalti, anaamini City watafunga penalti ijayo.

"Tumekosa penalti nne mfululizo kwa sasa, lakini pengine tutafunga tutakapohitaji kushinda kitu fulani," alisema Guardiola akiiambia BBC Sport.

"Nafasi ya golikipa ni nzuri, lakini penalti ijayo tutafunga!"

Licha ya Aguero kukosa penalti hiyo, City ilipata pointi zote tatu kwenye mchezo huo, shukrani kwa bao la Jesus aliyetokea benchi na kufunga zikiwa zimesalia dakika 10 mpira kumalizika.

Dakika tatu baada ya Jesus kuingia uwanjani aliitumia vizuri pasi ya nyota wa zamani wa Leicester, Riyad Mahrez na kufunga bao hilo.







# BRAITHWAITE: SITAFUA JEZI NILIYOKUMBATIWA NA MESSI

**BARCELONA,** Hispania

MARTIN Braithwaite alifurahia kupindi cha pili wakati akiichezea kwa mara ya kwanza Barcelona baada ya kusajiliwa wiki iliyopita - na alibainisha kwamba hatafua jezi yake baada ya kukumbatiwa na Lionel Messi.

Baada ya wiki ngumu ya klabu hiyo, Barca waliwafumua Eibar 5-0 kwenye mchezo uliopigwa dimba la Camp Nou, huku manne yakifungwa na Messi, baada ya kipindi cha kwanza kufunga 'hat-trick'.

Kabla ya mchezo huo, mashabiki wengi wa Barca walipeperusha skafu nyeupe dhidi ya rais, Josep Maria Bartomeu na kuimba wakimtaka ajiuzulu kwa madai yaliyotolewa mapema wiki iliyopita kwamba anawayumbisha wachezaji wa klabu hiyo wa sasa na wa baadaye, akiwamo Messi.

Braithwaite alisajiliwa kwa usajili unaotajwa kwamba ni wa utata kutoka Leganes baada ya kuruhusiwa na Shirikisho la Soka la Hispania kufanya hivyo kwa dharura, baada ya washambuliaji wake wa wawili, Ousmane Dembele na Luis Suarez kuumia na watakuwa nje kwa muda mrefu.

Lakini mchezaji huyo wa kimataifa wa Denmark alifurahia mwanzo wake huo baada ya kuhusika kwenye bao la nne la Messi na lile la tano la Arthur.

Wakati alipoulizwa nini alichoambiwa na Messi baada ya kumsaidia kufunga, Braithwaite aliwaambia waandishi wa habari: "Alinipongeza, ni mtu mzuri.

"Anifanya nijisikie vizuri, alikuwa akinipasia mipira. Sitafua jezi yangu niliyokumbatiana nae," alisema Braithwaite.

# *Ronaldo afikia rekodi ya Batistuta Serie A*

**TURIN,** Italia

CRISTIANO Ronaldo ameungana na Gabriel Batistuta na Fabio Quagliarella kwenye rekodi ya vitabu vya Ligi Kuu ya Italia, Serie A, baada ya kufunga kwenye mechi ya 11 mfululizo kwenye Ligi Kuu.

Ronaldo, akicheza mchezo wake wa 1,000 tangu aanze kucheza soka la kushindani, aliiweka Juventus mbele dakika ya 39 kwenye mchezo huo wa Jumamosi dhidi ya SPAL, akifunga kwa kuunganisha krosi ya Juan Cuadrado.

Bao hilo lilimfanya Ronaldo mwenye umri wa miaka 35 kumfikia gwiji wa zamani wa Fiorentina, Batistuta na nyota wa Sampdoria, Quagliarella, ambapo wote sasa wamefunga kwenye mechi 11 mfululizo za Serie A.

Wakati Batistuta aliweka rekodi hiyo msimu wa 1994-95, Quagliarella - ambaye ana umri wa miaka 35 alifanya hivyo msimu uliopita.

Hata hivyo, Ronaldo anaweza kuweka rekodi yake kama atafunga kwenye mchezo ujao na maana atakuwa amefunga kwenye mechi 12 mfululizo.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAZARD AIPA PIGO TENA REAL MADRID

## Hatarini kuikosa Man City Uefa, Barcelona kwenye Clasico...

**MADRID,** Hispania

UWEZEKANO wa Eden Hazard kuwapo kwenye mchezo wa Real Madrid dhidi ya Manchester City na Barcelona ni mdogo baada ya Zinedine Zidane kubainisha kwamba majeruhi yake ya hivi karibuni "siyo mazuri".

**Fowadi huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alionekana akichechemea kipindi cha pili wakati wakifungwa 1-0 na Levante Jumamosi na alionekana akitibiwa kwenye benchi chini ya mguu wake wa kulia.**

Hazard ndio kwanza alikuwa amerudi dimbani baada ya kuumia enka katika mguu wa kulia na sasa anaonekana kupata tatizo jingine ambalo linampigia kengele ya hatari Zidane.

Madrid itacheza na Man City ya Pep Guardiola kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora Jumatano, kabla ya kwenda kwenye mchezo wa Clasico dhidi ya vinara wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, Barcelona wikendi ijayo.

"Hali inaonekana sio nzuri," alisema Zidane akiwaambia waandishi wa habari. "Ni pigo kubwa kwetu, amepata majeruhi pale alipoumia, ngoja tuone itakavyokuwa.

"Kwa sasa inaumiza, lakini tutaona kesho (leo) vipimo vitakavyoonesha."

Ulikuwa wakati mbaya zaidi kwa Madrid kwenye mchezo huo baada ya kupokea kichapo hicho shukrani kwa bao la Jose Luis Morales dakika za majeruhi.

Madrid ilitoka sare ya kufungana 2-2 na Celta Vigo nyumbani kwenye mchezo wake uliopita na sasa watacheza na Barcelona Jumapili ijayo wakijua kwamba wamepitwa pointi mbili na vinara hao kwenye mbio za ubingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Nahodha Sergio Ramos alibainisha wapo kwenye mkanganyiko baada ya matokeo ya mchezo huo na aliandika kwenye kurasa zake za mitandao ya kijamii.

"Hali sio nzuri kwetu," aliandika Ramos kwenye ukurasa wake wa Twitter.

"Lakini hatuwezi kwenda vichwa vikiwa chini.

"Tunatakiwa kujipanga upya sasa na kesho na kuhakikisha tunajituma zaidi, kwani sasa kila wiki ni muhimu kwetu na tunaihesabu."

## ZISIKUPITE

### MAN UNITED WAMTAKA JOTA

KLABU ya Manchester United wameonesha nia ya kutaka kumsajili msimu ujao mshambuliaji wa Wolves na timu ya taifa ya Ureno, Diogo Jota mwenye umri wa miaka 23. ***(Calciomercato).***

### BERNARDO SILVA ATAKIWA

MIAMBA wa Ligi Kuu ya Hispania, Barcelona wanajipanga kimsajili kiungo wa kati wa Manchester City, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 25 wakati wa kipindi cha usajili cha majira ya joto. ***(Daily Express)***

### HODGSON KUONGEZA MKATABA

KOCHA wa Klabu ya Crystal Palace, Roy Hodgson yuko tayari kusaini mkataba wake mpya na timu hiyo, kwa sababu anaamini kwamba klabu inamaono mazuri hasa ya kipindi cha usajili.***(Sky Sports)***

### AGOMBEWA CHELSEA, BARCA

TIMU ya Barcelona iko tayari kupambana na Chelsea katika mbio za kuwania usajili wa golikipa wa Ajax, Andre Onana mwenye umri wa miaka 23 ambaye ni raia wa Cameroon. ***(Diario Sport - in Spanish)***

### HANA MPANGO NA RAHEEM

KOCHA wa Real Madrid Zinedine Zidane anaamini Raheem Sterling mwenye umri wa miaka 25 wa Manchester City na England ni mshambuliaji mzuri, lakini hafikirii uwezekano wa kumsajili. ***(Goal.com)***

### MAN CITY YAPATA WAKILI

KLABU ya Manchester City imemtafuta wakili ambaye amefanikiwa mara mbili kuzuia mchakato wa Uingereza kujiondoa kwenye Muungano wa Ulaya, kubatilisha uamuzi wa kupigwa marafuku ya kutocheza Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa miaka miwili. ***(Daily Mirror)***

### ARSENAL YAWINDA BEKI

KLABU ya Arsenal inapanga kumsajili beki wa Bayer Leverkusen na Ujerumani, Jonathan Tah ambaye kwa mujibu wa mkataba wake anathamani ya pauni milioni 34. ***(Bild)***

### INTER MILAN YAONGEZA NGUVU

INTER Milan inajipanga kutoa wachezaji kwenda klabu ya Verona kama sehemu ya mpango wa kumnasa beki wa Albania, Marash Kumbulla mwenye umri wa miaka 20, ambaye anawaniwa na Liverpool. ***(Inside Futbol)***

### ALITAKA KUMSAJILI ERIKSEN

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer alikuwa akitaka kumsajili Christian Eriksen, 28, kabla ya raia huyo wa Denmark kuhamia Inter Milan akitokea Tottenham. ***(Manchester Evening News)***

### JUVE, INTER ZAMWINDA EMERSON

KLABU za Juventus na Inter Milan zipo kwenye mbio kuwania kumsajili beki wa pembeni wa Chelsea, Emerson Palmieri mwenye umri wa miaka 25, lakini bado ofa rasmi hazijatumwa, wakala wake abainisha. ***(Goal.com)***

### LUIZ AIPA ARSENAL KOMBE

DAVID Luiz mwenye umri wa miaka 32, anaamini Arsenal wana kiwango cha ubora cha kuwafanya washinde taji la Ligi ya Europa msimu huu, baada ya kushindwa msimu uliopita. ***(Evening Standard)***

HABARI MICHEZO

## Kili Canvas yawa gumzo Moshi

**Na Mwandishi Wetu,** KILIMANJARO

KILI Canvas iliyozinduliwa na Kampuni ya Bia Tanzania (TBL) kupitia bia yake ya Kilimanjaro Premium Lager hivi karibuni jijini Dar es Salaam, imekuwa kivutio kikubwa kwa wakimbiaji mbalimbali wa mji wa Moshi mkoani Kilimanjaro.

Canvas hiyo lengo lake kuhamasisha wakimbiaji wa vitongoji mbalimbali wa Mkoa wa Kilimanjaro katika kuelekea kilele cha mbio za Kili Marathon zinazotarajiwa kufanyika Machi Mosi, 2020 mkoani Kilimanjaro.

Kili Canvas ni picha maalumu iliyochorwa kwa ukubwa ambapo mkimbiaji yeyote akipita karibu yake anapigwa picha na picha hiyo yenye muunganisho wa teknolojia ya kisasa baadaye kumtumia picha hiyo kupitia simu yake ya mkononi. Hata hivyo mkimbiaji anatakiwa kujisajili na kupewa chipu maalumu ambayo anatakiwa kuwanayo kwa maelekezo ya wahusika.

Kwa mujibu wa Meneja wa Bia ya Kilimanjaro, Pamela Kikuli baada ya shamra shamra za maandalizi ya wakazi wa Jiji la Dar es Salaam, Kili Canvas sasa itakuwa mkoani Kilimanjaro mjini Moshi, ambapo wakazi wake watapata fursa ya kupigwa picha kwa teknolojia maalumu ya kisasa na kisha kutumiwa kwenye simu zao.

Pamela alisema zaidi ya nchi 52 duniani baadhi ya wananchi wake wamejiandikisha kushiriki kilele cha mbio hizo na amewataka Watanzania na waandaaji kuhamasishana kushiriki kilele cha mbio hizi za Kili Marathon ambazo kwa mwaka hufanyika mara moja tu.

## Azam kuendelea kuitafuta Simba

**Na Mwandishi Wetu**

PAMOJA na kuambulia alama moja katika michezo miwili kutoka mikoa ya kusini, na wakati huo huo wapinzani wao, Simba wakizidi kupaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu, Azam FC imesema "hatujakata tamaa ya ubingwa".

Juzi, Jumamosi Azam ilikubali kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa Namungo FC kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi matokeo hayo yakija baada ya kuambulia sare ya 1-1 mkoani Mtwara dhidi ya Ndanda FC.

Shukrani kwa Reliants Lusajo aliyeifungia timu yake bao hilo pekee katika dakika ya 60 lililoiwezesha Namungo kufikisha pointi 43 mbili nyuma ya Azam FC iliyopo nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Lakini licha ya kushuhudia wapinzani wao katika mbio za ubingwa, Simba wakizidi kujiimarisha kileleni kufuatia ushindi wao wa mabao 3-1 dhidi ya Biashara United juzi, Kocha Msaidizi wa Azam, Iddi Cheche amesema bado hawajakata tamaa.

"Tumeyakubali matokeo, tunarudi kujipanga kwa ajili ya michezo inayofuata, lakini bado hatujakata tamaa ya mbio za ubingwa," alisema Cheche wakati huu wakizidiwa pointi 17 na Simba kileleni baada ya timu hizo kila timu kucheza mechi 24.

# LUSAJO AMKIMBIZA KAGERE KIMYA KIMYA

**Na Mwandishi Wetu**

HUKU akizidi kuongeza kasi ya mabao kuelekea mbio za kutwaa Kiatu cha Dhahabu cha ufungaji wa Ligi Kuu Bara, mshambuliaji Reliants Lusajo amesema "Namungo" kwanza.

Lusajo juzi alifunga bao lake la 10 kwenye Ligi Kuu msimu huu wakati Namungo FC ikishinda 1-0 dhidi ya Azam kwenye mechi iliyopigwa Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi.

Bao hilo linamfanya Lusajo kuwa nyuma kwa mabao manne dhidi ya mshambuliaji wa Simba, Mnyarwanda Meddie Kagere anayeongoza katika orodha ya wafungaji kwenye ligi hiyo.

**Hata hivyo, akizungumza na Nipashe baada ya mechi hiyo, Lusajo alisema lengo lake ni kuhakikisha timu yake inamaliza nafasi za juu katika ligi hiyo na si ufungaji bora.**

"Lengo ni kuipasha timu yangu kwanza na si ufungaji bora, nataka timu yangu imalize katika nafasi nzuri," alisema.

Ushindi huo wa Namungo ambayo mechi iliyopita iliichapa KMC FC kwa mabao 2-1, unaifanya sasa kufikisha pointi 43, mbili nyuma ya Azam iliyopo nafasi ya pili kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Simba ndiyo ikiyopo kileleni mwa ligi hiyo ikiwa na alama 62 baada ya kushuka dimbani mara 24 kama ilivyo kwa Azam na Namungo.

NDONDO...



Mchezaji wa timu ya Fedha FC, Julius Zowange (kushoto), akimiliki mpira huku akizongwa na wachezaji wa Super Eagle katika mchezo wa nusu fainali ya michuano ya Kombe la Mbuzi, uliofanyika katika Uwanja wa Hospitali ya Kitunda Kivule nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam juzi. Eagle ilishinda mabao 4-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Twiga Stars yarejea nchini*

**Na Somoe Ng'itu,** UTURUKI

KIKOSI cha timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), kimerejea nchini leo alfajiri kikitokea Tunisia huku Kocha Mkuu wa timu hiyo, Bakari Shime akisema wachezaji wake wameimarika kutokana na ugumu wa mashindano waliyoshiriki dhidi ya wenzao wa Kanda ya Kaskazini.

Twiga Stars ilimaliza mashindano ya Kombe la UNAF yaliyomalizika juzi katika nafasi ya pili baada ya kujikusanyia pointi saba wakati Morocco waliofikisha pointi 12 walitwaa ubingwa na nafasi ya tatu ikienda kwa wenyeji Tunisia.

Shime aliliambia Nipashe kuwa wachezaji wake wamepata 'darasa' kubwa kupitia michuano hii na anaamini watatumia vema mbinu walizojifunza kuelekea mchezo wao dhidi ya Uganda na Kenya inayotarajiwa kuchezwa hivi karibuni.

Kocha huyo alisema kuwa amefurahi kuona wachezaji wake wamepata uzoefu zaidi kwa kucheza dhidi ya wenzao wa Kanda ya Kaskazini ambao hukutana mara chache.

"Tumepata mafunzo mazuri kupitia mashindano haya, kuna mazuri pia tumeyaonyesha ambayo tunatakiwa kwenda kuyaimarisha, naamini tumerudi na faida, ingawa inatuuma kuhusu kukosa ubingwa," alisema Shime.

Alisema anafurahi pia ushirikiano ulioonyeshwa na wachezaji kwa wachezaji kila baada ya kumaliza michuano hiyo na anaamini wakipata nafasi ya kualikwa katika mashindano mengine wataonyesha ubora wao.

Mshambuliaji chipukizi wa timu hiyo, Aisha Masaka ambaye alifunga bao la kusawazisha katika sare ya goli 1-1 dhidi ya Tunisia alisema amejifunza mambo mbalimbali kupitia michuano hiyo na anaahidi ataendelea kujituma akipata nafasi hiyo.

"Tunaomba Watanzania wayapokee matokeo ambayo tumeyapata huku (Tunisia), tulipambana katika kiwango cha juu lakini hatukufikia malengo, tunawaahidi hasira zetu zitawaelekea Uganda katika mashindano ya U-17 na Kenya itakapokuja kucheza na sisi Twiga Stars," alisema Masaka.

Kikosi hicho kilianza mashindano ya UNAF kwa ushindi wa mabao 7-0 dhidi ya Mauritania halafu ikawafunga Algeria magoli 3-2 na mechi yake ya tatu ikapoteza dhidi ya Morocco kwa kichapo cha mabao 3-2 na ilimaliza michuano hiyo kwa sare ya bao 1-1.

Twiga Stars itawakaribisha Kenya katika mechi ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (AWC).

# Michezo

Jumatatu Februari 24, 2020
Nipashe



Hazard aipa pigo tena Real Madrid UKURASA 30




Mchezaji wa Manchester United, Bruno Fernandes, akiangushwa na golikipa wa Watford, Ben Foster wakati wa mchezo wa Ligi Kuu ya England uliopigwa uwanja wa Old Trafford nchini England jana. Man United ilishinda 3-0.

# Sare ya Yanga yazua kasheshe Mkwakwani

## ●●● Polisi watuliza hali ya hewa, makocha, wachezaji wagoma kuzungumza baada ya...

**Na Isaac Kijoti,** TANGA

BUNDI wa sare ameendelea kuganda mtaa wa Twiga na Jangwani baada ya jana kutoka sare ya nne mfululizo kwenye mwendelezo wa Ligi Kuu dhidi ya Coastal Union.

**Sare hiyo ilipokelewa kwa hisia tofauti kwa makocha na wachezaji wa Yanga kugoma kuzungumza na waandishi wa habari huku Ofisa Mhamasishaji, Antonio Nugaz akimkunja shabiki mmoja aliyekuwa akiwarekodi.**

Baada ya mechi hiyo, baadhi ya viongozi wa Yanga walionekana kujadili sare hiyo kwa hisia tofauti ndipo shabiki huyo alipoamua kuwarekodi kabla ya kunyang'anywa simu na kuwekwa mtu kati, lakini Polisi waliwahi na kuwatoa nje.

Kabla ya mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa Mkwakwani, Yanga ilitoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Mbeya City, kisha suluhu na Tanzania Prisons mechi zote zikipigwa dimba la Taifa jijini Dar es Salaam.

Baada ya hapo chupuchupu balaa la kupoteza liikumbe Yanga, lakini ikabahatika kulazimisha sare ya bao 1-1 dhidi ya Polisi Tanzania katika Uwanja wa Ushirika mjini Moshi.

Katika mchezo wa jana, Coastal ilizidiwa zaidi kipindi cha kwanza, lakini dakika 45 za mwisho Yanga ilionekana 'kukata pumzi' na wenyeji kuutawala mchezo.

Umakini wa kipa Metacha Mnata ulilinusuru jahazi la Yanga kuzama kutokana na mashuti makali yaliyokuwa yakirindimishwa langoni mwao na Ayoub Semtawa na Ayoub Lyanga.

Licha ya timu zote kufanya mabadiliko katika kipindi cha pili, hayakuweza kubadili matokeo ya mchezo huo ambayo yanaifanya Yanga kufikisha pointi 41 baada ya mechi 22.

Yanga iliwatoa Balama Mapinduzi, Tariq Seif na kuingia Mrisho Ngasa na Ally Mtoni huku Coastal ikiwapumzisha Mudathir na Semtawa na kuwapisha Hija Ugando na Kanduru.

Katika kipindi cha kwanza mpira ulichezwa zaidi langoni mwa Coastal Union na Yanga ilipata jumla ya kona sita dhidi ya moja ya wenyeji.

Hata hivyo, kama ilivyokuwa kwenye mazoezi ya Yanga juzi, ndivyo ilivyotokea jana kwa kikosi hicho cha Mbelgiji Luc Eymael kushindwa kuzitendea haki kona hizo.

Juzi katika mazoezi, Yanga ilikuwa ikifanyia kazi kona na hakuna hata moja waliyofanikiwa kuizamisha kimyani wakiwa mazoezini.

Yanga ilikuwa ya kwanza kufika langoni mwa Coastal, dakika ya kwanza tu, lakini haikuweza kuleta madhara kwa kipa Soudy Dondola wa Coastal.

Jaribio la kwanza na hatari langoni mwa Yanga ilikuwa katika dakika ya 16, lakini kipa Mnata alikuwa makini kuzima mashambulizi ya Yanga.

Umakini wa kipa Dondola wa kulicheza shuti la Bernard Morrison katika dakika ya 32 uliinusuru Coastal kuwa nyuma kwa bao moja.

Shambulizi lingine hatari kwa Yanga ilikuwa dakika ya 45 baada ya Semtawa kuachia shuti kali kwa mguu wa kushoto, lakini Mtacha alikuwa makini kulicheza.

# Sven akoshwa wachezaji kufuata maagizo yake

**Na Saada Akida**

LICHA ya kushinda mbao 3-1, Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck (pichani) amesema sasa anaendelea kutoa mbinu ili kikosi chake kiwe imara.

Simba imeendeleza wimbi lake la ushindi baada ya juzi kuifunga Biashara 3-1 katika mchezo uliopigwa Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Mabao ya Simba yalifungwa na Luis Miquissone dakika ya 35, Meddie Kagere dakika ya 68, Francis Kahata aliyetia mpira nyavuni dakika ya 86.

Akizungumza na Nipashe jijini Dar es Salaam, Sven amesema amefurahishwa kuona vijana wake wamefanyia kazi kile alichowapa katika mazoezi.

Alisema baada ya kushinda bao 1-0 katika mchezo wa Kagera Sugar aliwataka washambuliaji wake kuhakikisha wanapata idadi kubwa ya mabao na wamefanyia kazi maagizo yake.

"Nimeona mabadiliko makubwa, wachezaji wangu wamefanya kazi nzuri na kufuata maelekezo niliyokuwa nawapa mazoezini, sasa tunarudi kwenye maandalizi mengine kwa ajili ya michezo yetu mingine," alisema.



Sven alisema aliona upungufu katika kikosi na sasa atahakikisha anawapa mbinu mpya zaidi nyota wake.

Naye kiungo Mshambuliaji Luis Miquissone alisema amefurahia kufunga bao lake la kwanza ndani ya Simba na malengo yake ni kuisaidia timu yake hiyo kutwaa ubingwa.

Alisema anafahamu mashabiki wanahitaji kuona timu yao inapata matokeo mazuri pamoja na mpira mzuri kutoka kwao.

"Ninafurahi kutupia bao ndani ya Simba, kikubwa ambacho nafikiria ni kuona kwamba ninaipa ushindi timu kwa kushirikiana na wachezaji wenzangu na hilo linawezekana," alisema Luis.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >